# Nipashe

Jumatatu Aprili 6, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580198

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Miili ya watu wanne yatupwa machimboni ikiwa imeharibika

UKURASA 2




UKURASA 13

# WIKI YA KUUMBUKA

**NI** watendaji waliofuja fedha za umma, vigogo wa Jeshi la Polisi kitanzini tena, Spika Ndugai atoa miezi mitatu washughulikiwe...*Endelea ukurasa 2*



## HOFU CORONA

## KKKT YAJIPANGA LIKIZO KWA WATUMISHI

UKURASA 12

Askofu Dk. Dickson Chilongani (aliyeshika fimbo), akisalimiana kwa miguu na mmoja wa waumini, baada ya kutoka kwenye ibada ya misa ya matawi, iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Angalikana Dayosisi ya Dodoma, kutokana na tishio la ugonjwa wa corona. **PICHA: PETER MKWAVILA**



## BAA LA CORONA

Ni salama kupokea kifurushi kutoka eneo lililo ripotiwa kuwa na virusi vya corona (Covid-19)? Uwezekano wa mtu aliyepata maambukizi kusambaza kwenye bidhaa ni mdogo na hatari ya kupata virusi hivyo kutoka kwenye kifurushi ambacho kimetoka, kusafirishwa katika hali ya joto tofauti pia ni mdogo. WHO

* Epuka mikusanyiko ya watu
* Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
* Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
* Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo.

## WAWEKWA KIZUIZINII KUINGIA KWA NJIA ZA PANYA

UKURASA 12




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** **USAJILI 11 BORA LIGI KUU MSIMU HUU** UK.15 **MAONI, KATUNI UK.6**

## Miili ya watu wanne yatupwa machimboni ikiwa imeharibika

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

MIILI ya watu wanne ambao hawajafahamika inasadikiwa kutupwa katika mto kando ya machimbo ya madogo ya dhahabu ya Mwabomba, Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga ikiwa imeharibika na kushindwa kutambulika.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema taarifa za tukio hilo wamezipata jana asubuhi na jitihada za kuopoa miili hiyo inaendelea kufanywa na Kamati ya Usalama ya wilaya hiyo na hadi jana mchana mwili mmoja wa mwanamume ulikuwa umeopolewa.

Macha alisema inadaiwa watu hao waliuawa maeneo ya mbali na kwenda kutupwa katika mto huo huku ikiwa imeharibika na kushindwa kutambulika ni ya kina nani.

Alisema miili mingine wanaendelea kuitafuta kwa kuwa mto huo umejaa maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha na kusababisha kazi hiyo kuwa ngumu.

Katika hatua nyingine, Macha alisema watu watatu wamefukiwa na kifusi kwenye machimbo ya dhababu Mwabomba, Kata ya Idahina halmashauri ya Ushetu baada ya kuporomokewa na matimba ambayo hutumika kama nguzo ya kuzuia ukuta wa shimo la dhahabu wakati wakichimba duara.

Alisema watu hao wamefukiwa tangu Aprili 4, mwaka huu na juhudi za kuwatafuta na kuwaokoa zinaendelea kufanyika kupitia kamati ya usalama ya wilaya hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine wa uokoaji. Hata hivyo, majina hayo bado hayajafahamika.

"Inawezekana namna ya uchepechepe wa udongo na mvua zinazoendelea ndiyo sababu ya matimba hayo kuporomoka na kuwafukia wachimbaji na inasemekana kuna watu watatu," alisema Macha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Deborah Magirigimba, akizungumza kwa njia ya simu amethibitisha kutokea kwa matukio hayo na kusema kuwa uopoaji wa miili ya watu waliosombwa na maji pamoja na kufukua watu waliofukiwa na kifusi unaendelea na kuahidi kutoa taarifa baadaye.



Ofisa wa Shirika lisilo la serikali la Convoy of Hope International Tanzania, Winfrida Roman (kulia), akitoa mafunzo ya kutumia kibuyu chirizi kunawa mikono ili kujikinga na corona, kwa walezi wa vituo vya watoto yatima jijini Arusha, kabla ya kuwakabidhi vyakula vya msaada kwa watoto yatima 530 wa vituo mbalimbali jijini Arusha. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Wiki ya kuumbuka vigogo waliofuja fedha za umma

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

NI wiki ya kuumbuka! Ndivyo ambavyo unavyoweza kuliita juma hili, kutokana na kinachokwenda kufanywa bungeni jijini Dodoma dhidi watendaji wa serikali waliofuja fedha za umma.

Iko hivi: Juma hili litakuwa mahsusi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuwasilisha bungeni ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Hatua hiyo inafuata baada ya Rais John Magufuli kukabidhiwa ripoti hiyo wiki mbili zilizopita na kinachofuata sasa ni ripoti hiyo kuwasilishwa bungeni ili serikali itoe majibu ya hoja mbalimbali za ukaguzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo CAG ni mkuu wake.

Machi 26 mwaka huu, Rais Magufuli alipokea ripoti hiyo Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma, ikigusa maeneo mengi ukiwamo ukusanyaji wa kodi kutoka vyanzo mbalimbali na mashauri ya rufaa za kodi, uandaaji na utekelezaji wa bajeti ya serikali, hali ya Deni la Taifa, usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa mali na madeni ya serikali, na usimamizi na uendeshaji wa taasisi za umma zikiwamo taasisi muhimu za kifedha.

Utaratibu wa kikatiba na sheria iliyoanzisha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, vinamtaka CAG kuwasilisha bungeni ripoti yake ya ukaguzi ndani ya siku saba za mwanzo za Bunge la Bajeti (pasi na kuzihusisha siku za mwishoni mwa wiki na sikukuu).

Bunge la Bajeti lililoanza Jumanne iliyopita, leo linaingia katika kikao (siku) chake cha tano. Kesho ni sikukuu ya Kumbukumbu ya Kifo cha Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume na Ijumaa itakuwa sikukuu (Ijumaa Kuu), hivyo ni lazima CAG Charles kichere atawasilisha ripoti yake bungeni ndani ya siku tatu ambazo ni ama leo, Jumatano au Alhamisi.

Baada ya kuiwasilisha, CAG atakabidhi ripoti yake kwa kamati mbili za Bunge zenye mamlaka ya kuifanyia uchambuzi ambazo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Miongoni mwa hoja zinazotarajiwa kuwa gumzo katika ripoti ya CAG ni madai ya uwapo wa ufisadi katika miradi na wakati wa utekelezaji wa shughuli za taasisi na mashirika ya umma pamoja na 'mchwa' wa fedha za maendeleo katika halmashauri mbalimbali.

Muhtasari wa ripoti hiyo uliotolewa na CAG Kichere kwa Rais Magufuli mwezi uliopita, uliodokeza kuwa ripoti hiyo pia itakuwa na taarifa kuhusu hali ya Deni la Taifa na uhimilivu wake, uwapo wa watumishi hewa na baadhi ya taasisi kulipa mishahara kwa watumishi ambao tayari walishafariki dunia.

Ripoti hiyo, kama zilivyokuwa zilizopita, pia inatarajiwa kutoa taswira halisi ya namna serikali inavyozingatia sheria na sera katika utendaji wake, zikiwamo sera za kodi, elimu na afya.

Katika ripoti ya mwaka 2016/17, kwa mfano, CAG alitoa ripoti ya ukaguzi mahsusi akiangazia hali ya miundombinu ya shule za msingi, hali ya usalama wa majengo ya umma dhidi ya majanga ya moto na hali ya utendaji wa mamlaka za maji nchini.

### MCHWA WA BAJETI

Miongoni mwa hoja zinazotarajiwa kuwa gumzo katika ripoti ya CAG ni madai ya uwapo wa ufisadi katika miradi inayosimamiwa na taasisi na mashirika ya umma na 'mchwa' wa fedha za maendeleo katika halmashauri mbalimbali hasa kwenye miradi ya sekta za maji, elimu na ujenzi.

Hoja nyingine ni kasi ya kukua kwa Deni la Taifa, uwapo wa malipo hewa na hali ya madeni katika mashirika na taasisi za umma.

### UFISADI KATIKA MASHIRIKA

Wakati Rais Magufuli akiingia madarakani mwishoni mwa mwaka 2015, kulikuwa na madai ya kuwapo kwa ufisadi katika taasisi na mashirika ya umma huku kiongozi wa nchi huyo akiamua kuzichukua fedha zao na kuzihifadhi kwenye akaunti maalum iliyoko Benki Kuu (BoT).

Katika Ripoti ya CAG mpya, Kichere, inatarajiwa kuwa na ukaguzi wa suala hilo ili kujua kama kuna mabadiliko ya kiutendaji katika mashirika na taasisi hizo.

### POLISI KITANZINI

Machi 12, 2016, serikali ilianza msako wa watumishi hewa na uhakiki wa vyeti vya watumishi wote wa umma, uhakiki ambao ulikamilika rasmi Machi 31, 2017, lakini serikali ikatangaza kuwa msako huo ni endelevu.

Tayari CAG Kichere ameshadokeza kuendelea kuwapo kwa dosari hiyo, alipomweleza Rais Magufuli wiki mbili zilizopita kuwa, amebaini Jeshi la Polisi limefanya malipo kinyume cha taratibu kwa kulipa mamilioni ya shilingi kama mishahara kwa watumishi ambao ni wafu.

Baada ya kupokea ripoti hiyo, Rais aliagiza mamlaka zote zinazohusika na ushughulikiaji wa hoja za CAG, zifanyie kazi zilizoibuliwa katika ripoti hiyo.

Na katika kikao cha kwanza cha Bunge la Bajeti Jumanne iliyopita, Spika Job Ndugai, aliagiza ripoti ya CAG ishughulikiwe ndani ya miezi mitatu na wahusika wawe wamejibu hoja za ukaguzi kufikia Juni 30 mwaka huu, ambayo ni siku ya ukomo wa Bunge la 11.

Hii si mara ya kwanza kwa Jeshi la Polisi kukumbwa na kashfa. Ripoti zilizopita za CAG zilionyesha kuwapo kwa kashfa nyingine ikiwamo ile ya ununuzi na ufungaji wa vifaa vya utambuzi wa alama za vidole kwenye vituo vyote vya polisi nchini, maarufu kashfa ya Lugumi.

Kashfa nyingine za kifisadi dhidi ya vigogo wa jeshi hilo ni ununuzi wa magari miaka mitatu iliyopita, ambayo Rais Magufuli alifichua kuwa yalikuwa chini ya kiwango na mengine kutoletwa nchini licha ya wahusika kulipwa.

Ripoti hizo pia zililitaja jeshi kuwa miongoni mwa taasisi mbili za serikali zinazoongoza kwa madeni na ununuzi mkubwa nchini. Taasisi nyingine 'inayokula sahani moja' na Jeshi la Polisi kwa kuwa na ununuzi mkubwa na madeni ni Shirika la Umeme (Tanesco).

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAO) ilianzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorejewa mwaka 2005) Ibara ya 143.

Kifungu 2(c) cha ibara hiyo kinaeleza kuwa CAG anatakiwa angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za serikali ya muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa serikali ya muungano na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Ratiba ya shughuli za Bunge wiki hii inaonyesha kutakuwa na kuhitimisha mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka ujao wa fedha utakaofuatwa na mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara mbili zilizopo chini ya Ofisi ya Rais.

## HABARI KITAIFA

# TPSF kutathmini athari za corona kwa uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imeanza kufanya utafiti kwa kutumia kongani zake 14 ili kutathmini ya athari za ugonjwa wa COVID-19 kwenye uchumi wa Tanzania.

Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Angelina Ngalula, alisema Jijini Dar es Salaam kwamyatawasilishwa serikalini ili kuona namna ya kusaidia sekta za uchumi zilizoathiriwa vikubwa na mlipuko huo na kujua hali halisi ya uchumi wa taifa .

"TPSF tunazo kongani 14. Tutaunda timu ya wataalamu wa masuala mbalimbali ili kufanya tathmini ya athari ambazo zimetokana na ugonjwa wa COVID-19. Matokeo ya tathmini hiyo tutayawasilisha serikalini kwa lengo la kufanyiwa kazi hususani kwa sekta ambazo zitakuwa zimeathirika vikubwa," alisema Ngalula. +Kongani hizo ni kilimo, viwanda, utalii, benki na fedha, madini, huduma, wakawake wajasiriamali, wafanyabiashara Zanzibar, ujenzi na uhandisi, mafuta na gesi, usafirishaji, kampuni , biashara na uchuuzi.

Ngalula aliwataka wafanyabiashara na waajiri wasiwe wepesi wa kulalamika wakati huu kwani TPSF, ikishirikiana na serikali, imo mbioni kufanya tathmini ya sekta zote za uchumi, ili kujua kwa kina maeneo ambayo yameathirika sana.

"TPSF ipo mstari wa mbele katika kushirikiana na serikali ili kuona namna nzuri ya kuweka uchumi wa nchi katika hali nzuri," alisisitiza Ngalula na kuongeza kuwa wadau wa sekta hiyo wasijifanyie tathmini zao binafsi na kupeleka malalamiko serikalini.

Kiongozi huyo alisema TPSF inaamini imo katika mwelekeo mzuri katika mapambano na ugonjwa wa COVID-19 kutokana na hatua ambazo zimechukuliwa zikiwamo utoaji wa elimu, kuhamasisha wadau katika utoaji wa rasilimali pamoja na kuweka mazingira mazuri katika kulinda ajira za Watanzania," alisema.

Kongani ambazo zimeonekana kuathirika moja kwa moja baada ya mlipuko wa COVID-19 ni utalii na kilimo, hususani kilimo cha matunda na mboga mboga, hali ambayo imechangia kuyumba kiuchumi kwa kongani hizo.

"Kongani ambazo zimeguswa moja kwa moja ni kwa sababu ya mwingiliano na mataifa mengine ambayo tayari yameweka zuio la watu kusafiri.



Mtoto akiwa amembeba mtoto mwenzake wakipita kwenye kidaraja cha miti, huku pakiwa na mmomonyoko katika mfereji unaopeleka maji katika Mto Mzinga Kitunda Dar es Salaam jana. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# Walikimbia soko kisa hofu ya corona

**Na Francis Godwin**, IRINGA

WAFANYABIASHARA wa Soko la TASAF Ilula mkoani Iringa, wamekimbia kufanya biashara katika soko hilo na kwenda mitaani kwa kile walichotaja kutokuwapo kwa wateja.

Wakizungumza na Nipashe wafanyabiashara hao wamesema wamelazimika kuondoka katika soko hilo kutokana na idadi ndogo ya wateja hivyo wamelazimika kwenda kufanya biashara mitaani ambako kuna wateja wengi.

Soko hilo kwa sasa limesalia na wafanyabiashara wachache ambao walieleza kuwa lengo la kujengewa kwa soko hilo ni kutaka wafanyabiashara wote kufanya biashara ndani ya soko ila sasa ni tofauti baada ya wenzao kukimbia.

Martha Msigwa, mfanyabiashara wa chakula sokoni hapo, alisema changamoto kubwa inayosababisha soko hilo kukosa wateja ni wafanyabiashara waliokuwapo awali kurudi kufanya biashara mitaani.

Alisema hali hiyo imesababisha wateja wote kutofika katika soko hilo na kuhatarisha uhai kwa kukosa wateja waofika kununua bidhaa sokoni hapo.

"Tunaiomba serikali ya mji wa Ilula kuwaondoa wafanyabiashara wanaofanya biashara zao mitaani na wote kuwapo katika soko hilo ili kulifanya soko kuwa hai na Halmashauri kupata mapato yake kupitia soko hilo vinginevyo fedha zilizotumika kujenga soko hilo zitakuwa zimepotea," alisema Msigwa.

Alisema serikali imetumia fedha nyingi kujenga soko hilo ambalo kwa sasa limetelekezwa pasipo kuwa na wajeta na hata meza zake zimeanza kuoza bila kutumiwa.

Thadei Mwitula, mkulima anayefanya biashara katika soko hilo, alisema kuondoka kwa wafanyabiashara ndani ya soko hilo si tu kuna ikosesha mapato Halmashauri bali kunawakandamiza wakulima kwa kuuza mazao yao kupitia madalali.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Yohanes Sarufu, alisema kuwa kutotumika vyema kwa soko hilo kunaikwamisha Halmashauri hiyo kupata mapato yake, hivyo lazima mbinu za ziada itumike kuwakusanya wafanyabiashara ili waweze kutumia soko hilo.

Mkurugenzi Ntendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Aloyce Kwezi, akizungumzia suala hilo alisema soko hilo ambalo lilijengwa kwa ajili ya wafanyabiashara mbalimbali ili kuingezea halmashauri kipato.

Alisema kwa sasa idadi ya wafanyabiashara ndani ya soko hilo si nzuri kwani wengi wao wametoka ndani ya soko hilo na kurejea katika maeneo yao ya asili jambo ambalo linasababisha soko hilo kukosa wafanyabiashara kinyume na malengo ya halmashauri.


## KUMBUKUMBU

**LEO** TAREHE **5/4/2020** UMETIMIZA MIAKA MIWILI (2) TANGU UITWE NA MWENYEZI MUNGU. INGAWA BABA YETU HAUPO NASI KIMWILI LAKINI KIROHO TUPO PAMOJA KATIKA SALA NA MAOMBI. ULIKUWA NGUZO IMARA KATIKA MAISHA YETU,
***HEKIMA NA BUSARA ZAKO TUTAZIKUMBUKA DAIMA.***

TUNAMSHUKURU **MWENYEZI MUNGU** KWA MAISHA YAKO KWETU, HAKIKA PENGO ULILOLIACHA HALITAZIBIKA KAMWE.



**MZEE GERALD MGEUSA NYINGE**
**1939 – 2018**

UTAKUMBUKWA DAIMA NA MKE WAKO ISABELLA; WATOTO WAKO EVANS, REGINALD, LILIAN, ERIC, LEVINA, DEOGRATIUS, ANNACLETUS, IRENE; WAKWE ZAKO NELLY, CAREEN, NASSORO, LEAH, BERTHA, SECILIA; WAJUKUU ZAKO, NDUGU, MAJIRANI NA MARAFIKI ZAKO.

RAHA YA MILELE UMPE EE BWANA NA MWANGA WA MILELE UMUANGAZIE, APUMZIKE KWA AMANI

156901



UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**TENDER CANCELLATION NOTICE**

**Invitation to bid: No. ITB/2020/SUP/002**

**ESTABLISHMENT OF FRAME AGREEMENT(S) FOR THE SUPPLY OF DIESEL FUEL – BULK DELIVERY**

Reference is made to above subject invitation to bid.

Please note that the Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Tanzania, has decided to cancel and withdraw the tender ITB/2020/SUP/002 for Establishment of Frame Agreement(s) for the Supply of Diesel Fuel – Bulk Delivery until further notice. The reason for cancellation of this tender is due to the current situation of **COVID-19 pandemic.**

We appreciate your interest in the tender and your decision to work with us. This is truly a lost opportunity. However, we remain interested in doing business together in future ventures should the occasion arise.

**If you had already submitted your offer, please be advised to come and collect your documents from our offices.**

**Thank you.**

156905

# Serikali kuwanusuru waliozingirwa na maji

**Mwandishi Wetu,** MANYARA

SERIKALI imeahidi kuchukua hatua za haraka kunusuru wakazi wanaozunguka Ziwa Basotu ambao makazi yao yamezingirwa na maji wilayani Hanang mkoani Manyara.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, alitoa ahadi hiyo jana alipotembelea eneo hilo kujionea athari hizo zilizotokana na mvua inayoendelea kunyesha nchini.

Katika ziara hiyo, Zungu aliyekuwa amefuatana na wataalamu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), aliahidia serikali kutumia wataalamu hao kufanya utafiti ili kupata suluhisho la kudumu.

Akizungumza na wananchi wa eneo hilo walioathirika na mafuriko, waziri huyo aliwaahidi kuliweka suala hilo kupitia miradi ya serikali inayotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

"Tumetazama tatizo hili hapa, panahitaji utaalamu mkubwa, tutachukua hatua kwani tunaona eneo lote la ziwa limeingiwa udongo na kufanya maji yafurike na tunaweza kudhani maji ni mengi kumbe wakati wa kiangazi tutakuwa na shida ya maji, kuweni na imani na serikali yenu, tutalifanyia kazi," alisema.

Mkuu wa wilaya hiyo, Joseph Mkirikiti, alisema athari zilizotokana na mafuriko hayo ni uharibifu wa miundombinu ikiwamo nyumba za wakazi wa eneo hilo kuzingirwa na maji.

Mkirikiti aliongeza kuwa kwa takriban wiki tatu sasa, kumekatika mawasiliano kati ya eneo hilo na Haydom kutokana na barabara iliyo kando mwa ziwa hilo kujaa maji.

Aliomba mamlaka zinazohusika, zichukue hatua kwa wakati ili kunusuru wananchi hao wasipate madhara zaidi kutokana na nyumba zao kuzingirwa na maji.

Itakumbukwa kuwa hivi karibu, serikali iliagiza barabara ya Haydom - Katesh isitumike ili kuepusha madhara kwa watumiaji kutokana na kufurika kwa maji hayo. Kaimu Mkurugenzi wa Utafiti na Hifadhi ya Mazingira wa NEMC, Lilian Lukambuzi, alisema tatizo hilo limetokea kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu ziwani.

Lukambuzi alisema panapaswa kufanyika utafiti kama ambavyo waziri alielekeza pamoja na kuweka mipango ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kunusuru ziwa hilo.

Alisema moja ya hatua za haraka zinazopaswa kuchukuliwa ni kuzuia shughuli za kibinadamu zinazofanyika katika maeneo hayo ambazo ndiyo chanzo cha tatizo hilo.

Mbunge wa Hanang, Mary Nagu, alionyesha hofu yake juu ya ziwa hilo kujaa udongo kutokana na mito inayotoka maeneo mbalimbali na hivyo kusababisha uhaba wa maji kwa wananchi wake.

Alimshuruku waziri huyo kwa kufika na wataalamu kutoka NEMC chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na kujionea madhara mbalimbali yanayotokana na kufurika kwa maji na kuwa tayari kuyafanyia kazi.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, Ziwa Basotu ni chanzo kikubwa cha maji kwa wananchi wa Wilaya ya Hanang.



Mhandisi Rasilimali za Maji, Bodi ya Maji Bonde la Kati, Moses Salumbi (kushoto), akiweka alama za ukomo wa maji ya mafuriko kwenye maziwa ya Kindai na Munang mkoani Singida mwishoni mwa wiki. Wengine kutoka kulia ni Mhandisi Ujenzi, Danford Samson, Mhandisi Mazingira, Nyagheri Mramba, Ofisa wa Maji, Bodi ya Maji Bonde la Kati, William Mabula na Ofisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi wa ofisi hiyo, Nelea Bundala. **PICHA: DPTTO MWAIBALE**

# Watakaokaidi tahadhari corona kuwekwa rumande

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, amewataka wakazi wa mkoa huo kuendelea kufuata maelekezo ya Serikali juu ya kujikinga na ugonjwa wa unaosababishwa na virusi vya corona Covid 19 , huku akisema watakaokaidi watapelekwa rumande.

Mndeme alitoa maagizo hayo wakati akizungumza na baadhi ya wafanyabiashara pamoja na wamiliki wa magari ya abiria wa Manispaa hiyo juu ya kujikinga na ugonjwa huo.

Mndeme ambaye alipita kukagua tahadhari zinazochukuliwa na wafanyabiashara hao katika maeneo yao ya biashara, likiwamo eneo la Soko Kuu la Songea, Mazese na stendi kuu ya daladala mjini Songea, alisema kama kila mmoja atachukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo, itakuwa ni rahisi kuepuka kuambukizwa ugonjwa huo.

Katika hatua nyingine, Mndeme aliwageukia watu ambao wanakaidi kutumia vitakasa mikono na kunawa maji wanapoingia katika maeneo mbalimbali ya huduma kuwa watachukuliwa hatua za kisheria, ikiwamo kuwalaza rumande.

Alisema kuna baadhi ya watu wanajifanya ni wababe wasiotaka kutumia vitakasa mikono na kunawa maji kwa sabuni, jambo ambalo halitavumiliwa.

Pia aliwataka madereva daladala na waendesha bodaboda kuacha kuzidisha abiria kwenye vyombo hivyo kwa kuwa kuzidisha abiria ni kosa la kisheria na linaweza kusababisha maambukizi ya magonjwa mbalimbali ukiwamo wa corona.

Pia aliwataka watu wanaoweka vitakasa mikono katika maeneo yao ya kazi kuvitumia vizuri ili visiharibike.

Mwenyekiti wa soko kuu la Songea, Leonadi Chunga, alimhakikishia mkuu huyo wa mkoa kuwa atajitahidi kusimamia taratibu zote walizoelekezwa na serikali kupitia watalaamu wa afya.

## Wivu wa mapenzi wapoteza maisha ya watu wawili

**Na Robinson Wangaso,** MARA

WATU watatu wamepoteza maisha katika matukio matatu tofauti mkoani hapa, wawili wakidaiwa kuuawa kwa wivu wa mapenzi na mmoja kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mara, Daniel Shillah alitoa taarifa hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema, katika tukio la kwanza Elina Felishian (30), mkazi wa mtaa wa Bomani, mjini Mugumu wilayani Serengeti, alipoteza maisha akiwa anapatiwa matibabu kufuatia kupigwa na mume wake kwa kilichoelezwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Alisema Elina alipigwa na mumewe Machi 25, mwaka huu na kufariki Machi 30, baada ya kufukuzwa na mume wake Juma Samweli (32) akiwa amepigwa na kuumizwa na kumlazimu kusafiri akiwa na hali mbaya na alipofika Karagwe akapoteza maisha akiwa anaendelea na matibabu.

Kufuatia tukio hilo, Kamanda Shillah alisema tayari wanamshikilia Samweli na atafikishwa mahakamani upelelelezi utakapokamilika.

Katika tukio la pili, Aneth Daudi (34), mkazi wa kisiwa cha Sozia, Wilaya ya Bunda, ameuawa kwa madai ya kushambuliwa na mpenzi wake Costa Stephano (32), kwa kile kinachoelezwa pia kuwa ni wivu wa mapenzi, wakati akipatiwa matibabu hospitali.

Alisema mtuhumiwa anashikiliwa na polisi na atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika na tayari mwili wa marehemu ulikabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya maziko.

Tukio la tatu lina muhusisha mwendesha bodaboda, Abdallah Elias Mzembe (30) mkazi wa kijiji cha Isaba, wilayani Butiama, aliyefariki dunia kwa kuuawa na watu wasiojulikana Machi 30, mwaka huu na kuporwa pikipiki yake akiwa anakaribia kufika nyumbani kwake.

Watuhumiwa wa tukio hilo wanatafutwa na polisi mkoani Mara na mpaka sasa hakuna anayeshikiliwa na polisi kwa kuhusishwa na tukilo hilo la mauaji.

# Sababu watalii wengi wa ndani Hifadhi Serengeti

**Na Daniel Sabuni,**
SERENGETI.

JUMLA ya watalii wa ndani 1,959,779 wametembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika kipindi cha miaka sita iliyopita kuanzia 2013 hadi 2019.

Imeelezwa kuwa idadi hiyo kubwa imetokana na hifadhi hiyo kuwa na vivutio mbalimbali pamoja na nyumbu wanaohama kila mwaka.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Kitengo cha Utalii na Ofisa wa Uhifadhi Mwandamizi, Tutinaga Mwakijambile, wakati akihojiwa na Nipashe juu ya mikakati ya kukuza utalii wa ndani.

Alisema watalii hao wa ndani 1,959,779 walitembelea hifadhi hiyo kwa vipindi tofauti ambapo mwaka 2013/2014 watalii wa ndani 388,105, 2014/20015 wageni wa ndani 372,917, 2015/2016 watalii 391,675, 2016/2017 watalii 355,815, 2017/2018 wageni 267,562 na 2018-2019 watalii 183,705.

Mwakijambile alisema idadi hiyo imefikiwa baada ya kushawishiwa kwa kutumia mbinu na mikakati mbalimbali za kutangaza vivutio adimu vinavyopatikana katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kupitia maonyesho mbalimbali, radio, majarida,televisheni na uhamasishaji wa mlango kwa mlango katika shule, kapuni ya watu binafsi na Serikali.

Alitaja vivutio vinavyopatikana Senapa ni wanyama wanaohamakutoka Tanzania na kuelekea Masai Mara nchini Kenya kila mwaka, makundi makubwa ya simba, tembo, mbwamwitu na muonekano wa uwanda mpana usio na mwisho kwa upeo wa macho.

Pia makundi ya twiga, mbuni, swala pala, viboko, chui, duma, pimbi, faru, nyati, mito mikubwa ya Grumet na Mara ambayo inatiririsha maji hifadhini na kivutio cha kuruka na puto.

"Vivutio kwenye hifadhi yetu kwa kweli ndivyo vinavuta maelfu ya watalii kuja kujionea, maana kubwa zaidi ni wanyama maarufu watano duniani wanapatikana hapa tena kwa wingi,kama hujawahi kumuona simba, chui na wanyama wengine wengi kwa karibu, asilimia kubwa hapa utamuona tu maana ni wengi...wakati wa nyasi fupi kwakweli watalii huwa wanafurahia utalii," alisema.




Mwenyekiti wa umoja wa wafanyabiashara wazalendo wa kupambana na corona, Abdulaswamad Abdulrahim (alievaa barakoa), akimpa maelezo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Muhamed Aboud (alievaa kofia), wakati akimkabidhi vifaa mbalimbali kwa ajili ya kujikinga na corona. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Askofu aasa waumini kuacha Imani potofu

**Na Hamisi Nasiri,**
TUNDURU

ASKOFU wa Jimbo Katoliki la Tunduru-Masasi, Filbert Mhasi, amesema Watanzania wanatakiwa kutambua njia pekee ya kupambana na ugonjwa wa corona ni kufuata maelekezo ya yanayotolewa na wataalamu wa afya na kumrudia Mungu kwa kufanya maombi kila wakati. Askofu Mhasi aliyasema hayo juzi mjini Tunduru wakati wa ibada ya Misa takatifu ya kubariki mafuta ya Krisma iliyofanyika kanisa kuu la jimbo katoliki la kanisa kuu mjini Tunduru

Alisema licha ya kuwa taarifa nyingi kuhusu ugonjwa wa corona zinawafanya watu kuhisi kuwa na hofu na utamaduni wao, wanapaswa kuwa na matumaini kwamba Mungu ndiye atasaidia kuondoa ugonjwa huo.

Alisema kwa sasa njia pekee ya kuendelea kufanya na kuifuata kila wakati ni kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa Wizara ya Afya kuchukua hatua ya kujikinga na ugonjwa wa corona kwa kunawa mikono kwa sabuni na kuepuka mikusanyiko isiyo na lazima.

Alisema ugonjwa huo tayari umeshaingia nchi nyingi duniani, hivyo Watanzania wasiupuuze kwa kutofuata maelekezo na kanuni za kujikinga ambayo hutolewa na wataalumu wa afya nchini.

Askofu Mhasi alisema kila Mtanzania kwa nafasi yake atumie muda wake kumrudia Mungu na kufanya maombi kila wakati naye atasikia maombi hayo na kusaidia kuangamiza ugonjwa huo.

Askofu Mhasi alisema waumini ambao wanaamini kupakwa kwa mafuta hayo ya Krisma yatawasaidia kutopata kwa ugonjwa huo wa corona ni dhana potofu na kuwataka kuchukua tahadhari zote.

"Haya mafuta mnayopaka hapa msidhani kuwa kwa ajili ya kujikinga na corona, hapana ondoeni kabisa dhana hiyo kama kuna anayefikiri hii leo anapaka mafuta haya eti kwa sababu tu ya kujikinga na ugonjwa huu, hakuna jambo kama hilo tuchukue hatua na kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya na kumuomba Mungu kila wakati," alisema.

Askofu Mhasi aliipongeza serikali kwa kuendelea kupambana pamoja na kutoa elimu kila siku kuhusu hatua za kuchukua na kujikinga na ugonjwa huo.

# Ilemela kinara urasimishaji makazi

**Na Munir Shemweta,**
MWANZA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ilemela Mkoa wa Mwanza, imeendelea kuongoza katika urasimishaji na umilikishaji makazi holela nchini.

Katika utekelezaji wa mpango huo, Halmashauri hiyo imeandaa michoro ya mipango miji 58,000, kupima viwanja 52,000 na kumilikisha jumla ya viwanja 72,000.

Hayo yalibainika jana katika viwanja vya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza wakati wa ugawaji hati miliki za viwanja 1,508 kwa wakazi wa Wilaya ya Ilemela, uliofanywa na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabaula. Mabula ambaye pia ni Mbunge wa Ilemela, alisema ameridhishwa na kasi ya upimaji na umilikishwaji ardhi unaofanywa na wataalamu wa Wilaya ya Ilemela.

"Pamoja na changamoto zote mlizonazo, bado wilaya yetu inaongoza katika urasimishaji, hongereni sana na hata Waziri wa Ardhi amekuwa akiwapongeza mara kwa mara,"" alisema Mabula.

Kupitia mpango huo, Naibu Mabula ameendelea kuzikumbusha kampuni za upimaji zinazotekeleza urasimishaji makazi kutekeleza agizo la Waziri wa wizara hiyo, William Lukuvi, la kukamilisha kazi zote zilizobaki ili kwenda sambamba na kasi ya serikali na kuwaondolea adha wananchi wanaohitaji huduma hiyo.

Ofisa Mipango Miji wa Mkoa wa Mwanza, Degratias Kalemenze, alisema katika kipindi cha miaka ya 1990 mtu yeyote aliyejenga bila kufuata sheria na taratibu alilazimika kubomoa na kujenga upya, tofauti na ilivyo sasa ambapo analazimika kulipia gharama kidogo na kumilikishwa.

Kalemenze aliwasisitiza wananchi kuitumia fursa ya urasimishaji kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ambaye pia ni Ofisa Ardhi na Mipango Miji wa Manispaa hiyo, Shukran Kyando, alielezea changamoto kubwa inayokabili urasimishaji makazi katika manispaa yake kuwa ni kasi ndogo ya wananchi kulipia gharama za urasimishaji.

Hata hivyo, alibainisha kuwa Halmashauri ya Ilemela katika jitihada za kuhakikisha kazi hiyo inafanyika, ameamua kutoa ilani ya siku 30 ya kuwataka wananchi hao kwenda kumilikishwa ardhi yao.

Mmoja wa wananchi aliyekabidhiwa hati, Veronica Byengo, kutoka Mtaa wa Ghana, alimshukuru Rais John Magufuli kwa uamuzi wake wa kuruhusu urasimishaji makazi holela, na kuwaomba wananchi wenzake kujitokeza kumilikishwa ardhi ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.


**CHETI KIMEPOTEA**



115691502

**GRACE ELISAMIA SUMARY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0110-0074** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2012 kupitia ILBORU CENTER. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/291475/2020.**

**KUPOTELEWA NA VYETI**



**EDWARD FIDEL** amepotelewa na vyeti viwili vya sekondari. Cha kidato cha nne chenye Na. CS130360312 cha shule ya sekondari Rwambaizi kilichotolewa mwaka 2013, na cha kidato cha sita chenye **Na. AC160092832** cha Kahororo Sekondari kilichotolewa mwaka 2016.

Vyeti hivyo viliibwa na mtu asiyejulikana, ametoa taarifa polisi na kupewa Na. **KAG/BUK/RB/143011/2020 na Na. KAG/BUK/RB/142559/2020.**
Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa polisi au awasiliane naye kwa namba **0758-632226**

156914

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF ichukue hatua kali wavunjifu zuio corona

**ZIMEBAKI** takriban siku 11 kabla ya zuio la serikali la kusimamisha shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo kumalizika rasmi.

Zuio hilo la serikali lililolitoa Machi 17, mwaka huu liliathiri pia Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kulazimika kusimama ikiwa katika raundi ya 28.

Lengo kubwa la serikali kutoa zuio hilo lilikuwa ni kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19) ambavyo kwa wakati huo vilishabisha hodi nchini kwa mtu mmoja kubainika kuwa na maambukizi.

Hata hivyo, hadi kufikia jana jumla ya watu walioambukizwa nchini walikuwa 20 na mmoja kati yao kupoteza maisha huku wawili wakiwa wamepona na kuruhusiwa kurejea nyumbani.

Na kwa upande wa dunia kwa ujumla virusi vya corona ambavyo Shirika la Afya duniani (WHO), limevitangaza kuwa janga la kimataifa, hadi kufikia jana jioni vilishaua jumla ya watu 65,832, wagonjwa wakiwa 1,217,724 na waliopona 253,744.

Italia ndiyo iliyoathirika zaidi kwa watu 15,362 kupoteza maisha, wagonjwa wakiwa 124,632, ikifuatiwa na Hispania vifo 12,418, wagonjwa 130,759 huku Marekani ikifuata kwa vifo 8,492 na wagonjwa 311,658.

Lakini kwa China ambayo virusi hivyo vilianzia nchini humo katika mji wa Wuhan, yenyewe imefanikiwa kuvithibiti kwa kiasi kikubwa kwani vimeua jumla ya watu 3,329 na hadi jana kukiripotiwa kuwa na wagonjwa wapya 30 na vifo vitatu tu.

Hiyo inaonyesha ni kwa namna gani corona ilivyogeuka kuwa tishio duniani hasa ukizingatia hadi leo bado havijapata tiba wala kinga na vinaendelea kuitesa dunia kwa kuteketeza maelfu ya watu. Hata hivyo, kinachotusikitisha ni kusikia baadhi ya wanachama wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kutotekeleza agizo la zuio lililotolewa na serikali la kusitisha shughuli zote za michezo nchini.

Baadhi ya timu zinadaiwa kuendelea na mazoezi ya pamoja wakati huu ambao TFF ilishazitaka klabu zote kusitisha kambi, mazoezi ya pamoja, ligi na mashindano mbalimbali yalikuwa yakiendelea nchini.

Na kwa kuonyesha mfano, TFF ilianza kwa kuvunja kambi ya timu ya Taifa, Taifa Stars iliyokuwa ikijiandaa na michuano ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) na ile ya michuano ya Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Nipashe kama wadau wa soka namba moja nchini, tumeshtushwa na TFF mwishoni mwa wiki kulazimika kuwakumbusha tena wanachama wake kutii agizo la serikali la kusitisha shughuli zote za michezo katika kipindi chote cha mwezi mmoja ilichotangaza, hiyo ikiwa ni baada ya taarifa ya baadhi kuendelea na shughuli hizo zinazochangia mikusanyiko ya watu.


Ingawa tunatambua ni vigumu kwa mchezaji yeyote anayejitambua na kujali umuhimu wa kazi yake, kukaa bila kufanya mazoezi, lakini kwa kulitambua hilo, si serikali wala TFF iliyotoa katazo la mazoezi binafsi.

Hivyo, huu ni wakati kwa makocha kubuni njia muafaka za kuwasiliana na kuwafuatilia wachezaji wao ikiwamo kupitia mitandao ya kijamii, simu na njia nyingine kama hizo ili kuhakikisha wanafanya mazoezi binafsi bila mikusanyiko.

Hatutaki kuona Tanzania inafikia katika hali ya hatari ya watu kuzuiwa hadi kutoka nje kama ilivyo si tu kwa mataifa ya Ulaya bali nchi jirani za Afrika Mashariki na Kati.

Tunawasihi Watanzania wote kwa ujumla na si wanamichezo pekee, pamoja na kufuata masharti kama ambavyo wizara ya afya nchini inaagiza ili kuepusha kasi ya maambukizi ya corona nchini, pia kuendelea kumuomba Mungu aiepushe Tanzania na kasi ya maambukizi ya virusi hivyo vinavyoitesa dunia kwa sasa na kwa wanachama wa TFF wanaokiuka agizo la serikali, shirikisho hilo liwachukulie hatua kali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Viongozi Yanga, GSM kwa nini mgombee fito?

Na Adam Fungamwango

**NAJUA** kwa sasa suala hili limemalizika, lakini ni lazima lisemwe, liwekwe sawa na kisha kutolewa ushauri ili lisijirudie tena. Mara nyingi kuna mambo yanajitokeza na yanaonekana kumalizika, lakini baadaye yanaibuka tena kutokana na upande mmoja au pande zote kutofuata makubaliano yaliyowekwa kwa pande zote.

Viongozi wa Yanga hivi karibuni waliitisha mkutano wa waandishi wa habari na kueleza kuwa tofauti zao na GSM zimemalizika na sasa wote wako kitu kimoja.

Hii ilitokana na kuibuka kwa sintofahamu kati ya baadhi ya viongozi wa Yanga na wadhamini wao GSM uliosababisha baadhi ya viongozi wa Kamati ya Utendaji ndani ya klabu hiyo kuenguliwa madarakani na wengine kujiuzulu. Wimbi hili lilitokana na wanachama wengi wa Yanga kuwajia juu viongozi wao kuwa wanamzuia mdhamini wao, Kampuni ya GSM kufanya kazi yake kwa ufanisi na kuwataka wachukua hatua za kinidhamu kwa wote waliohusika, la sivyo viongozi wa ngazi ya juu wataubeba msalaba huo.

Wanachama na mashabiki wa Yanga walikuja juu baada ya Kampuni ya GSM kuandika barua ya kujitoa kwenye masuala yasiyo ya kimkataba wa udhamini wao ndani ya klabu hiyo. GSM, imekuwa ikitoa mishahara kwa baadhi ya wachezaji na kusajili pia, kutoa posho na mambo mengine ambayo awali hayakuwa kwenye mkataba baina ya pande hizo mbili.

Wanachama na mashabiki wa Yanga, wakajua fika kuwa kama GSM wakijiweka kando kwenye masuala hayo, basi timu itarejea kule kule kwenye kusajili wachezaji wa kuungaunga, na hata mishahara ya wachezaji kuwa shida, huku yote hayo, mwisho wake hata ushindi kuupata kwa tabu.

Kilichoonekana hapo ni mgongano wa kimadaraka na si kitu kingine chochote kile na kwa vile tayari viongozi wa Yanga na GSM wameshapatana, inabidi sasa wawekeane mipaka kwenye ufanyaji kazi ambao vile vile uwe ni wa kushirikiana.

Kwa upande wao viongozi wa Yanga, waliona kitendo cha mdhamini wao kujichukulia jukumu wa kusajili mwenyewe bila wao kushirikishwa au wao kufanya kazi hiyo ni kama kuwadharau au kuwapoka madaraka yao.

Wanaona kuwa wao ndiyo wana mamlaka kikatiba kufanya kazi hizo za klabu na mdhamini afanye kazi zake zilizomo kwenye mkataba.

Tukienda kwa upande wa pili, tatizo ni kwamba viongozi wengi wa klabu za Kibongo hawaaminiki.

Nafikiri GSM iliona kama ikiwapa moja kwa moja pesa kwa ajili ya kusajili wachezaji, basi kuna baadhi ya viongozi watapiga panga kwa lugha ya kimichezo, lakini kwa ile ya kawaida ni kwamba mchezaji hazimfikii zote.

Sasa hapa kwa sababu wameshapatana na kuwa kitu kimoja kinachotakiwa ni kukaa na kuangalia ni utaratibu gani utatumika ili pande zote mbili zihusike kwa wakati mmoja kwenye masuala ya usajili na hata yale ambayo yapo nje kimkataba.

GSM na viongozi wa Yanga inabidi washirikishane kwa mambo yote ambayo yanataka kufanyika siyo mmoja wanamficha mwenzake, au kila upande unafanya mambo kivyake wakati wote lengo lao ni moja tu, kusukuma gurudumu la Yanga mbele.

Haileti picha nzuri, wote wanajenga nyumba moja, lakini wananyang'anyana fito. Kila mmoja afanye kazi yake. Viongozi wafanye kazi yao ya kuongoza klabu na GSM afanye kazi yake iliyo ndani ya mkataba.

Na chochote kile ambacho kiko nje ya mkataba na kina manufaa kwa Yanga, ni lazima GSM iwaite viongozi wa Yanga na kuwashirikisha na kufanya maamuzi kwa pamoja, ili kila mmoja ajione ni sehemu ya mafanikio. GSM waone pesa yao imetumika kama ilivyopangwa na haijachakachuliwa, huku viongozi nao wakipewa hadhi yao ya kusajili wachezaji kama ilivyo kawaida.

Haya yakizingatiwa, basi pande zote zitafanya kazi bila migongano, lakini yakipuuzwa, ipo siku isiyo na jina, mambo yanaweza kuvurugika tena na hali kuwa mbaya zaidi.

## MJADALA & BARUA

# Wastaafu wanahitaji maboresho

**Mhariri,**

*NCHINI kwetu ni kawaida kuona watumishi ambao baada ya kustaafu, wanakuwa na maisha magumu. Kuna kilio cha kutotosheka na maslahi ya pensheni wanazopewa, hata kukidhi mlo na mahitaji ya lazima ya kila siku.*

*Vijana walioko kazini wakiona wazazi wao iwe baba na mama au babu na bibi wanavyonyanyasika na mara kwa mara maisha duni, daima si kishawishi sahihi kwao katika maisha ya kila siku.*

*Nashauri kwamba, kuna haja kubwa ya kuona namna ya kuandaa maslahi bora kwa wastaafu hawa wapige hatua kimaisha katika zama hizi pia tukiwa katika harakati za kusaka maendeleo yetu.*

**Samson S. Kissenge**
**S.L.P 94**
**Usangi - Mwanga**

# Mafuriko barabara ya Nyerere balaa

**Mhariri,**

*Katika siku kadhaa ambazo mvua zinayesha jijini Dar es Salaam, kuna jambo huwa naliona. Maji yanajaa sana katika barabara kuu ya Nyerere, kati ya eneo la Sido na stesheni ya Tazara.*

*Ni mafurko yanayoanza katika eneo la mfereji wa kutiririsha maji machafu, mafuriko haya yakiwa ni kiashiria kuhitaji hatua zichukuliwe, ikitiliwa maanani yanachukua umbali mrefu.*

*Barabara ya Nyerere ni kubwa, ya heshima na inatumiwa na magari mengi, ikianzia na yote yaendayo katika Uwanja wa Ndege wa Nyerere na maeneo kama Buza, Gongolamboto na vitongoji vyake, Pugu na Kisarawe.*

**Mwasha Shabani,**
**Ukonga Madafu, Dar es Salaam.**


**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz


# Ligi Kuu Bara inavyonukia kugeuka bonanza la vitambi




**Na Adam Fungamwango**

**WACHEZAJI** karibia wote duniani kwa sasa wapo majumbani kutokana na Ligi Kuu na michuano yote ya mpira wa miguu kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

Makocha wengi duniani wameonekana kuimba wimbo mmoja tu kuwataka wachezaji wao wanapokuwa majumbani kufanya mazoezi ya kuweka miili yao sawa.

Hili ni jambo la msingi sana kwa sasa, kwani hawajui ni lini serikali zitaruhusu tena michezo kuendelea baada ya kuona tishio la corona limepungua au kumalizika kabisa.

Ni jambo la hatari sana kwa timu yoyote ambayo itajikuta mechi zimeruhusiwa, lakini wachezaji wake wamerejea wakiwa hawako fiti, au wamekuwa na vitambi kutokana na kukaa nyumbani bila mazoezi.

Kwa wenzetu Ulaya sina wasiwasi sana kwa sababu kwanza wachezaji wao wengi wanajitambua na majumba yao yamekamilika kwa upande wa vifaa vya mazoezi na eneo la kujifua.

Kule watu wanaishi kwa sababu ya mpira, hawana muda wa kumtunza mtu hata kwa kumuweka kambini wiki nzima, badala yake mchezaji anajitunza mwenyewe. Kwa hili janga la corona, kama wameambiwa kuwa wajitunze wenyewe, wachezaji wa Ulaya na mataifa mengine ambao wanajitambua pamoja na kwamba wako nyumbani, lakini wanajua nini wafanye, waishi vipi wakiwa nyumbani, muda gani wa kufanya mazoezi, kula, wale nini, wanywe nini, kwa muda gani, walale saa ngapi na mengine yanayofanana na hayo.

Yeyote atakayekiuka agizo hilo kama akirejea klabuni akiwa kama meneja, basi klabu za huko wala hazikopeshi, zitamsugulisha benchi ili kuwa fundisho kwa wengine siku nyingine.

Lakini pia nafasi yake itachukuliwa na mtu mwingine aliyekuwa anakaa benchi na kuombea ni lini atapata uwanjani ili aonyeshe kitu alichonacho.

Tatizo linaweza likawa kwa wachezaji wetu hapa Tanzania. Wengi wao kama inavyojulikana siku zote hawajalelewa kwenye misingi ya soka. Hawajaandaliwa kuwa wanamichezo tangu wakiwa wadogo.

Wengi wamekuwa wachezaji kwa bahati mbaya. Hawakuruhusiwa kucheza mpira na wazazi wao kwa kuhofia kuumia, kuvunjika viungo na kuathiri masomo yao.

Lakini baadaye mambo yanapokuwa mabaya, labda kwenye uchumi nyumbani na kushindwa kusomeshwa, wengi wanaanza kurejea tena kwenye soka wakiwa na miaka 19 hadi 23, kitu ambacho kinawafanya washindwe kutambua vitu ambavyo hawakuvipitia hasa jinsi gani ya mchezaji anavyotakiwa kuishi.

Matokeo yake wanapoanza kupata pesa na maisha yao kubadilika, nao pia tabia zinabadilika na kuendeleza starehe na vitu vingine ambavyo ni mwiko kwa mchezaji. Napatwa na wasiwasi kama wachezaji wengi wa Kibongo wanaweza kukaa nyumbani na kufanya mazoezi inavyotakiwa, kutofanya starehe zisizokuwa na maana, lakini pia hata kuepuka aina fulani ya vyakula.

Nina wasiwasi kwa sababu nchi zingine hata Ulaya wanakaa ndani, lakini kwa Wabongo wao wanatembea tu ingawa kwa tahadhari, lakini hii inaweza kuwapa fursa wachezaji wasiojitambua kuzurura badala ya kufanya mazoezi.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, ameshawapa maagizo wachezaji wake jinsi ya kujitunza na akawaambia waepuke sana kula vyakula vyenye sukari kwa sababu pamoja na matatizo mengine ya kiafya vinaongeza uzito kwa mlaji.

Juma Abdul, mchezaji wa Yanga, amesema wao wameshauriwa kuacha kula vyakula vya mafuta mengi ili kuepuka kuongezeka uzito.

"Tumeshauriwa kuacha vyakula vya mafuta kama vile chips kuku, pia kutokula wali mara kwa mara kwa sababu ya kuepuka kuongezeka uzito ghafla," alisema.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola amesema wachezaji ambao watashindwa kufuata maagizo ya makocha wao watakuwa wanarudisha nyuma maendeleo ya klabu zao kwa sababu wao ndiyo wanaocheza na si makocha.

"Iwapo ligi itarejea na wao hawajafanya mazoezi ya kutosha na kutofuata masharti ya jinsi ya kuishi na vyakula, itakuwa ni kazi nyingine ya makocha kuanza upya na zitakuwa zimebaki mechi chachetu," alisema kocha huyo. Kwa maneno ya Matola ni kwamba kuna timu zinataka kuchukua ubingwa, zingine kutoshuka daraja na zingine kutwaa Kombe la FA, hivyo kama wachezaji watarejea wakiwa na vitambi na mechi zitachezwa kama bonanza, kuna uwezekano mechi zisiwe za kuvutia na ufundi, lakini pia kupatikana kwa matokeo yasiyotarajiwa kutokana na kwamba wachezaji wengi hawako fiti.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Corona yabadili utaratibu kumbukumbu ya Karume

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mohamed Aboud Mohamed, amesema maadhimisho ya kumbukumbu ya marehemu Abeid Amani Karume kwa mwaka huu yatatekelezwa kwa namna nyingine, tofauti na ilivyozoeleka kutokana na kuwapo kwa ugonjwa wa virusi vya corona.

Katika taarifa aliyoitoa jana kwa vyombo vya habari, Aboud Mohamed alisema ifikapo siku ya kumbukumbu ya marehemu Abeid Karume Aprili 7, kutakuwa na dua maalumu katika eneo la kaburi lake Kisiwandui.

Alisema tukio hilo litahudhuriwa na idadi ndogo ya viongozi watakaoongozwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, na viongozi wa dini wakati wa asubuhi.

Alisema idadi maalumu ya wanafamilia wataandaliwa utaratibu wa kwenda kuomba dua wakati wa jioni, shughuli zote zitasimamiwa na wataalamu wa afya ili kuzingatia taratibu za kukinga maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona kwa watakaokuwapo eneo hilo.

"Kutokana na agizo la serikali la kuepuka mikusanyiko ya watu katika shughuli mbalimbali ili kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona kwa mwaka huu, shughuli zinazohusiana na maadhimisho ya wiki ya kuwaenzi viongozi wakuu wa kitaifa na kumbukumbu ya marehemu Abeid Amani Karume hazitatekelezwa kwa utaratibu tuliouzoea," alisemaAboud Mohamed.

Aidha, Aboud Mohamed aliwasihi wakazi wa Zanzibar kuendelea kuchukua tahadhari na maelekezo yanayotolewa na viongozi na wataalamu wa afya juu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.




Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kivukoni, jijini Dar es Salaam, Sharik Choughule, akikabidhi ndoo na sabuni za kunawia mikono kwa viongozi wa Shina la CCM la Kivukoni, Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yaombwa kuondoa VAT vifaa vya maji

**Na Francis Godwin,**
IRINGA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Rural Development Organization (RDO), Mufindi na Kilolo, mkoani Iringa, limeomba serikali kuondoa ongezeko la thamani (VAT) katika vifaa vya maji na vingine vinavyotolewa msaada na wahisani kwa ajili ya kusaidia kutatua kero ya maji kwa wananchi wa vijiji vya wilaya hizo ambao hawajawahi kuwa na majisafi ya bomba. Akizungumza jana, Mkurugenzi wa Shirika RDO, Fidelis Filipatali, alisema pamoja na ushirikiano mkubwa kati ya Shirika hilo na serikali ya Mufindi, Kilolo na Mkoa wa Iringa kuhudumia wananchi, wanaomba uendelee na kwenye vikwazo vitatuliwe.

Filipatali alisema, Shirika hilo linasaidiwa na wakulima wa Austria ambao wamejichanga na kusaidia miradi mbalimbali ikiwamo ya maji na elimu ya ufundi kwa watoto wa wananchi wasio na uwezo kuendelea na elimu ya sekondari, hivyo wameiomba serikali kuondoa VAT hiyo.

Shirika hilo lilianza mwaka 2002 likiwa linajishughulisha na kilimo bora na endelevu chini ya Jumuiya ya Kilimo Bora kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kilimo endelevu na kutunza mazingira kupitia makontua.

Alisema Shirika la Maendeleo Vijijini (RDO), lina ofisi kuu katika kitongoji cha Lyovela, Kijiji cha Ikanga, Wilaya ya Mufindi, linatoa huduma katika wilaya ya Mufindi na Kilolo katika maendeleo ya vijijini. Alitaja vijiji vinavyopatiwa huduma kwa Wilaya ya Mufindi kuwa ni Ibwanzi, Mafinga, Malangali, Luhunga (Village Centre), Wakati Wilaya ya Kilolo ni Lulanzi na Isele.

Alisema shughuli zinazofanywa ni mradi wa kusaidia watoto yatima na wenye mazingira hatarishi, kutoa huduma ya mahitaji muhimu ya nyumbani kama mafuta ya kula, sabuni, mafuta ya kupaka, blangeti, mavazi na magodoro inapobidi. Pia, alisema shirika linatoa huduma ya mahitaji ya shule kama ada na michango mingine ya shule daftari, sare za shule, peni, penseli, daftari kubwa na viatu, gharama za ujenzi wa nyumba kwa familia zisizokuwa na kaya ama familia zenye nyumba mbovu na gharama za matibabu na chakula kama huduma za dharura.

## Mkakati kusukuma kesi za jinai waanza

**Na Innocent Kansha**

KAMATI ya Taifa ya Mahakama Kuu ya Tanzania ya kusukuma mashauri ya Jinai, imefanya kikao chake cha kupitia maendeleo ya kesi za jinai ambazo hazijakamilika kusikilizwa ndani ya siku 60 na zaidi, ili kutambua sababu za ucheleweshwaji na kuchukua hatua stahiki za kiutawala kuharakisha usikilizwaji wa mashauri hayo.

Akifungua rasmi kikao hicho katika Kituo cha Mafunzo na Habari kilichopo Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu,Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Bennhaji Masoud, aliwataka wadau wote wa haki jinai kutambua mchango wao wa moja kwa moja kupunguza msongamano na kuweka mazingira wezeshi ya utoaji haki.

Aidha; Jaji Dk. Benhajj aliwataka pia wadau wa kikao hicho kuendelea na wajibu wa utoaji haki kwa wote na kwa wakati licha ya changamoto ya ugonjwa wa corona. "Ugonjwa huu ni changamoto ambayo hatuna budi kuikabili kwa kutumia njia mbadala za usikilizwaji wa mashauri mahakamani ili kuondosha mlundikano wa mashauri na msongamano usio wa lazima," alisema Jaji Benhajj.

Jaji huyo aliwataka wajumbe wa kikao hicho kushughulikia changamoto zilizopo kwa ngazi ya kitaifa na kuwataka wadau wa Haki Jinai kutoa ushirikiano wa dhati kufanikisha azma ya kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani hasa kwa ngazi ya mikoa na wilaya. "Matumizi ya tehama kwa Mahakama na wadau hayakwepeki hasa katika kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona vinavyosambaa kwenye mazingira ya msongamano... kuna haja ya mahakama na wadau wake kuongeza jitihada ambazo zilishawekwa kupitia kanuni za kusajili mashauri kwa njia ya mtandao 'E – Filing System' kupitia Gazeti la Serikali toleo na 148 la mwaka 2018," alieleza.

Aliongeza kuwa Mahakama haiwezi kutimiza jukumu lake peke yake bila kuwapo na ushirikiano wa wadau wa haki jinai katika kutoa ushauri na mwelekeo wa maagizo mbalimbali ya ngazi za juu, changamoto kwa mahakama na husunani kwa kamati hii ili kutafakari na kushauri namna bora ya kusukuma mashauri na kupunguza mlundikano.

Nae, Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Sharmilla Sarwatt, alisema lengo la kikao kazi cha kusukuma mashauri ni kujadili namna ya kuendesha na kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani hasa katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona.

Sarwatt alizitaja mbinu za kupunguza mashauri mahakamani ni kuendesha mashauri ya jinai kwa njia ya mtandao, utaratibu wa kupanga muda wa kusikiliza kesi ili kuondoa msongamano usio wa lazima mahakamani na pia kusajili kesi mahakamani pindi upelelezi unapo kuwa umekamilika.

Mkurugenzi Msaidizi Upelelezi Makosa ya Jinai nchini, Charles Kenyela, alipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kushirikisha wadau wa haki jinai ili kutatua changamoto na kutafuta namna bora ya uendeshaji wa mashauri hasa katika kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona.

HABARI KITAIFA

# H/shauri yaagizwa ujenzi shule kidato cha tano, sita

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKUU wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Deodatus Kinawiro, ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba kuhakikisha ifikapo Julai, mwaka huu shule za Rubale na Ryamahoro ziwe zimeanza kutoa elimu ya kidato cha tano na sita.

Lengo ni kuwezesha watoto wanaofaulu kidato cha nne kupata nafasi za kutosha kuendelea na masomo.

Alitoa maelekezo hayo katika kikao cha baraza la madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, ambayo inakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na shule hata moja inayotoa elimu ya kidato cha tano na sita.

Shule za sekondari za Rubale na Ryamahoro ambazo zinatoa elimu hadi kidato cha nne, zimechaguliwa na madiwani wa Halmashauri ya wilaya hiyo kuboresha majengo yake ili zianze kutoa elimu ya kidato cha tano na sita.

"Tunazalisha watoto wa kujiunga na kidato cha tano kila mwaka, lakini hatuna shule... haya ni maelekezo, tutumie muda tulionao tufanye kila jitihada ili shule hizi mbili zilizochaguliwa kufikia Julai zianze kutumika kwa lengo la kuongeza nafasi kwa watoto wetu wanaohitimu kidato cha nne," alisema.

Alisema shule kongwe za sekondari zenye kidato cha tano na sita za Nyakato, Kahororo, Rugambwa na Ihungo zilizoko katika wilaya yake yenye halmashauri mbili ambazo ni manispaa ya Bukoba na Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba zipo tangu zamani, lakini zinasimamiwa na serikali kuu, hivyo halmashauri zinatakiwa kujenga shule nyingine zilizoko katika mamlaka zake.

Alisema Manispaa ya Bukoba ina shule moja tu inayosimamia ya Kagemu sekondari, ambayo inatoa elimu ya kidato cha tano na sita, wakati Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba hakuna shule yoyote.

Aliwataka madiwani kuanzia sasa kuweka nguvu katika shule hizo ili zifikie viwango na wataalamu wafike kuzikagua ili Julai zianze kupokea wanafunzi wa kidato cha tano.

Alisema kutokuwa na shule hizo ni tatizo kubwa maana nafasi za wanafunzi zinakuwa chache hata kama mwanafunzi ana alama nzuri, bado anabaki kwa kuwa hana shule ya kwenda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Solomon Kimilike, alisema halmashauri hiyo ina kata 29 na kila kata ina shule ya sekondari ambayo inaishia kidato cha nne, hivyo zikipatikana angalau shule mbili zenye kidato cha tano na sita, zitakuwa mkombozi kwa watoto wanaohitaji kuendelea na masomo.



Gari ndogo aina ya IST yenye namba za usajili T. 785 DBM, ikitolewa ndani ya bwawa la maji, baada ya kuangukia humo na kuua watu wanne waliokuwa ndani ya gari hilo, katika barabara ya Oldshinyanga-Bubiki hadi Mwanza, PICHA: MARCO MADUHU

# OUT yawakumbuka waathirika mafuriko

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT) Tawi la Iringa, kwa kushirikiana na serikali ya wanafunzi wa chuo hicho, wametoa msaada wa vitu mbalimbali kwa wakazi wa Kitongoji cha Mbingama katika Kijiji cha Isele Wilaya ya Iringa walioathirika na mafuriko katika taarafa ya Pawaga.

Hivi karibuni, Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, aliwataka wakazi wa Kitongoji cha Mbingama ili kuepukana na mafuriko, ambayo yamekuwa yakiwasababisha anguko la kiuchumi, afya na maendeleo.

Akizungumza baada ya kutoa msaada hiyo kwa Kasesela kwa niaba ya waathirika hao, Mkurugenzi wa OUT Kituo cha Iringa, Dk. Bukaza Chachage, alisema wameguswa na tukio hilo na kuamua kuchangishana kama watumishi wa chuo kwa kushirikiana na serikali ya wanafunzi na kutoa vitu mbalimbali, zikiwamo nguo na mashuka.

Alisema pamoja na kufanya utafiti mbalimbali kama taasisi ya elimu, pia wanatoa kwa jamii zinapopata matatizo na kuziomba taasisi mbalimbali zilizopo Iringa na watu binafsi wajitokeze kusaidia jamii zinapopata majanga pamoja na kufanya kazi za jamii.

Dk. Chachage aliogeza kuwa wameitikia wito wa DC Kasesela wa kuwataka watu mbalimbali wajitokeze na kusaidia waathirika wa mafuriko yanayotokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

"Tumeitikia wito wa DC Kasesela wa kutaka jamii kusaidia wakazi hao ambao nyumba zao zilibomoka na kuomba vifaa kwa ajili ya kuzijenga baada ya kuhamishiwa makazi mapya," alisema Dk. Chachage.

Kwa upande wake, Kasesela aliishukuru OUT kwa kutoa msaada huo, na kuomba taasisi na watu binfsi kujitokeza kusaidia jamii zinapokumbwa na matatizo.

Alisema zaidi ya kaya 200 zimeachwa bila ya makazi, na kwamba ili kuepukana na mafuriko ya kila mwaka, lazima wananchi wahame katika kitongoji hicho, ambacho kimekuwa kikipata mafuriko ya mara kwa mara.

# Benki ya Stanbic yateua Mkurugenzi Mkuu mpya



**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania, imemteua Kevin Wingfield (pichani) kuwa Mkurugenzi Mkuu kuanzia Aprili 1, mwaka huu.

Wingfield anachukua nafasi ya Ken Cockerill, ambae ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Standard Bank nchini Lesotho.

Safari ya Wingfield ilianza mwaka 1998, katika taasisi ya Standard Bank Group, na mpaka sasa ana uzoefu wa zaidi miaka 20. Wingfield ameshika nyadhifa mbalimbali ndani ya taasisi hiyo ikiwamo; Mkurugenzi wa maendeleo ya kimkakati kwa wateja, huduma za kibenki za watu binafsi na biashara - Standard Bank Africa; Mkurugenzi wa huduma za kibenki za watu binafsi na biashara - Standard Bank Ghana; na Mkurugenzi wa huduma za kibenki za watu binafsi na biashara - Stanbic Bank Uganda.

Katika wadhifa wake huu mpya, Wingfield anategemewa kuongoza ukuaji wa benki, na kuendeleza ubunifu na uvumbuzi ambao utawezesha mafanikio ya kifedha ya watu na biashara nchini Tanzania. Pia kuunga mkono mpango wa kukuza uchumi kupitia uwekezaji katika viwanda na uboreshaji wa miundombinu.

Akizungumza juu ya uteuzi huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Stanbic Tanzania, Prof.. Mark Mwandosya, alisema: "Wingfield ana wito wa uongozi, taaluma na uzoefu ambao ameupata kwa kufanya kazi katika masoko mbalimbali barani Afrika. Tunaimani kwamba chini ya uongozi wake, benki hii itaendelea kukua na kuchangia maendeleo ya nchi yetu."

# Mchungaji aomba punguzo la bili za maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MCHUNGAJI wa Kanisa la IEAGT International la Shinyanga Mjini, David Mabushi, ameiomba Serikali kutoa tamko la kupunguza bili za maji, ili wananchi wa hali ya chini wamudu kulipia gharama za maji.

Aidha amesema hatua hiyo itasaidia wananchi kujikinga na maambukizi ya virusi vya homa ya corona.

Mabushi alibainisha hayo jana kanisani hapo kuwa njia mojawapo ya kujikinga na janga la corona, ni kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka.

Alisema katika kipindi hiki cha tahadhari dhidi ya maambukizi ya corona, wananchi wanatumia maji sana kujikinga, hivyo kuna haja kwa Serikali kutoa tamko la kupuguza bili za maji, ili wamudu kulipa bili hizo na kuendelea kupata huduma ya maji.

"Tunaiomba Serikali itoe tamko la kupunguza bili za maji, kwa sababu kuna uwezekano baadhi ya wananchi hasa wa hali ya chini wakashindwa kulipia bili hizo, na kusababisha ongezeko la maambukizi ya virusi vya corona," alisema Mabushi.

"Nampongeza pia Rais wetu John Magufuli kwa kuruhusu ubada ziendelee, kwa sababu janga hili la maambukizi ya corona, bila kumtanguliza Mungu hatuwezi kupona," aliongeza.

Pia aliwataka waumini wa kanisa hilo kutii maagizo ya Serikali, kwa kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia sabuni na maji tiririka, kutoshikana mikono, pamoja na kupiga chafya kwa kujifunika.

Naye Mwenyekiti wa umoja wa wanawake wa kanisa hilo, Christina Yohana, aliwataka wanawake kuwa mstari wa mbele kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya corona,

# Mikoa 12 yapewa jukumu uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameitaka mikoa 12 ifikapo Septemba mwaka huu iwe imeandaa na kuzindua miongozo ya fursa za uwekezaji kama mikoa 14 mingine ilivyofanya.

Mikoa ambayo imezindua miongozo ya fursa za uwekezaji ni Ruvuma, Songwe, Pwani, Lindi, Kagera, Mtwara, Geita, Kilimanjaro, Simiyu, Manyara, Dodoma, Mwanza, Kigoma na Morogoro.

Akiwasilisha hotuba ya bajeti ya ofisi yake, Mjalowa ameitaka mikoa hiyo 12 kutenga maeneo ya uwekezaji ili kuhamasisha na kuvutia uwekezaji.

Waziri Mkuu alitoa maelekezo hayo wakati akiwasilisha bugeni jijini hapa hotuba ya bajeti ya ofisi yake kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021.

"Tunapokuwa na miongozo wa uwekezaji katika mikoa yetu inarahisisha uhamasishaji na kumvutia mwekezaji kuja nchini na kufanya uwekezaji ambao utakuwa na tija kwa taifa," alieleza Majaliwa.

Alisema kwamba Tanzania kijiografia na kibiashara iko sehemu nzuri na kuna kila sababu ya kuandaa miongozo yenye kuainisha fursa za uwekezaji zilizopo katika mikoa na kutenga maeneo ya uwekezaji.

Miongozo hiyo itachochea uwekezaji nchini.

"Kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara jumla ya mikoa 14 ndiyo iliyokwishazindua miongozo ya fursa za uwekezaji. Hivyo ni lazima mikoa iliyobaki iandae miongozo hii ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kujitangaza kimataifa kupitia fursa zilizopo nchini," alisema na kuongeza:

"Miongozo ya fursa za uwekezaji za kila mkoa zitawekwa katika tovuti ya Kituo cha Uwekezaji Nchi (TIC) ili kuzitangaza ndani na nje ya nchi," alisema. Amesema TIC ina jukumu la kuhamasisha na kutangaza vivutio vya uwekezaji na kufafanua kwamba miongozo hiyo itaongeza kasi ya wawekezaji kuja Tanzania na kuwekeza katika meneo ya vipaumbele vyao.

"Kupitia TIC tumeandaa kitengo cha huduma mahala pamoja'one stop centre' chenye watendaji kutoka Taasisi 10 ambao wameendelea kutoa huduma za muda mfupi kwa wawekezaji wetu kupitia Kituo hicho," alisema. Ameliambia Bunge kuwa hadi kufikia Februari 2020, jumla ya miradi 146 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,514.57 imesajiliwa na inategemewa kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 26,384.

"Endapo tutafanikiwa kuandaa miongozo ya fursa za uwekezaji nchini na kuweka katika tovuti ya TIC idadi ya miradi ya uwekezaji itaongezeka zaidi hii ikiwa ni pamoja na maboresho ya mazingira ya biashara yanayoendelea kufanywa na serikali," amesema Majaliwa



Mkuu wa Wilaya ya Musoma mkoani Mara, Dk. Vincent Anney (Wanne kushoto), akipokea moja ya mabati ya kutengenezea milango na madirisha kutoka kwa Meneja wa Benki ya CRDB tawi la Musoma, Salomon Marwa, kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya Shule ya Msingi Murunyigo. Benki hiyo imetoa mabati, manumba ya vyuma na mifuko 60 ya saruji vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni mbili. **PICHA: MPIGA PICHAWETU**

# Madiwani wataka utekelezaji Sirari kupandishwa hadhi

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MADIWANI na wenyeviti wanaowakilisha maeneo yanayounda mji wa Sirari wameazimia kupaza kilio chao kwa Rais Dk. John Magufuli, wakiomba utekelezaji wa kuupatia hadhi ya mamlaka mji huo.

Septemba 21, 2001 aliyekuwa Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, akiwa ziarani wilayani hapa akihutubia mkutano wa hadhara katika viwanja vya Tarafa alitangaza uamuzi wa serikali kuupandisha hadhi mji huo kuwa mamlaka ya mji.

Miaka 19 imepita agizo hilo halijatekelezwa na madiwani hao wakizungumza katika kikao cha pamoja mwishoni mwa wiki walisema agizo hilo limechelewa kutekelezwa kwa muda mrefu licha ya mji huo kukua kwa haraka na idadi ya watu kuongezeka na upatikanaji wa huduma za jamii.

Diwani wa kata ya Regicheri, John Bosco, alisema badala ya mamlaka zinazohusika kutekeleza agizo hilo halali lililotolewa na aliyekuwa Waziri Mkuu kipindi hicho, pinda hivi sasa kuna zoezi linaendelea la kujumuisha mji huo katika Halmashauri ya mji wa Tarime.

Alisema wananchi katika mji huo na kata za pembezoni zinazotarajiwa kuunda mamlaka hayo wameeleza kutoridhishwa na mchakato wa kugawa mji huo kuelekea Tarime mji.

"Sisi kama wawakilishi wa wananchi tunasikitika kutupiliwa mbali agizo halali la serikali lililotolewa miaka tisa iliyopita na badala yake kuna mchakato unaendelea bila kutuhusisha sisi wawakilishi kumega mji huo na kata za pembezoni kuelekea katika Halmashauri ya Mji wa Tarime," alisema.

Diwani wa Kata ya Sirari, Paul Nyangoko, alisema kutokana na kuimarika huduma za jamii katika mji na idadi ya wakazi wanaozidi 20,000, pia kata tatu jirani za Regicheri, Gwitiryo na Pemba, zikijumuishwa zinatosheleza wananchi wake kufikishiwa huduma ya serikali ya utawala.

"Mji wa Sirari unakua kila kukicha, hivi sasa tuna kituo cha kisasa cha afya, tawi la benki, shule zisizopungua tano za msingi, shule moja ya sekondari na kituo kikuu cha forodha kinachohudumia nchi zote za Afrika Mashariki na makao makuu wilaya ya kipolisi Sirari," alisema Nyangoko.

Mamlaka za Serikali za Mitaa huanzishwa kwa kuzingatia Ibara 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ibara hizi zinaelekeza kuanzishwa kwa vyombo vya serikali za mitaa katika eneo la mikoa, wilaya, mji na kijiji.

Ili kutekeleza matakwa haya, Sheria za Serikali za Mitaa zimeweka masharti, misingi na taratibu za kufuatwa katika kuanzisha mamlaka za serikali za mitaa.

Utaratibu wa kuanzisha mamlaka za serikali za mitaa ni mapendekezo au maombi ya kuanzisha mamlaka hizo kupata ridhaa ya wananchi kupitia vikao vilivyowekwa kisheria katika ngazi za vijiji, kata, halmashauri, wilaya (Kamati ya Ushauri ya Wilaya –DCC na Mkoa (Kamati ya Ushauri ya Mkoa - RCC).



HABARI ARUSHA

# Mashahidi wanane Jamhuri kujenga kesi ya kigogo OBC

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MASHAHIDI wanane upande wa Jamhuri, wataanza kutoa ushahidi wao Aprili 16, mwaka huu katika kesi ya kuajiri raia 10 wa kigeni kinyume cha sheria inayomkabili Mkurugenzi wa Kampuni ya Uwindaji ya Otterlo Business Coparation (OBC), Isaya Mollel, inayomilikiwa na mwanamfalme wa Falme za Kiarabu. Inadaiwa kuwa Mkurugenzi huyo amekiuka sheria ya kuratibu ajira na uhusiano kwa wageni.

Akizungumza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, mbele ya Hakimu Rose Ngoka, Wakili wa serikali, Charles Kagirwa, alidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na atakuwa na mashahidi wanane wa kutoa ushahidi wao.

Wakili Kagirwa alieleza mbali na mashahidi hao pia watatoa vielelezo vya risiti 10 za malipo ya faini za watu 10 walioajiriwa kinyume cha utaratibu. Aliwataja watakaotoa ushahidi huo ni Flaviana Chacha, Bariki John, Koplo Innocent, PC Halima, Natalia Mushi, Joshua Makoo, Mohamed Ahmed na Elisamia Mmari.

Katika kesi hiyo, Mollel ni mshitakiwa wa kwanza kati ya wafanyakazi 10 wa kigeni, waliokuwa wanashitakiwa naye kwa madai ya kuingia nchini bila vibali, ambao walikiri makosa yao Oktoba 3 mwaka jana na kuhukumiwa kulipa Sh.milioni 100 au kwenda jela miezi 12 kisha kurejea katika nchi zao.

Raia hao wa kigeni waliohukumiwa na kulipa fedha hiyo ni Darweshi Jumma, Riaz Aziz Khan, Mohammad Tayyab, Ali Bakhash, Abdulrahman Mohammed, Martin Crasta, Imtiaz Feyaz, Arshad Muhammad, Hamza Sharif na Zulfiqar Ali.

Hakimu Ngoka aliahirisha kesi hiyo hadi Aprili 16, mwaka huu itakapoanza kusikiliza ushahidi upande wa Jamuhuri na mshtakiwa yupo ndani kutokana na kuwa na kesi nyingine ya uhujumu uchumi.

Awali Wakili Mwandamizi wa serikali Mkoa wa Arusha, Abdallah Chavula, akiwa na Wakili Idara ya Kazi Arusha, Emmanuel Mweta , alidai Mollel anashitakiwa kuajiri wafanyakazi kumi kinyume cha sheria ya kazi nchini kati ya Novemba 2018 na Januari mwaka 2019 jana katika OBC iliyopo eneo la Loliondo wilayani Ngorongoro mkoani Arusha.



Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa (kulia), akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkandarasi wa kampuni ya Juin Company Ltd ya jijini Dar es Salaam, Inosent Benard (kushoto), baada ya Waziri huyo kutembelea mradi wa ujenzi wa maji kukagua tenki linalojengwa na mkandarasi huyo katika kijiji cha Umba wilayani Muheza mkoani Tanga, Mradi huo umechelewa kukamilika, hivyo mkandarasi huyo kunusurika kuwekwa mahabusu, na kuagizwa uwe umekamilika kufikia Juni, mwaka huu. Picha. **Na STEVEN WILLIAM**

# NGAUWSA yahamishiwa rasmi AUWSA

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI kupitia Wizara ya Maji imevunja Mamlaka ya Maji ya Mji Mdogo wa Ngaramtoni (NGAUWSA ) na kuhamishia usimamizi wa maji eneo hilo kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWSA).

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, ambayo yalijumuisha mali zote za NGAUWSA pamoja na madeni yaliokuwapo kwa mujibu wa sheria, Katibu Tawala Wilaya ya Arumeru, James Mchembe, aliitaka AUWSA kuhakikisha wananchi wanapata majisafi.

"Septemba mwaka jana serikali ilitangaza rasmi kuivunja NGAUWSA na kuihamishia AUWSA na leo tumekutana hapa kwa ajili ya kushuhudia makabidhiano haya muhimu, AUWSA mhakikishe mnatimiza majukumu yenu kikamilifu ya kuwapatia wananchi huduma ya maji muda wote" alisema.

Aidha aliiagiza kukusanya madeni yote ikiwa ni pamoja na kwenye taasisi zote za serikali na watu binafsi na kuwapa elimu juu ya umuhimu wa uboreshaji miundombinu ya maji ambayo mingi ni chakavu.

Awali Mwenyekiti wa Bodi hiyo, John Sirikwa, alisema mamlaka hiyo ilikuwa inakabiliwa na changamoto ya watu binafsi, kutokusanya ankara za maji kutokana na uelewa mdogo kwa kutojua umuhimu wa kulipa ankara za maji.

"Tumeendesha mamlaka hii kwa shida kwa sababu ilikuwa inakabiliwa na changomoto nyingi ikiwamo gharama kubwa za uendeshaji kuliko makusanyo pamoja na wananchi kutokuwa na elimu ya umuhimu wa kulipa ankara za maji," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa AUWSA, Mhandisi Justine Rujomba, alisema maelekezo yote yaliyotolewa na serikali watatekeleza ya kukarabati miundombinu ya maji maeneo yote, kikubwa wanaomba ushirikiano kutoka kwa viongozi.

"Lakini tutahakikisha wananchi wanapata maji muda wote kwa kuwa sasa Jiji la Arusha upatikanaji wa maji ni asilimia 95 tofauti na awali ambayo ilikuwa asilimia 35," alisema. Akizungumza kwa niaba ya wanachi eneo la Ngaramtoni ambapo zaidi ya kata tano zitanufaika na maji yatakayosimamiwa na AUWSA, Nanginyi Laizer alisema maji yatapatikana kwa uhakika, kutokana na AUWSA kuwa na wataalam wengi na vitendea kazi.

# Madereva bodaboda Namanga lawamani

**Na Zanura Mollel,** NAMANGA

MADEREVA bodaboda mpaka wa Namanga upande wa Tanzania, wanalalamikiwa kusafirisha abiria kutoka Kenya bila kufuata utaratibu wa kupita katika kituo kimoja cha forodha (OSBP) kwa ajili ya ukaguzi wa afya zao.

Akizungumza nwishoni mwa wiki Ofisa Afya Mfawidhi, mpaka wa Namanga Dk.Gabriel Mdachi, alisema kwa sasa wasafiri wamepungua kuingia nchini ambapo wanaoingia ni Watanzania waliokuwa nchini Kenya katika shughuli mbalimbali.

"Hakuna abiria, hii ni kutokana na maeneo mengi ya nchi mbalimbali kufunga mipaka ya wasafiri kuingia isipokua magari ya mizigo," alisema.

Alisema pamoja na kuwapo kwa Watanzania wanaorejea nchini, lakini kumekua na tatizo la wasafiri hao kutopita njia rasmi na badala yake wanatumia bodaboda kuingia nchini kwa kukwepa kukaa karantini siku 14.

Dk. Mdachi alisema kuwa baadhi yao wanaopita mpakani wanakaguliwa na kubainika hawana dalili zozote za COVID 19, lakini wanapoelezwa maelekezo ya serikali yanasema ni lazima kuhifadhiwa karantini kwa siku 14 kwa gharama zao wenyewe, wanakataa na kudai wanarejea nchi waliyotoka.

"Wakisema wanarejea tunakubali warejee, lakini cha kushangaza hawarejei, wanatumia njia ya pikipiki kuwavusha hadi wanapoikuta gari la abiria na kisha kupanda kuendelea na safari," alisema Dk. Mdachi.

Akitolea mfano kuwapo kwa raia wawili wa Burundi na mmoja Mtanzania waliomba kurejea nchi walizotoka, lakini baada ya muda walikamatwa kwenye gari aina ya Noah wakiwa wanaelekea Mjini Arusha . "Wamekamatwa na pasipoti zao tumeomba zizuiwe hivyo tunafanya maandalizi ya kuwahifadhi karantini, maeneo yapo yaliyotengwa na serikali kupitia kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya," alisema Dk.Mdachi.

Dk. Mdachi aliwataka madereva wote wa vyombo mbalimbali vya usafiri kutii sheria za nchi kwa kuzingatia afya za Watanzania,na kuwaomba wananchi wenye nia njema na nchi kushirikiana kutoa taarifa dhidi ya raia wanaoingia nchini bila kukaguliwa afya zao.

Akizungumza Ofisa Mtendaji wa Mji wa Namanga, Nevely Mungaya, alisema alithibitisha kuwapo tabia ya madereva bodaboda kusafirisha watu bila kufuata utaratibu, lakini wameshatoa elimu na kuwataka kuacha tabia hiyo, kwani atakapo bainika yeyote atachukuliwa hatua kali za kisheria .

"Bodaboda hizo zinatumika kwa biashara nyingi haramu ikiwamo kusafirisha wahamiaji haramu mfano Wasomali, dawa za kulevya, lakini sasa wameanza kuvusha wasafiri ambao hawataki kupita kwenye kitengo cha afya OSBP kukaguliwa afya zao...hawa wanataka kutusababishia maambukizi kuenea nchini, tutawashughulikia," alisema Mungaya.

Katibu wa madereva wa Hiace, Samuel Chala, alisema wameshatoa elimu kwa madereva wa magari kutopakia abiria njiani wanaopelekwa na bodaboda na atakayekiuka agizo hilo atachukuliwa hatua za kisheria .

"Dereva akikamatwa,gari linarejeshwa hadi mpakani na abiria wanashusha kuingizwa kwenye ukaguzi kisha dereva atawekwa chini ya ulinzi wa polisi na gari itafungiwa kufanya kazi," alidai Chala.

Akijibu tuhuma za magari aina ya Hiace kuonekana kushirikina na madereva bodaboda kuvusha magendo na watu wanaokwepa kuwekwa karantini, alisema hali hiyo imepungua kutokana na wao kushirikiana na viongozi wa serikali kutoa elimu na kuziba mianya yote ya magendo.

# Kituo cha afya chakabiliwa uhaba vitendea kazi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

KITUO cha Afya Kisiwani kilichopo Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, ambacho kilijengwa kwa fedha za umma zaidi ya Sh. milioni 400 na kukamilika, hakina uwezo wa kutoa huduma za afya kwa kiwango kinachotakiwa kutokana na kukabiliwa na uhaba wa vifaa tiba na vitendanishi.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alikiri kituo hicho kuhitaji msaada wa hali na mali wa vifaa mbalimbali ili kiweze kutoa huduma stahiki kwa wananchi wa ukanda wa milimani.

Alikuwa akizungumza na Nipashe jana, baada ya kupokea msaada wa vifaa yakiwamo magodoro ambayo yametolewa na mmoja wa wazawa wa Kata ya Mwembembaga, wilayani humo, Seif Seif.

"Ni kweli majengo ya kisasa yapo pamoja na miundombinu bora ya kwaajili ya kutoa huduma ipo, lakini kituo hiki cha afya kisiwani kina tatizo la uhaba wa vifaa. Tunamshukuru hata mfadhili aliyejitokeza na kuleta zaidi ya magodoro 30," alisema Senyamule.

"Magodoro haya yamekuja wakati sahihi, kwa sababu ni wakati ambao tunahitaji wadau wengi kuchangia huduma za afya hasa wakati huu wa mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona."

Kata hiyo ilipokea magodoro hayo kutoka kwa mdau huyo wa afya, kupitia kampeni maalumu ya kijiji Change, furaha yangu.

Kituo hicho kilijengwa na serikali ili kusogeza huduma za afya kwa jamii hiyo ya ukanda wa milimani kwa ajili ya kupunguza vifo vya mama na mtoto.

"Nawakaribisha wadau wengine kuchangia upatikanaji wa vifaa mbalimbali vya kituo hiki, kwa kuwa bado tunahitaji vifaa ili huduma ziende vizuri zaidi. Pia nawakumbusha kuendelea kujikinga na corona kwa kuzingatia maelekezo ya serikali pamoja na kumuomba Mungu," alisisitiza Senyamule.

# KKKT yajipanga likizo kwa watumishi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TISHIO la virusi vya corona kusambaa kwa kasi zaidi katika nchi za Afrika ya Mashariki, limeisababisha Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), kuchukua hatua zaidi za kujikinga, baada ya kuagiza kila mkuu wa kituo kinachomilikiwa na kanisa hilo kupanga haraka likizo za watumishi.

Pia, Dayosisi hiyo imeelekeza wakristo watakaoshindwa kuhudhuria ibadani kwa sababu ya ugonjwa, wanaweza kutoa sadaka zao kwa wazee wa usharika, wateteri au kwa njia ya mtandao wa simu zilizosajiliwa kwa jina la usharika. Jana, Katibu Mkuu wa Dayosisi hiyo, Arthur Shoo, alithibitisha kuwa wameongeza umakini zaidi katika suala hilo kwa kuongeza kipengele hicho.

"Tumeelekeza tena kwamba, hivi sasa kila mkuu wa kituo atathmini idadi ya watumishi wake ili aweze kuona jinsi ya kuwapangia likizo na watu washauriwe kula vizuri vyakula vyenye kujenga na kulinda mwili," alisema.

Pia, katika waraka ulioandikwa Aprili 3, mwaka huu na kusainiwa na Askofu wa Dayosisi hiyo ambaye pia ni Mkuu wa KKKT nchini, Dk. Frederick Shoo, unaelekeza sharika na vituo vya dayosisi hiyo vibane matumizi yasiyo ya lazima, angalizo liwekwe kwenye ibada ya Pasaka ziwe fupi na zenye watu wachache.

Pamoja na mambo mengine, waraka huo umeelekeza pia kila Usharika ujitahidi kuwa na vipima joto (themoscan) vinavyoweza kupima joto mbali.

Vile vile, waraka huo uliosomwa jana katika makanisa yote ya Dayosisi ya Kaskazini umeelekeza wazee wa kanisa wanapohesabu sadaka wavae barakoa pamoja na gloves, ibada za watoto na mafundisho ya kipaimara ziahirishwe kwa sasa.

Wiki iliyopita, Askofu Dk. Shoo alisema wakati wowote, kanisa hilo litachukua hatua za ziada katika kukabiliana na kasi ya maambukizi ya corona. Alisema katika kukabiliana na janga hilo, watachukua hatua za ziada katika taratibu za ibada, ingawa hawataacha kumuabudu Mungu.



Watendaji wa vituo vya forodha vya Holili na Tarakea pamoja na baadhi ya wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wakitembelea baadhi ya maeneo likiwamo la kuwahifadhi watu watakaopatikana na dalili za Corona. Aliyevaa Koti Jekundu ni Mwakilishi wa wabunge wa Bunge la EAC, Pamela Maasai , anayemfuata kushoto ni Mkuu wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi na wengine ni maofisa wa ngazi mbalimbali za Forodha wa vituo hivyo. **PICHA ZOTE NA ASRAJI MVUNGI**

# Wanaoingia mipakani njia za panya wawekwa kuzuizini

**Na Asraji Mvungi,** ROMBO

KUFUATIA maeneo yanayopakana na nchi jirani mkoani Kilimanjaro kuendelea kutumika kupitisha wageni kwa njia za panya, watendaji wa vituo vya forodha vya Holili na Tarakea vilivyopo wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro wamelazimika kuanza kuwaweka kizuizini watu waliobainika kuingia nchini kwa utaratibu huo ikiwa ni hatua ya kuepusha kuenea kwa virusi vya corona.

Wakizungumza na ujumbe wa wabunge wa bunge la EAC waliotembelea vituo hivyo kujionea changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa hatua za tahadhari za kujikinga na corona watendaji hao wamesema tayari watuhumiwa 20 wameshakamatwa na wako katika vituo vilivyotengwa kwaajili ya kuweka watu wanaoingia nchini kwa siku 14 kwa gharama zao. Mmoja wa watendaji hao akiwemo, Eliachi Marandu wa kituo cha Tarakea alisema, wamelazimika kufikia hatua hiyo kutokana na wananchi wengi kuendelea kukaidi agizo la kuingia nchini kwa kupitia njia za panya na kwa sasa wanashirikiana na wenyeji wanaosaidia kuwapitisha badala ya kutoa taarifa.

"Kutokana na ukubwa wa mipenyo vya mpaka huu, jitihada zetu za kudhibiti tatizo hili kwa njia za kawaida zinakwama, na mbaya zaidi wamekuwa wakiwatumia watu wa bodoboda, yaani inakuwa ngumu sana kuwadhibiti," alisema Marandu.

Ofisa mfawidhi wa afya wa kituo cha Tarakea, Rashidi Mkanjika, alisema pamoja na changamoto hizo wanaendelea kufuatilia mwenendo wa afya za watu hao ambao kati yao yupo raia mmoja wa Kenya na wengine ni Watanzania waliokuwa wanaishi ama kuendesha shughuli zao nchini humo.

Pia Mkanjika alisema wanaendelea kuwapima wanaoendelea kufuata sheria za kupitia katika maeneo halali wakiwamo madereva wa malori wanaosafirisha bidhaa mbalimbali vikiwamo vyakula ambao wamewekewa utaratibu maalumu wa kuchekiwa afya zao katika maeneo yote wanayopita na utaratibu huo unakwenda vizuri.

Mkuu wa Mamlaka ya Mapato mkoani Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, alisema wanaendelea kushirikiana na watendaji wa taasisi zingine kuhakikisha kuwa majukumu ya msingi yanaendelea, tahadhari zinachukuliwa na sheria pia zinafuatwa.

Naye Meneja Msaidizi wa Forodha wa Mkoa wa Kilimanjaro, Edwin Iwato, alisema pamoja na changamoto hizo wameendelea pia kutoa elimu kwa wananchi wa mpakani ya kuwawezesha kuendelea kufanya majukumu yao katika mazingira ya tahadhari japo wengi wao wanakuwa wagumu kutekeleza.

"Maeneo haya kuna wafanyabiashara wadogo wengi ambao wanatoka eneo moja kwenda lingine, tumekuwa pia tukiwashauri njia salama za kuendelea na majumu yao kwa kufuata sheria, lakini wengi wanakuwa wagumu kwa kuwa walishazoea na tunaendelea kuwaomba viongozi wa kijamii kusaidia kuwaelimisha kimsingi sisi tutaendelea kusimamia sheria," alisema.


Pia alisisitiza umuhimu wa nguvu kubwa zaidi kukabiliana na janga hilo kuelekezwa kwenye vituo vya forodha hasa kuongeza vitendea kazi.

Akizungumza na watendaji hao baada ya kutembelea kujionea hali halisi na pia kusikiliza changamoto zao mwakilishi wa wabunge hao wa Bunge la EAC kutoka Tanzania, Pamela Maasai, amepongeza hatua zinazoendelea kuchukuliwa kukabiliana na janga la corona.

Alisema licha ya athari zitakazotokana na hatua zinazochukuliwa itabidi ziendelee kuchukuliwa kwa kuwa utaratibu huo ukiachwa kuendelea utaleta maafa makubwa badaye ambayo udhibiti wake utakuwa mgumu.

NIPASHE JUMATATU APRILI 6, 2020

Nipashe Spotika



## KWA NINI CEBALLOS ABAKISHWE ARSENAL?

UK. 20




### ISIKUPITE

WAKATI Jumatatu iliyopita Sergio Ramos akisherehekea kutimiza miaka 34, ameendelea kushikilia rekodi ya mchezaji anayeongoza kwa kuonyeshwa kadi nyekundu nyingi (20) kwenye LaLiga. Kwa ujumla Mhispania huyo ametolewa nje ya uwanja mara 26 kwenye mashindano yote. Pia akitolewa nje mara nne kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, hivyo kufikia rekodi katika michuano hiyo.

# USAJILI WA MAANA 6 EPL

Kiungo wa Liverpool, James Milner akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Napoli, Kalidou Koulibaly kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa msimu huu. Koulibaly anatajwa kuwa mmoja wa mabeki wanaoweza kutatua tatizo la safu ya ulinzi ya Manchester City. **HABARI UK. 16-17**

SOKA

# 11-BORA YA LIGI KUU UFARANSA



Mbappe

**PARIS, Ufaransa**

MARA zote Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, inatajwa kama ya mbio za farasi mmoja. Na hata kama PSG wako mbali dhidi ya timu nyingine kileleni mwa msimamo. Hata hivyo kuna mengi ya kuzungumza msimu huu ambayo yamekuwa yakuvutia.

Hivyo, hebu tuanze na wachezaji bora. Nyota Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 17 wa klabu ya Rennais amekuwa na mwaka mzuri, huku Lyon wakionekana kumpata Alexandre Lacazette ajae kwa Moussa Dembele ambaye ana mabao 16 msimu huu.

Makala hii inakuchambulia kikosi bora cha wachezaji 11 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa hadi sasa kwa msimu huu, hawa hapa...

**Kipa: Predrag Rajkovic (Reims)**

Stade Reims imekuwa na safu imara zaidi ya ulinzi msimu huu, ikiwa imeruhusu mabao 21 tu kwenye ligi ambayo ni idadi ndogo zaidi kwenye Ligue 1, na nyuma ya mafanikio hayo yupo Predrag Rajkovic. Kipa huyu wa kimataifa wa Serbia amekuwa na kiwango cha kuvutia kwa kuokoa hatari langoni mwake, pia akiwa hajaruhusu bao kwenye mechi 12. Akiwa na wastani wa 2.6 kwa mchezo kuokoa hatari langoni mwake.

**Beki wa Kulia: Fabien Centonze (Metz)**

Metz wamekuwa na msimu wa moto, lakini Fabien Centonze amekuwa na kiwango cha kuvutia. Akiwa amesajiliwa kipindi cha majira ya joto kutoka timu ya Ligue 2, Lens, uwezo wake wa ukabaji umekuwa wa kuvutia mno. Amekuwa akizuia kila nafasi ya washambuliaji kufunga mabao, huku pia akitoa pasi za mwisho za kutosha. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa nguzo imara zaidi kwa safu ya ulinzi ya Metz.

**Beki wa Kushoto: Hassane Kamara (Reims)**

Orodha hii ingeonekana kutawaliwa na wachezaji wa PSG, lakini ukuta imara wa Reims unaifanya kutoa nyota mwingine. Hassane Kamara ni mmoja wa wachezaji wanaoufanya ukuta huo kuwa imara zaidi.

Aina ya uchezaji wake imekuwa ni ya kuvutia, kwani amekuwa akicheza kwa kupanda na kushuka huku akisaidia mashambulizi kwenye safu yake ya ushambuliaji.

**Beki wa Kati: Marquinhos (PSG)**

Raia huyu wa Brazil amechukua majukumu mapya ya kucheza safu ya beki wa kati. Amekuwa akiokoa hatari nyingi za kuelekea langoni mwake. Pia amekuwa mzuri zaidi wa kugawa mipira na anaonekana kuvaa viatu vya Thiago Silva kwa siku za usoni.

Alikuwa nguzo muhimu wakati wa ushindi dhidi ya Real Madrid na Borussia Dortmund kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Beki wa Kati: Yunis Abdelhamid (Reims)**

Stade Reims imekuwa na safu ngumu na imara ya ulinzi msimu huu na mmoja wa wachezaji anayeiimarisha ni Yunis Abdelhamid. Amekuwa kiongozi wa mfano akiongoza kuokoa hatari langoni mwake. Raia huyu wa Morocco amekuwa na mchango mkubwa zaidi kwa kikosi chake hicho msimu huu.

**Kiungo wa Kulia: Angel Di Maria (PSG)**

Kile ambacho Kevin de Bruyne amekuwa akikifanya kule Manchester City, ndicho ambacho Angel Di Maria amekuwa akikifanya pale PSG. Yeye ni 'ofisa' wa ubunifu kwenye kikosi chake, amekuwa msaada mkubwa wa nguvu ya ushambuliaji ya PSG.

Pasi zake za mwisho 14 zimekuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye ligi na yeye ndiye mchezaji mwenye pasi nyingi zaidi katika kikosi hicho.

**Kiungo wa Kati: Idrissa Gueye (PSG)**

Idrissa Gueye amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia akiwa amesimama pale kwenye dimba la kati. Mchezaji huyu wa zamani wa Everton amekuwa na pasi zenye uhakika mara zote. Gueye amekuwa ndiye kama muhimili wa kuanzisha mashambulizi ya PSG.

**Kiungo wa Kushoto: Dmitri Payet (Marseille)**

Mchezaji huyu wa zamani wa West Ham United ameendelea kuonyesha umwamba wake kwa kiwango cha kuvutia. Amekuwa nguzo muhimu kwa kikosi cha Marseille. Amefunga mabao tisa kwenye kikosi chake msimu huu na pia kuwa mgawaji mzuri wa pasi za uhakika kwenye Ligue 1.

**Winga wa Kushoto: Neymar (PSG)**

Nyota huyu wa zamani wa Barcelona amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara msimu huu, lakini hilo halijamzuia kuonyesha kiwango chake. Akiwa na mabao 13, anaburuzwa na wachezaji watatu tu kwenye ligi hiyo ambao wanaongoza kwa kucheka na nyavu.

**Winga wa Kulia: Kylian Mbappe (PSG)**

Inaonekana kama Kylian Mbappe amefanya ya kutosha kuthibitisha kuwa mchezaji bora. Kutokana na kiwango chake bora cha kufunga mabao kumemfanya kuwa mchezaji wa aina yake na kuwa kwenye orodha ya wachezaji wenye thamani kubwa duniani. Mbappe kwa mara nyingine tena anaongoa mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu akiwa na mabao 18, huku akiwa na 'asists' pasi za mwisho saba.

**Mshambuliaji: Wissam Ben Yedder (AS Monaco)**

Wissam Ben Yedder amekuwa nyota muhimu kwa Monaco inayofufuka. Uwezo wake wa kufunga mabao na kusaidi mengine umeisaidia zaidi Monaco, amekuwa na mchango wa asilimia 41 kwenye kikosi chake. Mshambuliaji huyo wa zamani wa Sevilla pia anawania Kiatu cha Dhahabu na Mbappe.

**JE, WAJUA?**



BEKI wa Liverpool, Virgil van Dijk, amemtaja nyota wa Barcelona, Lionel Messi, kama mpinzani hatari zaidi aliyewahi kukutana naye katika wasifu wake kisoka. Wawili hao walikutana katika mechi mbili za nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita. Lakini pia Van Dijk amemsifu Sergio Aguero, kama miongoni mwao wakati akikutana na Manchester City.

## MICHEZO

# USAJILI 11 BORA LIGI KUU MSIMU HUU

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kwamba Ligi Kuu imesimama kwa muda kwa ajili ya ugonjwa wa COVID-19 unaotokana na virusi vya corona, bado mashabiki wa soka nchini wanakumbuka ushindani mkubwa uliokuwapo kwenye ligi msimu huu, tofauti na misimu kadhaa iliyopita.

Pia wanakumbuka ubora wa baadhi ya wachezaji waliokuwa wakitoa burudani uwanjani, wengine wakiwa kwenye viwango vya juu msimu huu.

Baadhi ya wachezaji hao ni wa msimu uliopita, lakini wengine walisajiliwa mwanzoni msimu huu wa 2019/20, huku wengine wakisajiliwa kipindi cha dirisha dogo.

Mara nyingi klabu nchini zimekuwa zikiingia mkenge kwa kusajili baadhi ya wachezaji wenye viwango duni, wengine vikiwa vya kawaida tu, lakini msimu huu kuna baadhi ya wachezaji wameufanya kuwa usajili bora.

Hawa ni baadhi ya wachezaji ambao wamefanya klabu, viongozi wao, wanachama na mashabiki kujisifu kutokana na usajili wao kulipa, wafahamu...

**1. Metacha Mnata- Yanga**

Ni kipa namba moja kwa sasa wa Yanga. Alisajiliwa msimu huu akitokea Mbao FC. Kwa sasa amekuwa ni mmoja wa wachezaji mhimili kwenye kikosi cha Yanga.

Amekuwa akiokoa hatari nyingi langoni ambazo zilionekana kuwa zingekuwa mabao, lakini pia ni jasiri awapo kwenye milingoti mitatu. Kwa sasa wanachama na mashabiki wa Yanga huwaambii chochote kwa kipa huyu ambaye usajili wake umekuwa na tija kwa klabu yao.

**2. Lamine Moro- Yanga**

Kama utakumbuka aliwahi kuja nchini kufanya majaribio na Simba katikati ya msimu uliopita, wakamtema. Mghana huyo alisajiliwa na Yanga msimu huu. Hata wenyewe walikuwa hawana uhakika naye kutokana na kudhihakiwa na watani zao kuwa wamesajili garasa. Kinyume chake kwa sasa ndiye beki tegemeo na mwenye uwezo mkubwa wa kuzuia na kupambana na mastraika hatari.

**3. Niver Tegere- Azam**

Ni raia wa Zimbabwe ambaye alisajiliwa na Azam FC kipindi cha dirisha dogo msimu huu. Awali alikuwa kama haelewiki hivi. Lakini baada ya kuizoea ligi ya Tanzania, amekuwa mchezaji wa kutegemewa kwenye nafasi ya kiungo mshambuliaji, akiwa tayari ameshapachika mabao mawili mpaka sasa.

**4. Yusuph Mhilu- Kagera Sugar**

Kagera Sugar ilimsajili kutoka Ndanda FC. Na hii ni baada ya kumaliza mkataba wake kutoka Yanga. Ndanda alikuwa akicheza kwa mkopo baada ya Yanga kumuona hafai. Kwa sasa anauwasha moto akiwa Kagera Sugar kwenye kiwango cha juu, kiasi cha kumezewa mate tena na Yanga wenyewe, Simba na hata Azam FC. Ameshapachika mabao 11 mpaka sasa.

**5. Deo Kanda- Simba**

Maneno yalikuwa mengi kwenye usajili wake wa mkopo kutoka TP Mazembe. Wengi hawakuamini kuwa TP Mazembe wanaweza kumtoa kwa mkopo mchezaji mzuri, badala yake wakadhani kuwa kiwango cha Mkongomani huyo kimeshashuka. Mwanzoni ni kweli alionekana hivyo. Lakini baadaye aligeuka na kuwa lulu kwa kikosi cha Simba, kiasi cha takwimu kuonyesha kuwa mechi yoyote ambayo Deo Kanda alianza, timu hiyo haijawahi kupoteza.

Uwezo wake umesababisha hadi TP Mazembe wenyewe kutaka kumrudisha, ingawa mwenyewe anasema anaipa kipaumbele Simba kwanza.

**6. Balama Mapinduzi- Yanga**

Alionekana ni mchezaji wa kujaza idadi ya wachezaji 30 tu aliposajiliwa mwanzoni mwa msimu akitokea Alliance FC. Lakini tangu mechi za mwanzo tu alionekana ana kitu. Mechi iliyomuibua zaidi na kumfanya ajulikane na yeye mwenyewe ajiamini zaidi ni ile ya Januari 4, mwaka huu alipofunga bao kwenye mechi ya watani, Simba na Yanga, zikitoka sare ya mabao 2-2.



Miquissone

**7. Luis Miquissone- Simba**

Ni mchezaji ambaye kila shabiki wa soka alitegemea kuwa kama akiwa kwenye kiwango chake kile kile walichokiona kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika akiichezea UD Songo dhidi ya Simba, basi atatisha.

Simba ilimsajili raia huyu wa Msumbiji kipindi cha dirisha dogo na ilionekana kama bado hajazoea mazingira. Alipokaa sawa ndiyo shughuli ikaanza. Amekuwa ndiye kipenzi cha wanachama na mashabiki wa Simba kutokana na uwezo wake mkubwa wa mbio, changa za maudhi, mashuti makali na uwezo wa kutengemeza nafasi na kufunga.

**8. Marcel Kaheza- Polisi Tanzania**

Baada ya kumaliza mkataba wake na Simba akitokea Kenya alikokuwa akicheza kwa mkopo, alijiunga na Polisi Tanzania msimu huu. Ni moja kati ya usajili bora si kwa Polisi Tanzania tu, bali kwa Ligi Kuu nzima msimu huu. Ameshapachika mabao sita mpaka sasa kwenye ligi.

**9. Blaise Bigirimana- Namungo**

Nadhani kama Namungo FC ingefahamu, isingempa mkataba wa mwaka mmoja. Mrundi Bigirimana Blaise amekuwa na kiwango kizuri msimu huu, akisajiliwa kutoka Alliance FC, ambapo kabla aliichezea pia Stand United. Ameshapachika mabao tisa mpaka sasa na tayari anayemelewa na klabu kubwa, hasa Yanga.

**10. Benard Morrison- Yanga**


Usajili wake haukuwa na mbwembwe sana kama ilivyo kawaida ya klabu kubwa. Lakini ametokea kuwa mchezaji tegemeo na kipenzi cha wanachama na mashabiki wa Yanga. Mghana huyu alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili na kuifanya Yanga iliyokuwa kama imedorora hivi, kuchangamka na mashabiki wao kuwa na la kuongea mitaani, kutokana na staili yake ya uchezaji wa mbwembwe na madoido.

**11. Francis Kahata- Simba**

Kuna baadhi hata Wanasimba wenyewe walisema kuwa klabu yao iliingia mkenge kumsajili Francis Kahata kutoka Gor Mahia ya Kenya. Kwa sababu kwenye mechi za mwanzo wa msimu huu hakuwa kwenye kiwango kizuri. Ujio wa Kocha Mpya Mbelgiji Sven Vandenbroeck ambaye alionekana kumuamini zaidi, kumemfanya mchezaji huyo kuonyesha kipaji na uwezo wake na kuwafanya mashabiki wa Simba kupagawa. Kahata ni mmoja wa wachezaji vipenzi kwa mashabiki wa Simba kwa sasa.

### NJE YA UWANJA

MANCHESTER City inatabiriwa kumaliza msimu wa Ligi Kuu England ikiwa nafasi ya pili na pointi 80, huku Liverpool ikipewa nafasi ya kuhitimisha na alama 101, hivyo kufanya tofauti ya pointi kuwa 21 ambayo itakuwa tofauti kubwa zaidi kuwahi kutokea katika ligi hiyo. Man City inashikilia rekodi ya kumaliza msimu kwa tofauti kubwa ya alama 19 hadi sasa, ikifanya hivyo dhidi ya Manchester United iliyomaliza ya pili msimu wa 2017-18.





WERNER

# USAJILI MMOJA WA MAANA KWA TIMU SITA BORA EPL

**LONDON, England**

HUKU michuano ya soka duniani ikiwa imesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, kitu kimoja kinaweza kuwa hewani katika dirisha la usajili linalokuja.

Chukulia kwamba msimu wa 2019-20 hautaendelea hadi katikati ya majira ya joto, hakuna mtu mwenye uhakika nini kitatokea kwenye dirisha la usajili - kama mambo yatakwenda hivyo.

Na kama ikiwa hivyo, litakuwa dirisha la usajili litakalokaa kwenye kumbukumbu - hasa katika tamaduni ya klabu sita za juu za Ligi Kuu ya England, ambapo tatu kati yake zinaonekana kukosa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wakati hilo likiwa akilini, namna gani vikosi vitaangalia jinsi ya kujiimarisha? Hapa tunaangalia usajili mmoja kwa kila klabu ambao utaleta maana kwa klabu sita za juu.

**#1 Liverpool - Timo Werner**

Liverpool walikuwa wanaondoka na taji la Ligi Kuu ya England kabla kusimamishwa ,na vijana hao wa kocha, Jurgen Klopp walikuwa wanajiamini kwamba watashinda taji lao la kwanza la ligi tangu msimu wa 1989-90. Hivyo, chukulia msimu wa 2019-20 unafikia mwisho na 'Wekundu' hao wanatwaa taji, watahitaji kweli kuimarisha kikosi chao kipindi cha majira ya joto? Kiukweli, si muhimu.

Tayari wana wachezaji bora duniani katika kila nafasi - Alisson Becker, Virgil van Dijk, Trent Alexander-Arnold, Mohamed Salah na wengineo - na ingawa safu yao ya kiungo haionekani kuwa bora kwenye magazeti, uwapo wa wachezaji kama Jordan Henderson na Georginio Wijnaldum utafiti kwenye mfumo wa Klopp.

Hiyo maana yake ni kwamba, kama Klopp anataka kuingia sokoni pengine itakuwa ni kwa ajili ya kutafuta wasaidizi wa nyota wake wa sasa. Usajili wa Januari wa Takumi Minamino unafiti vizuri, hivyo mashabiki wa Wekundu hao wanaweza kusahau kuhusu wachezaji kama Kylian Mbappe na Philippe Coutinho kutua pale Anfield.

Kwa wachezaji waliopo, nyota wa RB Leipzig, Timo Werner anaweza kufiti. Liverpool wana safu bora zaidi ya ushambuliaji inayowajumuisha Salah, Roberto Firmino na Sadio Mane, lakini msaidizi wao pekee kwa sasa ni Divock Origi.

Werner kwa upande mwingine, baada ya kufunga mabao 27 katika mechi 36 msimu huu - si tu atakuwa msaidizi wa washambuliaji wa Wekundu hao kwa sasa, lakini pia atatoa changamoto ya namba kwenye kikosi cha kwanza. Na kwa kuwa fungu lake la kuondoka ni pauni milioni 50 - ni aina ya mchezaji anayefaa kusajiliwa Liverpool kwa sasa.

**#2 Manchester City - Kalidou Koulibaly**

Manchester City ya Pep Guardiola kikosi chake hakina udhaifu mwingi, baada ya kutumia fedha nyingi katika vipindi vya usajili vilivyopita. Kwa uhakika, kiungo David Silva anapanga kuondoka pale Etihad kipindi cha majira ya joto, lakini klabu tayari ina mtu ambaye anaweza kuziba pengo lake ambaye ni kijana Phil Foden. Hata hivyo, bado kuna tundu kwenye nafasi ya beki wa kati.

Hilo lisingekuwa tatizo msimu mmoja uliopita, lakini kuondoka kwa Vincent Kompany na kukabiliwa kwa majeruhi kwa Aymeric Laporte kumemuacha Guardiola akiwa na wachezaji wenye viwango vya kupanda na kushuka, John Stones na Nicolas Otamendi, pamoja na kiungo, Fernandinho.

Msimu wa 2018-19, ulishuhudia City wakipoteza mechi nne tu na wakiruhusu nyavu zao kutikiswa mara 23; lakini kwa msimu wa sasa tayari wameshapoteza mechi saba na wameruhusu mabao 31, huku zikiwa zimebaki mechi 10 ligi kumalizika. Hivyo kama Guardiola anataka kikosi chake kirudi kwenye kasi yake, analazimika kuimarisha safu ya ulinzi kipindi cha majira ya joto.

Hivyo usajili wa beki wa kimataifa wa Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 28, anayecheza pale Napoli ni muhimu. Beki huyo wa kati alikuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Manchester United msimu uliopita, lakini ilishindikana, na akaamua kubakia pale kwenye dimba la San Paolo, ambako alikabiliwa na majeraha na kujikuta akicheza mechi 15 za ligi msimu huu.

Licha ya hilo bado ni mtu muhimu kwa kikosi hicho kuliko wote wawili Stones na Otamendi.

**#3 Tottenham Hotspur - Max Aarons**

Tottenham Hotspur imekuwa kwenye wakati mgumu zaidi kati ya klabu sita za juu msimu huu. Kuanza vibaya kwa msimu huu kumewaacha kwenye wakati mgumu wa kupambana kutafuta nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, huku pia Mauricio Pochettino akipoteza kibarua chake, lakini huku Mourinho akiwa amefanya angalau vizuri kidogo, kikosi hicho bado hakijawa kwenye wakati mzuri.

Miamba hao wa Jiji la London walimuuza Kieran Trippier kwenda Atletico Madrid kipindi cha majira ya joto na hawajapata mbadala wake.

Badala yake Spurs imeamua kumtumia Serge Aurier kama ndiye beki wa kulia chaguo la kwanza na amekuwa akifanya makosa mengi ya wazi.

Kutokana na hali ya kifedha, ni wazi kwamba Spurs hawako kwenye nafasi ya kusajili beki wa kulia wa daraja la juu. Lakini wanachaguo moja la Max Aarons wa Norwich City. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, anaonekana anaweza kushuka daraja na kikosi hicho na hivyo Spurs wana nafasi ya kutumia mwanya huo kumsajili kwa bei rahisi.

**#4 Chelsea - Dean Henderson**

Msimu wa kwanza wa Chelsea chini ya kocha mpya, Frank Lampard umekwenda vizuri, ingawa si kwa kiwango bora zaidi. Kwa sasa 'Blues' hao wanashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu na wakiwa na nafasi nzuri ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao wa 2020-21, na Lampard anatumia wachezaji ambao ni zao la akademi yao kama Tammy Abraham na Mason Mount na Reece James pamoja na Billy Gilmour.

Hata hivyo, mchezaji mmoja ambaye amekuwa kwenye presha kubwa msimu huu ni golikipa, Kepa Arrizabalaga. Raia huyu wa Hispania- ambaye alisajiliwa kutoka Athletic Bilbao kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kwa makipa ya pauni milioni 71.6 kipindi cha majira ya joto ya mwaka 2018 - alikuwa na mwanzo mzuri, kabla ya kiwango chake kushuka.

Na sasa Chelsea wanaonekana kutafuta mbadala wa Kepa, huku uvumi ukimhusisha kipa wa Burnley, Nick Pope.

Hata hivyo, pengine usajili mzuri zaidi unaweza kuwa wa Dean Henderson. Kipa huyu wa timu ya Taifa ya England chini ya umri wa miaka 21, amekuwa akicheza kwa mkopo pale Sheffield United akitokea Manchester United na amekuwa na kiwango bora kabisa.

Kwa hali jinsi ilivyo, alikuwa anatarajiwa kurudi kwa klabu yake ambao ni 'wazazi' wake, lakini tayari Man United wana kipa namba moja wao, David De Gea ambaye ana mkataba wa muda mrefu na wa gharama kubwa na hilo litamfanya kutokuwa na nafasi pale. Hivyo, Chelsea wanatakiwa kutumia nafasi hivyo kumsajili kipa huyo.

**#5 Manchester United - Jack Grealish**

Ole Gunnar Solskjaer amekuwa akipata shutuma kadhaa tangu alivyothibitishwa kuwa kocha mkuu wa Manchester United, lakini kwa wakati wake raia huyo wa Norway amefanya kazi nzuri. Wachezaji walionekana kutokuwa wa muhimu kama Ashley Young, Romelu Lukaku, Chris Smalling na Matteo Darmian wote wameondolewa na ukafanyika usajili wa Harry Maguire, Aaron Wan-Bissaka na Bruno Fernandes - ambao bila shaka yoyote wameimarisha kikosi cha kwanza cha 'Mashetani Wekundu' hao.

United safu yao ya ulinzi inaonekana kuwa imara, huku safu ya ushambuliaji ikionekana kuwa hatari chini ya Anthony Martial, Marcus Rashford, Daniel James na Mason Greenwood na kiungo chao kina Fernandes - ambaye naye anafanya vizuri.

Hivyo, usajili wa nyota wa Aston Villa, Jack Grealish utakuwa na maana kubwa kwenye kikosi hicho. Grealish atakuwa msaada mkubwa zaidi kwa Man United katika kuiunganisha cha safu ya ushambuliaji.

**#6 Arsenal - Lewis Dunk**

Arsenal bila shaka inaimarika chini ya kocha mpya, Mikel Arteta tangu alipotua hapo Desemba mwaka jana. Chini ya kocha huyo raia wa Hispania, 'Washikabunduki' hao wamekuwa wanavutia kuwaangalia dimbani, hasa vijana wao kama Bukayo Saka, Eddie Nketiah na Dani Ceballos.

Hata hivyo, safu yao ya ulinzi bado inapwaya, na bila shaka yoyote beki wa Brighton, Lewis Dunk mwenye umri wa miaka 28, anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwako.

## Nukuu

"Niwe muwazi kwamba nataka kurudi Barca, sasa ninajiona binafsi nikiwa kocha, nadhani ninaweza kuchangia kitu kwa wachezaji. Ningependa kufanya kazi pamoja na watu ambao ninaimani nao, ambao kuna uaminifu, na ni watu gani halali, tunazungumza kuhusu Carles Puyol, ambaye alikuwa nahodha wa Barca, na Jordi Cruyff, biashara nzuri na uzoefu mkubwa katika ukatibu wa ufundi," **Xavi Hernandez ambaye kwa sasa anainoa Al Sadd ya Qatar.**



"Najisikia vizuri sana, natakiwa kufanyiwa vipimo tena kwa siku kadhaa, lakini kwa sasa najisikia vizuri zaidi ikilinganishwa na wiki mbili au tatu zilizopita. Nahisi vizuri mara 10 zaidi kwa sasa. Kwa upande wangu, sasa ni suala tu la kurudi dimbani haraka kuanza mazoezi kwa kucheza mechi kwa ajili ya timu yangu," **Marcus Rashford.**



"Wote tunajua namna gani hali ilivyo ngumu, leo hii wote tunapambana kama timu. Tuwe imara kwenye mapambano haya. Kama tunaweza kumsaidia mtu, tufanye hivyo. Hali hii inamuathiri kila mmoja wetu, hivyo tunawaomba kufuata maelekezo na kusikiliza nani anajua zaidi. Tuwe makini na tuamue kupambana kwa pamoja," **mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski baada ya yeye na mkewe kuchangia euro milioni moja sawa na Sh. bilioni 2.4 za Tanzania katika mapambano dhidi ya virusi vya corona (COVID-19).**



# ATHARI 6 LIGI KUU BARA KAMA IKIFUTWA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ugonjwa wa, virusi vya corona COVID-19 ukiitesa dunia, bado mashabiki wa soka wamekuwa na mijadala mbalimbali juu ya mustakabali wa ligi duniani.

Tayari nchini Ubelgiji ligi ya nchini humo imefutwa na klabu iliyokuwa inaongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo, Club Brugge ikitawazwa kuwa mabingwa, huku klabu ya zamani ya Mtanzania Mbwana Samatta, KRC Genk ikifuzu moja kwa moja Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini pia kutokana na ligi hiyo kusitishwa kutokana na janga la corona, hakuna timu iliyoshuka daraja msimu huu, huku timu mbili zikipandishwa.

Nchini Tanzania, nako kumekuwa na mijadala inayoendelea kwenye redio, televisheni, mitandaoni na hata vijiweni juu ya mustakabali wa ligi hiyo, kama janga litaendelea kuwa kubwa na serikali ikaendelea kusimamisha michezo yote nchini.

Wengine wanadai ligi ifutwe na msimu huu kusiwe na bingwa, badala yake timu zianze kujiandaa na msimu ujao. Kuna baadhi yao wanadai ligi ifutwe, lakini anayeongozwa apewe ubingwa wake. Wapo wanaotaka ligi ikifutwa, basi bingwa wa msimu uliopita ndiye awakilishe nchini kwenye michuano ya kimataifa.

Hata hivyo, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wilfred Kidao, akizungumza na wanahabari majuzi, alisema mustakabali wa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara utaamuliwa na vikao maalum, iwapo tu janga hili litaendelea na kuwa tishio na si vinginevyo na kuongeza kuwa, hata hivyo bado ni mapema kuliongelea suala hilo.

"Bado ni mapema sana kusema tumefuta msimu, pamoja na kwamba msimu unaweza kwenda hadi Juni 31," alisema.

Kwa maana hiyo ili kuwa na uwezekano na ligi kufutwa ni lazima kwanza ifike Juni 31 na ligi iwe bado imesimama. Hata hivyo, kuna athari kubwa kama Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu itafutwa.

Katika makala haya tumekukusanyia baadhi ya athari iwapo jambo hilo litatokea, tiririka nayo....

**1. Michuano ya Kombe la FA nayo kufutwa**

Kwa sababu yote ni michezo ya soka, hivyo sababu zitakazofanya Ligi Kuu kufutwa ndizo hizo hizo zitaifanya michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), maarufu kama Kombe la FA nalo kufutwa msimu huu pia.

Kwa maana hiyo, timu zote zilizofanikiwa kuingia hatua ya robo fainali nazo pia hazitocheza tena, ikiwamo Simba, Yanga, Azam na Namungo ambazo zilikuwa zikipigana vikumbo kuwania kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

**2. Simba, Azam kuwakilisha tena nchi**

Iwapo Ligi Kuu msimu huu itafutwa na kama Simba itapewa ubingwa kwa sababu inaongoza ligi, basi itaiwakilisha nchi msimu ujao kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na kwa sababu FA haitokuwapo, Azam FC itaiwakilisha nchini kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho kiulaini kwa sababu ndiye bingwa wa msimu uliopita.

**3. Mechi Simba, Yanga na zote msimu huu kufutwa**

Kama corona ikiendelea bila ufumbuzi na ikaamuliwa Ligi Kuu ifutwe ni kwamba mechi zote 284 zilizochezwa msimu huu mpaka sasa zitakuwa zimefutwa na hazitowekwa kwenye rekodi yoyote ile kwa sababu ligi haikukamilika. Kadhalika, mechi zote mbili za Simba na Yanga nazo ni kati ya mechi 284, hivyo hazitokuwamo kwenye rekodi yoyote ile ya mechi za Ligi Kuu baina ya watani wa jadi kwa sababu ligi imefutwa.

Kwenye mechi ya kwanza Januari 4, mwaka huu, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2 na Machi 8, mwaka huu, Yanga iliichapa Simba bao 1-0 lililofungwa na Benard Morrison. Hapa ni kwamba Yanga itaathirika na rekodi yake kwenye mechi hizi, hasa ya pili.

**4. Timu za Daraja la Kwanza kutopanda**

Gwambina FC ni moja kati ya timu zenye uhakika wa moja kwa moja msimu ujao kucheza Ligi Kuu, kama Ligi Daraja la Kwanza itaendelea.

Timu za Ihefu FC na Dodoma FC nazo zinapigana kufa na kupona kuhakikisha zinapanda.

Kama corona ikiendelea kuwa tishio na kusababisha ligi kufutwa, kuna uwezekano mkubwa timu zisishuke daraja msimu huu. Na kama hazitoshuka, basi hakutokuwa na timu yoyote itakayopanda Ligi Kuu msimu ujao.

Hii inatokana na kwamba tayari Ligi Kuu ina timu 20 na zilitakiwa zishuke nne na msimu ujao kuwe na timu 18 tu. Kwa maana hiyo sidhani kama TFF inaweza kuruhusu timu 22 au 24 msimu ujao.

**6. Hasara kwa wadhamini wa Ligi, klabu**

Kampuni iliyoingia mkataba wa kuonyesha mechi itakuwa imeingia hasara kwa sababu haitoonyesha tena ligi kwenye mechi zilizobaki, lakini pia kampuni ambazo zilikuwa zinatangaza bidhaa zao kwenye jezi za klabu, nazo pia zitakuwa zinahesabu maumivu kwa sababu hazitopata tena nafasi hiyo.



Winga wa Yanga, Bernard Morrison (kushoto), akishangilia na wenzake baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Simba Machi 8, mwaka huu. Endapo Ligi Kuu Bara ikifutwa, ushindi huo nao utafutwa kwenye rekodi ya watani hao wa jadi.
**PICHA: MAKTABA**

**NAJUA WAJUA**

KIPA wa Liverpool, Alisson ndiye mlinda mlango wa kwanza kutoa pasi ya mwisho 'assist' kwenye Ligi Kuu England tangu Machi 2010 wakati Pepe Reina alipofanya hivyo wakati 'Wekundu' hao wakicheza dhidi ya Sunderland.



SOKA



# SABABU SALAH ANASTAHILI TUZO MCHEZAJI BORA EPL

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah amekuwa mmoja wa wachezaji bora kwa Jurgen Klopp tangu aliposajiliwa Liverpool mwaka 2017. Klopp ameweka imani yake kwa mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea raia wa Misri, tangu alipomsajili kutoka AS Roma kwa ada ya euro milioni 42.

Salah amelipa fadhila ya kuaminiwa na kocha huyo raia wa Ujerumani kwa mabao mengi na pasi za mwisho za kutosha. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ameichezea mechi 100 Liverpool kwenye Ligi Kuu na kufunga mabao 70 kwa kipindi chote hicho.

Liverpool imejipambanua kwa kuwa na safu bora zaidi ya ushambuliaji ya watatu mbele, Sadio Mane, Roberto Firmino na Salah ambao kwa pamoja wametengeneza moja ya safu bora zaidi ya ushambuliaji.

Baada ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019, kitu pekee kilichobaki kwa vijana hao wa Klopp ni kubeba taji la Ligi Kuu ya England. Liverpool ipo kwenye nafasi ya kulitwaa taji hilo walilolisubiria kwa muda mrefu wakiwa wanaongoza kwa tofauti ya pointi 25 dhidi ya Manchester City waliopo nafasi ya pili.

Salah ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka Ligi Kuu England mwaka 2018 na sasa anaangaliwa kama ataweza kuitwaa tena msimu huu, lakini anakabiliwa na ushindani mkubwa kutoka kwa Kevin De Bruyne, Jamie Vardy, Jordan Henderson, Virgil van Dijk na Mane.

Hapa tunaangalia sababu tatu kwa nini Salah anastahili tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka Ligi Kuu msimu huu, hizi hapa...

**#1 Mfungaji anayeongoza Liverpool**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Misri ndiye anayeongoza kwa ufungaji bora mbele ya Mane na Firmino. Amefunga mabao 16 kwa kikosi chake katika Ligi Kuu msimu huu na anaweza kufunga mengi zaidi kabla ya msimu kufungwa.

Salah anashika nafasi ya tatu katika orodha ya wafungaji bora kwenye Ligi Kuu akiburuzwa na Jamie Vardy na Pierre-Emerick Aubameyang ambao wamefunga mabao 19 na 17 kwa majina yao. Na huku Liverpool wakiwa wamebakiwa na mechi tisa ili kumaliza ligi, anaonekana anaweza kuwapiku wote wawili na kutwaa Kiatu cha Dhahabu.

**#2 Asisti za kutosha**

Pamoja na kufunga mabao, Salah anapenda kuwatengeneza wachezaji wenzake pia. Ana 'asists' pasi za mwisho sita kwa jina lake na ametengeneza pasi muhimu 47, akitengeneza nafasi 53 kwa Liverpool kwenye mechi 26 za Ligi Kuu alizocheza.

Salah amepiga chenga mara 44 sawa na aslimia 61. Zaidi ni kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ana wastani wa kufunga kila baada ya dakika 140. Salah pomoja na Mane na Firmino wametengeneza safu hatari zaidi kwa timu pinzani.

**#3 Mshindi wa mechi**

Salah amejithibitisha yeye mwenyewe kweye matukio kadhaa kwamba, Liverpool wanaweza kumtegemea zaidi kwenye wakati mgumu. Mshambuliaji huyo wa zamani wa Roma amefunga mabao kadhaa ya kusawazisha na ushindi kwa kikosi cha Klopp msimu huu na kuendeleza rekodi yao nzuri hadi walipokumbana na kipigo cha kushitukiza kutoka kwa Watford msimu huu.

Wekundu hao walikuwa hawajafungwa katika mechi 27 za Ligi Kuu, kabla ya kupoteza kwa Watford. Lakini mchezaji pekee aliyeonyesha uhai wa Liverpool alikuwa ni Salah. Alionyesha kiwango cha kuvutia kwa kuwapa presha muda wote wa mchezo.

Salah ameiokoa mara kadhaa timu yake na amefunga mabao ya ushindi mengi kwa timu hiyo tangu mwaka 2017. Ameendelea kuwa kwenye rekodi yake msimu huu, akiwa amefunga mabao saba ya ushindi ambayo ni mengi zaidi kwa mchezaji wa Ligi Kuu.

NDANI YA 18



Gareth Barry mwenye umri wa miaka 39, ambaye kwa sasa anaichezea klabu ya Championship (Ligi Daraja la Kwanza England), West Bromwich Albion, ndiye mchezaji anayeshikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi za Ligi Kuu England (653), akifuatiwa na Ryan Giggs (632) pamoja na Frank Lampard (609).

Nipashe
Spotika



HUKU michuano ya soka duniani ikiwa imesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, kitu kimoja kinaweza kuwa hewani katika dirisha la usajili linalokuja.

Uk. 16-17

# KWA NINI CEBALLOS ABAKISHWE ARSENAL?

**LONDON, England**

JE, Dani Ceballos amefanya ya kutosha hadi anunuliwe kwa kitita cha fedha ndefu Arsenal? Ana uwezo wa kuziba pengo la Aaron Ramsey? Kuna nafasi ya kumsajili mwingine zaidi ya yeye? Maswali yanaendelea kutiririka kumhusu Ceballos pale katika klabu ya London Kaskazini, kama anatakiwa kubaki kwa kupewa mkataba wa kudumu au kurudishwa kule Real Madrid. Lakini baada ya mjadala mrefu mashabiki wengi wa Arsenal wanaamini kwamba anafaa kupewa mkataba.

Tangu alivyoanza kucheza kwenye Ligi Kuu ya England katika mchezo dhidi ya Burnley, Ceballos amekuwa kipenzi cha mashabiki pale katika dimba la Emirates.

Ni mchezaji mwenye ubunifu na mwenye uwezo wa kutawala presha ya mchezo, mashabiki wengi wamekuwa wakivutiwa na aina ya uchezaji wake, mbinu na akili ya mchezo.

Kinachosemwa kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 ni kwamba, tangu katikati ya Agosti ametengeneza pasi za mwisho mbili. Lakini amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara, huku pia ugumu wa ligi hiyo nayo umefanya kuwa na wakati mgumu pia.

**Nini kinamfanya Ceballos bora?**

Ubora wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania wa kuhimili presha kwenye hali ngumu, uwezo wa kumiliki mpira na kutengeneza nafasi ni kati ya vitu vichache ambavyo anavyo. Uwezo mkubwa wa kuwatengenezea nafasi wachezaji wenzake dimbani ni mkubwa, ana wastani wa pasi 70 za uhakika (sawa na asilimia 88.9).

Staili ya uchezaji ya Ceballos ni ya kuvutia, anakuwa mchezoni na kujituma kisawasawa. Jambo la muhimu zaidi ni uwezo wake wa ulinzi umechangia matokeo ya kujitolea - akiwa na wastani wa kukaba wa 2.7 na kuzuia mipira kwa asilimia 90. Ukimchezesha kwa pamoja na Lucas Torreira kwenye nafasi ya kiungo, wanatengeneza upatina wenye thamani kubwa zaidi.

Kocha Mikel Arteta, anatakiwa kutokuacha kutumia mfumo wake wa 4-2-3-1, ili kuipa nguvu zaidi safu ya kiungo. Nyota huyo wa Real Madrid tangu alipotua kwa mkopo hapo London kipindi cha majira ya joto kilichopita amekuwa na kiwango cha kuvutia. Hata hivyo, anakosa mchango kwenye mabao.

Huku akiwa na 'asists' pasi za mwisho mbili na bao moja tu kwenye mechi 24 katika mashindano yote, Ceballos atatakiwa kufanya kazi ya ziada kuisaidia safu ya ushambuliaji na hilo linaweza kumfanya apate nafasi ya kuendelea kubakia pale Arsenal mwishoni mwa msimu huu.

**Dili linaweza kukwama?**

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa mpya kuhusu hali halisi ya Ceballos. Kwa mujibu wa gazeti la Evening Standard, Arsenal inapanga kuongeza mkataba wake wa mkopo baada ya Juni 30.

Na hiyo ni kutokana na ukweli kwamba, yeye ni vigumu kupata namba kwenye kikosi cha kwanza cha kocha Zinedine Zidane pale Real Madrid. Nyota wa Ajax, Donny van de Beek na Paul Pogba wa Manchester United wote wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kutua kule Bernabeu na hivyo kumfanya Ceballos kutokuwa na namba pale.


Akiwa na thamani ya euro milioni 40, anaweza kupatikana kwa kiasi cha chini ya hapo hadi euro milioni 25, na 'Los Blancos' hao wanaweza kuangalia uwezekano wa kumsajili kiungo mwingine kipindi cha majira ya joto.

Ni viungo wachache sana wenye ubora wake ambao wanaweza kupatikana kwa thamani ya euro milioni 30 au chini ya hapo sokoni kwa sasa, hivyo 'Washikabunduki' hao kwa namna yoyote ile wanatakiwa kuhakikisha wanambakisha mchezaji huyo kikosini kwa kumpa mkataba wa kudumu.




Ceballos

**USILOLIJUA**



KATIKA ligi tano bora Ulaya; Premier League, La Liga, Serie A, Bundesliga na Ligue 1, ni klabu ya Juventus ya Italia pekee, ambayo inashikilia rekodi ya kutwaa ubingwa kwa pointi nyingi (pointi 102), ikifanya hivyo katika msimu wa 2013-14.





Wakazi wa Kata ya Ikimba katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wakimwaga zege kwenye Kituo cha Afya cha Kata hiyo ambacho wameanza ujenzi wake, baada ya Serikali kuwapatia Sh. milioni 200 kwa ajili ya ujenzi huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mmalawi anaswa na kitambulisho cha mpigakura

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IDARA ya Uhamiaji mkoani Mbeya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na Usalama, inamshikilia raia wa Malawi, Tiddy Mwaisemba (48), akituhumiwa kuingia nchini kinyemela na dola za kimarekani 30,000 (milioni 68.1 za Tanzania) bila kufuata taratibu za usafirishaji wa fedha.

Akizungumza na wandishi wa habari ofisini kwake, Mkuu wa Idara Uhamiaji wa Mkoa wa Mbeya, Msafiri Shomari, alisema mtu huyo alikamatwa mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) akijiandaa kurejea Malawi.

Alisema mbali na kukutwa na fedha hizo, pia alipopekuliwa alikutwa na hati ya kusafiria ya Malawi na kitambulisho cha mpigakura ambacho kinatolewa na Tume ya Uchaguzi ya Tanzania (NEC) wakati yeye sio raia wa Tanzania na hastahili kuwa nacho. Alisema kwa mujibu wa sheria za fedha, mtu yeyote anayetaka kuingia nchini na fedha nyingi za kigeni, ni lazima afuate taratibu za forodha kwa kuzitolea maelezo na kwamba ataruhusiwa.

"Kitambulisho cha mpiga kura cha Tanzania ni haki ya raia wa Tanzania pekee, hivyo akikutwa nacho ambaye sio Mtanzania tafsiri yake ni kwamba alitoa taarifa za uongo ili akipate, sasa huyu tutamfikisha mahakamani kwa ajili ya hatua za kisheria," alisema Kamanda Shomari.

Mwaisemba alikiri kuwa raia wa Malawi wa kusajiriwa kwa maelezo kuwa ni mzaliwa wa Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya na aliamua kuwa raia wa Malawi baada ya kuwekeza zaidi katika nchi hiyo.

Alisema yeye pekee ndiye raia wa Malawi, lakini familia yake yote ipo Tanzania, na kwamba mke wake na watoto wanaishi jijini Dar es salaam ambako huwa anaenda mara kwa mara.

Alisema fedha alizokutwa nazo ni kiasi kilichobakia baada ya kufanya manunuzi ya vitu mbalimbali vya kwenda kuuza Malawi, na kwamba kitambulisho cha mpiga kura aliamua kukitafuta kwa sababu anampenda rais Dk. John Magufuli.

"Nina watoto sita ambao wote wanaishi Dar es Salaam na mke wangu, wote ni Watanzania pamoja na wazazi wangu, mimi peke yangu ndiye mmalawi, lakini huwa nakuja kununua mizigo huku na kwenda kuuza Malawi," alisema Mwaisemba.

Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) Mkoa wa Mbeya, imesema ni kosa kisheria kwa mtu yeyote kuingiza fedha za kigeni bila kibali na kwamba adhabu yake ni fedha hizo kutaifishwa ama kukatwa asilimia 10 kulingana na kiwango. Ofisa Elimu kwa Mlipa Kodi, Selapio Luanda, alisema endapo mtu ataingia nchini na fedha za kigeni zisizozidi Dola 10,000 na akakamatwa atatozwa faini ya asilimia 10 ya fedha hizo na kwamba fedha hizo zikizidi kiwango hicho zinataifishwa.

# Biashara mpaka wa Kasumulu kuendelea

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

PAMOJA na tishio la maambukizi ya ugonjwa wa corona nchini, Serikali imesema haitaufunga mpaka wa Tanzania na Malawi uliopo Kasumulu wilayani Kyela na badala yake shughuli zote zitaendelea kufanyika.

Akizungumza na baadhi ya wananchi katika mpaka wa Kasumulu wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema pamoja na kutoufunga mpaka huo, lakini kuna taratibu zilizowekwa kwa ajili ya kulinda mipaka.

Alisema Mtanzania yeyote ambaye ataenda Malawi kwa ajili ya shughuli zake, akirejea atawekwa karantini kwa siku 14 kwa ajili ya matazamio na kwamba baada ya siku hizo kama hataonyesha dalili za ugonjwa huo ataruhusiwa kuendelea na shughuli zake.

Chalamila alisema ipo Kamati maalumu ya Mkoa huo ambayo imeundwa kwa ajili ya kufanya shughuli ya kupambana na maambukizi ya ugonjwa huo ambao umekuwa janga la dunia.

"Muwe huru kabisa kwenda Malawi lakini ukirudi utatengwa kwa siku 14 na kwa gharama zako mwenyewe na madaktari wetu wataendelea kukuangalia mpaka siku ya mwisho," alisema Chalamila.

Alisema mpaka sasa hakuna mtu yeyote ambaye amebainika kuugua ugonjwa huo katika Mkoa wa Mbeya, hivyo akawataka wananchi waendelee kufuata taratibu wanazopewa na wataalamu wa afya ili mkoa huo uendelee kuwa salama.

Chalamila alisema vituo mbalimbali vimeandaliwa katika kila Wilaya mkoani humo kwa ajili ya kuwalaza wagonjwa wa Corona endapo itatokea ugonjwa huo ukaingia.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, alisema kwa sasa wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya namna ya kujikinga na ugonjwa huo kupitia vyombo vya habari na kuwatembelea wananchi kwenye maeneo wanayokutana kwa wingi.

Alisema magari yote ya abiria yamesisitizwa kuwa na maji tiririka na sabuni kwa ajili ya wagonjwa kunawa kabla ya kuingia kwenye magari hayo ili kuepuka kuambukizana.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuacha utamaduni wa kusalimiana mikononi na kukumbatiana kwa maelezo kuwa utamaduni wa aina hiyo unachochea maambukizi.

"Tuepuke maelezo ya watu ambao hawana utaalamu, maana kuna watu wanapotosha, tujitahidi kunawa mikono na kuepuka kugusana hasa na watu ambao wanaonekana kuwa na dalili za magonjwa ya mapafu," alisema Dk. Manyatta.

Hata hivyo, baadhi ya waendesha pikipiki za abiria (Bodaboda) walilalamikia baadhi ya maofisa kuwazuia kufanya shughuli zao katika mpaka wa Kasumulu wakati Serikali imewataka waendelee na shughuli zao.

Mmoja wa madereva hao, Jumanne Mwaijumba, alisema wanazuiliwa kufanya shughuli zao na kwamba wanaokaidi wanakamatwa na polisi na wengine wanatozwa faini.

## Sekta ya uwekezaji kuleta fursa nchini

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WATANZANIA wametakiwa kutambua kuwa sekta ya uwekezaji imekuwa na mchango mkubwa nchini kutokana na wawekezaji wengi kulipa kodi na kuongeza fursa za ajira.

Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimesema hali hiyo imekuwa ikichangia kuharakisha shughuli za kiuchumi na maendeleo ya wananchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja wa TIC, Venance Mashiba, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na hali ya uwekezaji katika mikoa ya nyanda za juu kusini.

Alisema wananchi wanapaswa kuwa na uhusiano mazuri na wawekezaji katika maeneo wanayoishi kutokana na kuwa wengi wa wananchi wanaokaa karibu na wawekezaji hao wamekuwa wanufaika wakubwa kutoka kwa wawekezaji hao katika ajira na huduma za kijamii.

Mashiba alisema ofisi ya tic imekuwa ikifanya jitihada za ziada kuhakikisha inawahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza katika mikoa ya nyanda za juu kusini kwa kuwa kuna fursa nyingi za uwekezaji katika Nyanja mbali mbali zikiwemo za kilimo.

"Katika mikoa ya nyanda za juu kusini kuna fursa nyingi katika sekta za kilimo, uchimbaji wa madini na usindikaji wa mazao ya kilimo na fursa zingine nyingi na kuwa ni muda mwafaka kwa wawekezaji wa ndani na nje kuchangamkia fursa hizo," alisema Mashiba.

Alisema umefika wakati kwa wawekezaji wa ndani kuhakikisha wanafika katika vituo vya uwekezaji kwa lengo la kufahamu na kuchangamkia fursa zilizopo hapa nchini na kutolea mfano kuwa wawekezaji wa ndani wanatakiwa kuwa na mtaji wa dola 100,000 na wawekezaji wa nje wanatakiwa kuwa na mataji wa dola 500,000.

Alisema ili kuhakikisha hali ya uwekezaji katika mikoa ya nyanda za huu kusini unastawi, ofisi hiyo imekuwa na mikakati endelevu ya mara kwa mara ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje pamoja na kuwajengea uwezo wananchi kutambua umhimu wa kuwekezaji.

"Alisema malengo ya TIC ni kuona wawekezaji na serikali zinanufaika katika uwekezaji hapa nchini, pamoja na wananchi katika maeneo ambayo wawekezaji wanawekeza," alisema Mashiba.

Alisema Ofisi ya TIC Kanda imekuwa ikifanya jitihada za kuhakikisha inatumia fursa za kuwahamasisha wawekezaji waliopo katika nchi jirani za Zambia na Malawi kuja kuwekeza katika mikoa ya nyanda za juu kusini na maeneo mengine ya nchi na kuwa mwaka jana kulikuwa na kongamano kubwa la uwekezaji kati ya nchi ya Tanzania na Malawi mkoani Mbeya.





# Akamatwa kwa kudaiwa kukwepa karantini

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, wamemkamata raia mmoja wa Marekani mwenye asili ya Tanzania, anayedaiwa kuingia nchini wiki nne zilizopita bila kukaa karantini ya siku 14 kuangalia kama ana virusi vya corona.

Machi 23, mwaka huu, serikali iliagiza wasafiri wote na wageni kutengwa kwenye hoteli na maeneo yaliyoandaliwa kwa siku 14 ili kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa huo.

Akizungumza mara baada kukamatwa kwa raia huyo, Katambi alisema alikamatwa juzi akiwa kwenye usafiri wa bodaboda baada ya kuingilia msafara wa viongozi waliokuwa kwenye ziara ya kikazi.

Alisema serikali imelazimika kufanya uchunguzi na kumuweka chini ya uangalizi wa timu ya wataalamu wa afya. "Raia huyu ametoa maelezo ya kujitetea kuwa alijiweka karantini kwa muda wa siku 14 nyumbani kwao, lakini hatuwezi kuyaamini moja kwa moja, hivyo lazima wataalamu wa afya wakamchunguze," alisema Katambi.

Akijitetea mbele ya Katambi, Raia huyo aliyefahamika kwa jina moja la Honeymoon, alisema alijiweka karantini ya nyumbani kwao kwa siku 14 katika chumba maalumu ambacho hakuruhusiwa kuingia mtu yeyote.

"Nyumbani kwetu kuna chumba ambacho ni maalumu kwa ajili ya mtu kujihifadhi hivyo nilivyoingia nchini nilijiweka karantini kwa muda wa siku 14 baada ya hapo ndipo nikaamua kutoka nje," alisema.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi), Mwita Waitara, akikagua moja ya darasa ambalo bado halijapauliwa katika Shule ya Msingi Manungu Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma.
**PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waitara aonya wazazi wanaotuma watoto minadani

**Na Augusta Njoji,**
KONGWA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, amewataka wazazi na walezi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona na kuacha kuwatuma kwenye watoto minadani.

Alitoa onyo hilo juzi alipokuwa kwenye ziara ya kikazi ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa madarasa ya Shule ya Msingi Manungu, Wilaya ya Kongwa na kutoa mabati 324.

Aliwataka kufuata maelekezo yanayotolewa na serikali pamoja na wataalamu wa afya kuepuka misongamano.

"Nitoe rai kwa wazazi na walezi wote nchini kuhakikisha wanachukua tahadhari dhidi maabukizi ya ugonjwa huu kwa watoto kwa kuwa hivi sasa wapo majumbani hivyo msianze kuwatuma kwa ndugu na minadani," alionya.

Alisema watoto hao wamezuiliwa kwenda shule ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa huo, isiwe sababu ya kufanya shughuli nyingine kwenye msongamano wa watu.

Alisisitiza kuzingatia kuosha mikono na maji tiririka, kutumia vitakasa mikono na taratibu nyingine zilizoelekezwa na wataalamu.

Kuhusu madarasa ya shule hiyo, Waitara alisema serikali imetoa mabati 324 kwaajili ya vyumba vya madarasa vitano yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi.

Alisema kutokana na juhudi za wananchi katika kushirikiana na serikali katika kuleta maendeleo kwenye sekta ya elimu ndani ya wiki mbili mabati yatakuwa yamewasilishwa katika shule hiyo ili kukamilisha ujenzi.

"Nataka shule zikifunguliwa baada ya janga la corona kuisha na wanafunzi wakirudi shule, madarasa haya yaanze kutumika ili kutatua uhaba wa madarasa katika shule hii, alisema.

Aliwapongeza wananchi wa Kongwa na Watanzania kwa moyo wa kujitolea na kuhakikisha wanajenga vyumba vya madarasa katika shule hiyo, ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha miundombinu ya elimu.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, alisema atahakikisha anasimamia vyema mabati hayo yaliyotolewa ili vyumba hivyo vya madarasa vikamilike na kutumika kwa wakati.

# Owenya ataka matibabu bure wenye VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (Chadema), Lucy Owenya, amewasilisha bungeni hoja binafsi kuhusu kuwapatia watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi huduma za matibabu ya magonjwa nyemelezi bila malipo.

Owenya aliwasilisha hoja hiyo bungeni mwishoni mwa wiki chini ya Kanuni ya 28(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Katika hoja yake, Mbunge huyo alisema maambukizi ya Ukimwi ni janga ambalo limeangamiza nguvu kazi kubwa ya taifa na kuzima ndoto za maelfu ya watoto, vijana na hata wazee.

Alisema pamoja na serikali kugharamia dawa za kupunguza makali au kufubaza VVU (ARVs), magonjwa nyemelezi yamekuwa msumari wa moto kwa wenye maambukizi.

"Matibabu ya magonjwa haya yanahitaji uchunguzi wa kina na wenye gharama kubwa na mara nyingine matibabu huchukua muda mrefu au kujirudiarudia," alisema.

Alisema kundi kubwa la watu wenye maambukizi hasusan vijijini mara nyingi hawazalishi ipasavyo kwa sababu ya hali zao za kiafya.

"Wengi wanaishi katika hali ya umaskini, hali hii hupelekea ulaji hafifu na kushindwa kumudu gharama kubwa za matibabu katika hospitali zetu na vituo vya afya na hatimaye kusababisha vifo vya mara kwa mara vitokanavyo na magonjwa nyemelezi," alisema.

Owenya alisema pamoja na huduma zinazotolewa na Bima ya Taifa ya Afya, vifurushi vya matibabu kwa njia ya bima vina gharama kubwa, hasa kwa kundi hilo ambalo kila mara linasumbuliwa na maradhi.

"Kwa hali ya uchumi ilivyo na inavyozidi kuwa ngumu ni dhahiri wengi wa wagonjwa wanashindwa kumudu gharama za matibabu, kutokana na uzito wa tatizo hili la gharama za matibabu kwa wenye mambukizi ya VVU ambao kila mara hukumbwa na magonjwa nyemelezi," alisema.

Alishauri wakati huu serikali kuridhia kutoa huduma za matibabu ya magonjwa nyemelezi bila malipo kwa kundi la wagonjwa wenye maambukizi hayo wanapohitaji matibabu kwenye zahanati, vituo vya afya au hospitali za serikali. Alisema nchi kama Brazil na Argentina zimefanikiwa kupunguza maambukizi na vifo vinavyotokana na Ukimwi kutokana na uamuzi wa serikali kutoa huduma za matibabu bila malipo kwa wenye maambukizi.

"Kutoa matibabu bure sio tu kutapunguza maambukizi bali kutachochea hamasa zaidi ya watu wengi kwenda kupima hali zao... itasaidia malengo ya serikali ya kupunguza maambukizi ifikapo 2030,"alisema.

Awali, alisema kwa mwaka 2018, takribani watu milioni 1.6 waliishi na VVU nchini na kiwango cha maambukizi kikiwa ni asilimia 4.6 kwa wenye umri kati ya miaka 15-49 huku maambukizi mapya yakifikia takribani watu 72,000, na vifo 24,000 kwa mwaka.

Pia, alisema takribani asilimia 72 ya watu waliokuwa wakiishi na VVU walikuwa wanatumia dawa za kufubaza virusi huku watoto ni asilimia 65. "Kwa hali ilivyo sasa tafiti zinaonyesha kuwa, kila siku takribani watu 225 huambukizwa virusi vya Ukimwi na kati yao 90 ni vijana, maambukizi mapya kwa mwezi ni takribani 6,750 hii ikiwa na maana kwamba kila saa watu tisa hupata maambukizi mapya," alisema.

Alisema takwimu hizo zinahitaji taifa kuwa na mkakati mahususi na wa dharura wa kuangalia janga hilo kwa mapana zaidi.



# Muswada kudhibiti vileo wakataliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameukataa Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Vileo uliowasilishwa katika kikao Cha Baraza la Wawakilishi na Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, Haji Omar Kheir.

Wakati wakichangia Muswada huo Wajumbe wengi walikataa kukubali kwa maelezo kwamba hautoshelezi katika kudhibiti athari mbaya za ulevi na ongezeko la baa katika visiwa vya Zanzibar.

Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Mohammed Said Dimwa, alisema Serikali imeleta Muswada huu baada ya miaka karibu 92, lakini bado hauonyeshi udhibiti makini wa vitendo vya ulevi na ongezeko la baa nchini.

"Mwenyezi Mungu akusamehe Mheshimiwa Waziri na Kamati ya Sheria iliyopitia Muswada huu, umebebeshwa msalaba huu peke yako, sheria zote zinaletwa humu Mwenyekiti wa Bodi anateuliwa na Rais, lakini sheria hii tu Bodi yake Mwenyekiti anateuliwa na Waziri," alisema Mohamed na kuongeza:

"Mimi sitaki kuingia kwenye kumbukumbu ya kupitisha Muswada huu, siungi mkono."

Alisema anashangaa Muswada huo umeweka adhabu ndogo sana ya faini ya Sh. 500,000 au kifungo cha miezi mitatu kwa watakaofanya biashara za ulevi katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, na kuwa adhabu hiyo haiwezi kudhibiti kwa vile wafanyabiashara wa pombe wanamudu kulipao faini hiyo na kuendelea kukashifu Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Aman, Rashid Ali Juma, alisema haungi mkono sheria hiyo kwa vile alitegemea ingekuja kuweka udhibiti na marufuku ya biashara hiyo kwa kuwa jimboni kwake tu baa zimekuwa nyingi sana na maeneo mengine ya nchi.

Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Mussa Ali Mussa, alitoa tahadhari kuwa Muswada huo siyo wa kuletwa kwa wakati huu kwa namna ulivyo kwa sababu haujaweka udhibiti wa kutosha wa biashara holela ya pombe.

Mwakilishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliishauri Serikali kurudi tena kufanyia marekebisho Muswada huo na kuweka masharti yatakayodhibiti ueneaji wa biashara ya pombe mitaani.

Aliitaka Serikali kufikiria baadhi ya nguvu alizopewa Waziri katika Muswada ni kubwa mno kwa kuwa anaweza kumuondoa Mjumbe wa bodi wakati wowote anaopenda bila kueleza sababu.

Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe, Ramadhan Hamza Chande, alisema haungi mkono Muswada huo mpaka hapo yatakapowekwa masharti ya msingi ya kukataza au kudhibiti vikali biashara ya ulevi nchini.

Akitoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja za Wajumbe Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Ussi Gavu, aliwaomba Wawakilishi hao kuupitisha Muswada huo kwani nia ya Serikali ni nzuri ya kuhakikisha inaweka udhibiti wa biashara ya vileo.

Aliwataka Wajumbe kupendekeza zaidi maeneo ambayo yafanyiwe marekebisho ili kuweka udhibiti mkali wa vileo badala ya kuukataa Muswada huo.

Hata hivyo Mswada huo haukupitishwa na Mwenyekiti wa Baraza aliyekuwa anaendesha kikao, Mwanaasha Khamis Juma, aliakhirisha kikao hicho na kumtaka Waziri kwenda kujiandaa vizuri na majibu ya hoja za Wajumbe.




Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed Said (kushoto), akikabidhi vifaa vya maji (mipira) na tanki kubwa kwa jimbo lake la Tunguu jana. Kulia ni Diwani wa Wadi ya Tunguu, Hadhar Abdalla. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Msajili atakiwa kuwatathmini wanasiasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BAADHI ya viongozi wa Vyama vya Siasa Zanzibar, wamemtaka Msajili wa vyama hivyo kutathmini kauli za baadhi ya viongozi wa vyama hasa wakati huu taifa linaeleka katika uchaguzi mkuu.

Akitoa tamko la Umoja wa Vyama vya Siasa Zanzibar, Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassan Ameir, alisema kauli hizo zinaashiria kuleta uvunjifu wa amani. Alisema, umoja wao unaridhishwa na utendaji wa serikali kwa kuwafikishia wananchi wake maendeleo na kudumisha amani, mshikamano na ustawi wa jamii.

Aidha, aliishauri Ofisi ya Msajili kuvifuta vyama vya siasa vinavyokwenda kinyume na havitakii mema nchi.

Akizungumzia Tume huru ya Uchaguzi iliyoundwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Ali Mohamed Shein, Ameir alisema, vyama vya siasa vyote vilishauriwa katika mchakato mzima wa kuundwa tume hiyo.

"Sisi viongozi wa vyama vya siasa kwa upande wa Zanzibar tumeridhishwa na uteuzi wa Tume uliofanywa na Rais ambao umekusanya wataalamu kutoka vyama mbalimbali vya siasa," alisema.

Hata hivyo, viongozi hao walishauri serikali kuangalia upya muundo wa serikali ya Umoja wa kitaifa ili kushirikisha vyama vyote vya siasa katika kuunda serikali.

Akizungumzia ugonjwa wa corona, alipongeza juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kupambana na ugonjwa huo, ambao umekuwa tishio na kuuwa watu wengi duniani.

Hivyo, aliwaomba wananchi kuwa watulivu na wafuate maelekezo yanayotolewa na viongozi wakuu pamoja na wataalamu wa afya katika kujikinga na janga la corona.

Vyama vilivyoshiriki katika tamko hilo, ni Demokrasia Makini, SAU, UPDP, NLD, DP, TLP, CCK, CCM, TADEA, AFP, NCCR-Mageuzi na ADC.

## Corona yasitisha kambi ya dagaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

Mkoa Mjini Magharibi umesimamisha kambi ya waanika dagaa katika Shehia ya Kihinani ili kunusuru athari za maambukizi ya maradhi ya corona.

Akizungumza katika ziara maalum iliyowashirikisha viongozi wa Wilaya na Manispaaa ya Magharibi 'A' Unguja kwa wafanyabiashara wa mkaa,wavuvi na waanika dagaa, Mkuu wa Mkoa wa Mjini, Hassan Khatib, alisema serikali imefanya uamuzi huo kwa kipindi hichi cha mlipuko wa maradhi hayo hadi hali itakapokuwa vizuri.

Alisema kwa sasa hakuhitajiki mikusanyiko, hivyo aliwaomba wananchi kuwa na subira, na kufuata maelekezo ya serikali na wataalamu wa afya.

"Tunaomba tuwe wastahamilivu kutokana na hali hii ya maradhi, kwani maradhi yapo tusidharau na tusiwe na dhana kuna maradhi haya ni ya watu weupe tu...tujikinge ili tubaki salama tupate kuendelea na shughuli zetu kama kawaida," alisema Hassan.

Aidha, aliwataka wavuvi, wafanyabiashara na madalali wa samaki katika eneo hilo kuchukua tahadhari maalum kuondoa misongamano na mikusanyiko ya watu.

Alisema ni vyema watu wakaenda kwa utaratibu maalum wa kununua samaki na bidhaa nyingine, na kuondoka badala ya kufanya sehemu hiyo kuwa ya mazungumzo.

"Naomba viongozi na wasimamizi wa maeneo haya tujitahidi hapa kuwaelemisha watu wetu wanaoingia katika eneo hili, ni vyema wafuate huduma na kuondoka," alisema.

Hata hivyo Hassan alipongeza umoja wa wauza mkaa wa eneo la Kihinani kwa utaratibu mzuri waliouweka wa kupeana zamu za kufanya biashara na kuepusha mikusanyiko huku wakifuata maelekezo ya wataalamu wa afya wa kuweka sehemu za kunawia mikono kwa watu wanaofuata huduma.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Magharibi 'A' Unguja, Amour Ali Mussa, alisema uongozi wa manispaa hiyo utaendelea kufanya kazi kwa karibu na viongozi wa jumuiya za wafanya biashara wa maeneo hayo ili kuona elimu ya afya inatolewa mara kwa mara kwa lengo la kuepusha mikusanyiko utakaosababisha maambukizo ya corona.

Kwa upande wao wanika dagaa wa eneo hilo walisema wamepokea maelezo yalitolewa na Mkuu wa Mkoa, na kuahidi kuwa watayatekeleza ili kunusurika na maambukizi ya corona.

# Shule 119 zaanza kilimo cha michikichi

**Na Ashton Balaigwa,**

KIGOMA

WANAFUNZI na walimu katika shule za msingi 119 na sekondari 16 wilayani Uvinza, mkoani Kigoma, wameanza kilimo cha michikichi ikiwa ni kuitikia agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa la kila taasisi kulima zao hilo ili kusaidia uzalishaji wa mafuta ya kula nchini.

Hatua hiyo inatokana na mikakati iliyowekwa na viongozi wa Wilaya ya Uvinza ya kuhamasisha kilimo hicho cha kwa taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali baada ya kutenga eneo la kutosha kwa ajili ya kilimo hicho pamoja na kujitokeza kwa mwekezaji kuonyesha nia ya kujenga kiwanda cha kisasa cha kukakamua mafuta hayo.

Akitoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari), Dk. Yohana Budeba, aliyetembelea wilaya hiyo kuangalia utekelezaji wa taasisi hiyo kufuatia wa agizo la Waziri Mkuu, Ofisa kilimo wa wilaya hiyo, Masolwe Salum, alisema mwitikio huo umetokana na Tari kwa kushirikiana na halmashauri hiyo kuzalisha vitalu vya mbegu za michikichi na kuzigawa bure kuhamasisha kilimo hicho.

Masolwe alisema, kitendo cha Tari kuzalisha mbegu hizo za kisasa aina ya Tenera na kuamua kugawa bure kwa wakulima na taasisi zinazotaka kulima kilimo hicho cha michikichi kimechochea kwa kasi watu kujitokeza kwa wingi na kuongeza kilimo hicho kutoka hekta 8,013 za zamani zilizokuwa zikilimwa ili kufikia hekta 32,462 zinazofaa kwa kilimo hicho.

"Hii miche ya michikichi aina ya Tenera inauzwa bei kubwa mmoja ni Sh. 6,000, sisi tulinunua na kugawa kwa baadhi ya taasisi chache ili kulima kilimo hicho, lakini baada ya serikali kupitia Waziri Mkuu kuipa majukumu Tari kuzalisha mbegu za miche hiyo na kutupatia bure miche 26,054 yenye thamani ya Sh. milioni 156 ili kuigawa bure, mwitikio ni mkubwa na mahitaji yameongezeka," alisema Masolwa.

Kwa upande wake, Ofisa Elimu Kilimo wa Wilaya ya Uvinza, Shingwa Hamisi, alisema baada ya agizo hilo walipita katika shule 16 za kata wilayani humo na kuhamisha kilimo hicho na mwitikio umekuwa mkubwa na tayari shule hizo zimeanza kutengenezewa vitalu vya uzalishaji wa mbegu hizo na nyingine zimeanza kilimo hicho kwaajili ya kuwafundisha wanafunzi ili wanapohitimu walime kilimo hicho.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyangabo, Parashido Sanga, alisema wameanza kupanda ekari sita kwaajili ya mradi wa kuongezea kipato shule hiyo na mkakati kufikia ekari 10 ili katika siku za usoni waweze kuondokana utegemezi wa fedha za kujiendesha kutoka serikalini.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, akimkabidhi hati ya umiliki ardhi Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, wakati wa ugawaji hati katika Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Wananchi waanza kunufaika vyoo bora

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WANANCHI wa Kijiji cha Mapilinga, Kata ya Igokelo wilayani Misungwi, mkoani Mwanza, wameanza kunufaika na mradi wa usafi wa mazingira kwa wote ili kukabiliana na changamoto ya vyoo kutitia.

Mradi huo unaotekelezwa na Netherland Development Organization (SNV) na serikali kupitia Idara ya Afya, umelenga kuwasaidia wananchi hao kukabiliana na changamoto ya kutitia kwa ardhi, ni ujenzi wa vyoo aina safi ambavyo vinawekwa sinki maalumu la kuzuia kutitia kwa ardhi.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wanufaika wa mradi huo, walisema ujio wa mradi huo ni ukombozi kwao baada ya vyoo vyao kutitia mara kwa mara. Mmoja wa wananchi wa kijiji hicho ambaye ni mnufaika, Jeremiah Tabula, alisema shida ilikuwa ni vyoo kubomoka mara kwa mara.

"Kwenda kutafuta mahala pa kujisaidia ilikuwa ni shida sana kwa kuwa awali tulikuwa na vyoo vya kawaida vya kuchimba shimo na kuweka miti ambavyo vilikuwa vinabomoka na kuanza kujenga upya kila mara," alisema Tabula.

Felister Mussa, alisema waliamua kujenga choo hicho kwa sababu ya usafi wa nyumbani, pia ni bora na kinachodumu, awali ilikuwa wakichimba choo baada ya miezi michache kinabomoka," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mapilinga Sospeter Cornely, alisema mradi huo umepokelewa vizuri kwa sababu ni wa gharama nafuu.

Wakala wa Shirika la SNV, Kata ya Igokelo, Anthon Faustini, alisema ni mradi ambao umekuja kwa wananchi kwa ajili ya usafi wa mazingira pamoja na kuwapunguzia gharama.

Naye msimamizi wa uzalishaji na uuzaji wa vyoo hivyo, Wilaya ya Misungwi, Paul Sanga, alisema ni teknolojia mpya ambayo imebuniwa kwaajili ya kukabiliana na changamoto ya kutitia kwa ardhi ambayo imekuwa ikitokea maeneo mengi ya Kanda ya Ziwa hasa katika maeneo ambayo walikuwa wakifanya kazi.

Alisema, mradi huo utamfikia kila mtu lengo ni jamii na taasisi kuboresha vyoo ili kujikinga na magonjwa yanayoambukizwa.

"Asilimia 75 ya ardhi ya kijiji cha Mapilinga ni mchanga walichimba choo kinatitia kwa muda mfupi, hivyo katika mradi huo likishachimbwa shimo wanaweka ringi ambayo inasaidia ardhi kutotitia na kufanya choo kuwa bora na salama kwa familia na mpaka sasa watu saba wamenufaika na mradi huu," alisema Sanga.

# PAET yalipa kodi ya nyongeza serikalini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya PanAfrican Energy Tanzania Limited (PAET), imelipa kodi ya nyongeza inayotokana na faida ya Sh. bilioni 27.3 kwa serikali.

Mkurugezi Mtendaji wa PAET, Andy Hanna, alisema hayo hivi karibuni na kueleza kuwa malipo hayo yameifanya PAET kuwa kampuni ya kwanza inayojishughulisha na mafuta pamoja na gesi kulipa aina hiyo ya kodi kwa serikali.

Alisema kodi iliyolipwa hivi karibuni inadhihirisha thamani ya kampuni kwa wananchi wa Tanzania.

"Kampuni yetu ndogo, inayoundwa kwa kiasi kikubwa na Watanzania wazawa, inajivunia kufikia mafaniko haya na tunategemea kwamba kutakuwa na malipo mengine ya aina hii kwa miaka mingine ijayo," alisema.

Alisema kampuni hiyo inaongoza kwa uzalishaji wa gesi kutoka Songo Songo na kuisafirisha mpaka jijini Dar es Salaam ambapo hutumika katika shughuli za kuzalisha umeme.

"Gesi hiyo pia inatumika kuendesha shughuli za uzalishaji katika viwanda vikubwa zaidi ya 40 jijini Dar es Salaam pamoja na kusambaza gesi asilia iliyogandamizwa yaani Compressed Natural Gas (CNG) kwa ajili ya kutumika kwenye vyombo vya usafiri kama magari, hoteli na viwanda," alisema.

Hanna alisema mkataba wa uzalishaji wa gesi asilia ya Songo Songo ulitiwa saini mwaka 2001 baina ya Serikali ya Tanzania na PAET.

"Mkataba huu unatoa mwongozo wa namna uzalishaji wa gesi unavyopaswa kufanyika pamoja na jinsi mgawanyo wa mapato unavyopaswa kuwa baina ya pande hizi mbili," alisema.

Alisema baada ya kuzalisha gesi asilia kwa zaidi ya miaka 15, kipengele hiki maalum cha mkataba hatimaye kimeweza kutumika.

"Linaweza kuonekana jambo geni kidogo kulizungumzia, lakini tunashukuru kwamba tumeweza kufanikiwa kutekeleza malipo haya makubwa na ya aina yake.

"Mpaka mwishoni mwa mwaka 2019, kampuni imeweza kuilipa Serikali ya Tanzania kiasi cha Sh. bilioni 555 kama kodi mbalimbali na kiasi cha Sh. bilioni 160 kama mgawanyo wa faida."

## China yawaenzi wahudumu wa afya waliofariki kwa corona

**BEIJING, China**

CHINA imefanya maadhimisho ya kuwakumbuka wahudumu wa sekta ya afya waliofariki wakati wakiwahudumia wagonjwa wa virusi vya corona.

Tukio hilo lililochukua muda wa dakika tatu za watu wote kukaa kimya huku bendera zikipeperushwa nusu mlingoti, kwa taifa zima kuwaenzi na kuwakumbuka wahudumu hao, wafanyakazi waliokuwa mstari wa mbele katika vita vya kupambana na ugonjwa huo.

Rais wa China, Xi Jinping alikuwapo katika kumbukumbu hiyo ya kitaifa mjini Beijing pamoja na viongozi wengine wa China mbele ya bendera ya taifa, vyombo vya habari vya serikali vimeripoti.

Virusi vya corona mara ya kwanza viliibuka mwisho wa mwaka jana huko China katika jimbo la Hubei, na kuua watu zaidi ya 3,300.

Kumekuwapo na malumbano iwapo China imekuwa wazi kutoa takwimu za afya juu ya virusi hivyo na tarehe ambayo virusi hivyo viliibuka.

Wakati China ikionekana kuwa inarejea katika hali ya kawaida baada ya kuwapo athari za virusi hivyo, maradhi hayo ya kuambukiza yameenea ulimwenguni, huku kukiwa na hali ya kukata tamaa na vifo.

Idadi ya maambukizi inaendelea kuongezeka wakati zaidi ya maambukizi milioni moja yakithibitishwa ulimwenguni na takriban vifo 60,000.

Marekani hivi sasa ndio penye maambukizi mengi ya virusi hivyo na watu walioambukizwa ni zaidi ya 278,000, lakini serikali yake bado haijakubali kuchukua hatua za pamoja kupambana na ugonjwa huo.

Badala yake Rais Trump ameyaambia majimbo wajitegemee kupambana na hali hiyo ambayo wakati huduma za afya zimeelemewa kutokana na janga hili.

Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia maambukizi (CDC) kimependekeza kuwa watu wavae barakoa kwenye mdomo na puani hata zisizokuwa za tiba kuzuia kuenea kwa virusi vya corona, wiki kadhaa baada ya kuuhakikishia umma kuwa barakoa hazikuwa lazima. Hata hivyo Trump amesema yeye hatovaa.

Trump amesema: "Nivae barakoa usoni wakati nina wasalimia marais, mawaziri wakuu, madikteta, wafalme na malikia – sioni hilo kufanyika."

Marekani na nchi nyingine wamegeukia masoko huria kuagiza vifaa vya afya na madawa kwa ajili ya wagonjwa na vifaa vya kujilinda wafanyakazi wa afya kutokana na maambukizi, wakishindana katika manunuzi kati yao na kusababisha bei kupanda juu zaidi.

**VOA**

# Waliofariki kwa corona duniani wafikia 60,000

**WASHINGTON, Marekani**

IDADI ya watu waliofariki kwa ugonjwa wa virusi vya corona duniani imefikia 60,000.

Kesi zilizothibitishwa na wagonjwa wa virusi vya ugonjwa huo nchini Marekani hadi kufikia juzi ilifikia watu 300,000.

Zaidi ya vifo vya watu 45,000 duniani kote vimetokea katika mataifa ya Ulaya, na kwamba Uingereza imeripoti kiwango cha juu cha vifo kwa siku, na kufikisha idadi ya vifo kuwa 4,300 kutoka jumla ya kesi za maambukizi 42,000.

Malkia wa Uingereza, Elizabeth wa pili, jana alihutubia taifa katika hotuba maalumu iliyolenga kuwataka watu kusimama na kupambana na changamoto hiyo pamoja na kuwashukuru wafanyakazi wanaowahudumua wagonjwa.

"Nina matumaini katika miaka inayokuja kila mmoja ataweza kujivunia ni kwa njia gani aliweza kupambana na changamoto hii,?" alisema Malkia Elizaberth.

Hadi kufikia jana kulikuwa na zaidi ya matukio milioni 1.2 yalithibitishwa ya mambukizi ya virusi vya corona duniani kote.

Rais Trump alisema kuwa Marekani haiwezi kuendelea kufungwa kutoka na tatizo la uwapo wa virusi vya corona.

"Mapambano dhidi ya virusi ni muhimu, lakini hatuwezi kuiharibu nchi yetu, nilisema tangu mwanzo , tiba haiwezi kuwa mbaya kuliko matatizo," alisema Rais Trump.

***DW***



Askari Polisi nchini Kenya, wakiwa katika doria wakihakikisha hakuna mwananchi anayetembea nje, baada ya kutolewa tangazo likiwataka wananchi kukaa ndani kwa siku 14 kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa corona. **PICHA: ALLIANCE**

# Yafahamu mataifa ambayo hayajapata maambukizi ya virusi vya corona

**LONDON, Uingereza**

JANUARI 12, mwaka huu ugonjwa wa virusi vya corona ulikuwa katika nchi ya China peke yake.

Na wakati huo hapakuwa na kisa hata kimoja kilichokuwa kimeripotiwa cha mgonjwa virusi vya corona nje ya nchi hiyo yenye wakazi zaidi ya bilioni moja.

Ilipofika Januari 13, mwaka huu virusi hivyo vikaanza kuwa tatizo la dunia, kisa cha kwanza kiliripotiwa nchini Thailand kabla ya Japan. Korea Kusini kufuata.

Hapo ndipo dunia nzima maambukizi yakaanza kushika kasi na idadi ya vifo vikaanza kuripotiwa. Hadi sasa kuna zaidi ya matukio milioni moja ya ugonjwa huo kote duniani.

Huku idadi ya vifo ikiongezeka na hospitali zikifurika wagonjwa, bado kuna mataifa ambayo hayajapata kabisa mgonjwa wa virusi vya corona.

Mataifa kama vile Visiwa vya Comoro; Kiribati; Lesotho; Marshall Islands; Micronesia; Nauru; Korea Kaskazini; Palau; Samoa; Sao Tome na Principe; Visiwa vya Solomon ; Sudan Kusini ; Tajikistan; Tonga; Turkmenistan; Tuvalu; Vanuatu, na Yemen, hadi sasa bado hayajaripoti kisa chochote cha mgonjwa wa virusi hivyo.

Hata hivyo, kuna baadhi ya visiwa vidogo vyenye wageni wachache ambavyo havitembelewi na watu kulingana na takwimu za Umoja wa Mataifa navyo bado havijaripoti tukio lolote na mgonjwa wa virusi hivyo.

Nauru, Kisiwa kilichopo katika bahari ya Pacific, kiko takriban maili 200 kutoka eneo lolote jingine - Kisiwa cha Banaba, sehemu ya Kiribati, ni kisiwa kilichopo karibu zaidi . Mji mkuu uliopo karibu ni Brisbane, uliopo maili 2,500 kusini -magharibi ambako inawabidi wasafiri kwa ndege kufika huko.

Kisiwa hiki kina takriban watu 10,000, ikiwa ni idadi ndogo zaidi baada ya ile ya wakazi wa Tulavu.

Ni moja ya maeneo ambayo yanatembelewa na watu wachache zaidi duniani. Ingawa hakionekani kwenye takwimu nyingi za hivi karibuni za UN, mmoja wa watu wanaoendesha shughuli za utalii anasema nchi hiyo hupata watalii 160 tu kila mwaka.

***BBC***

## HABARI KITAIFA

# Walia na biashara petroli majumbani

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

WANANCHI wa Kata ya Ulowa, Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamelalamikia uwekaji wa mafuta aina ya petroli kwenye mapipa katika makazi ya watu unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wa bidhaa hiyo, wakieleza kuwa ni hatari kwa usalama wao.

Wakizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, wananchi hao walisema wafanyabiashara hao wanahatarisha maisha yao kwa kuweka mapipa yenye mafuta katika nyumba wanazoishi ambazo zimezungukwa na makazi ya wanakijiji.

Mlekwa Kashindye, mkazi wa kata hiyo, alisema kumekuwapo na utaratibu huo wa uuzaji holela na uhifadhi wa ovyo mafuta ya petroli, unaohatarisha maisha ya wakazi na nyumba zao.

“Hatupingi kufanyika kwa biashara hiyo, tunachohofu ni madhara ambayo yanaweza kutupata yanayosababishwa na uhifadhi hafifu wa mafuta hayo, muda wowote yanalipuka na watu wengi hawajui kama yanahifadhiwa vibaya na wengine kuendelea kuvuta sigara karibu nayo,” alilalamika.

Diwani wa Ulowa, Paschal Mayenga, alisema mbali ya biashara hiyo kuhatarisha maisha ya wakazi, pia inafanyika kinyume cha sheria kwa kuwa wahusika hawalipi kodi kwenye Mamlaka ya Mapato (TRA) na ushuru kwenye halmashauri.

“Miaka ya nyuma kulikuwapo mtu mmoja aliyekuja kuweka mafuta nyumba ya wageni, lakini walitokea watu wawili waliokuwa wanaiba kwa kumimina na mwingine kutokea akiwa anavuta sigara, mlipuko ulisababisha watu wawili kufariki dunia na wengine wengi kujeruhiwa na nyumba kuteketea kwa moto, hivyo ni jambo la hatari,” alionya.

TRA wilayani Kahama ilifuatilia malalamiko ya wananchi hao na kukuta takribani mapipa 13 kwenye nyumba ya mfanyabiashara John Jaji anayeishi Kata ya Ulowa.

Jaji John, mtoto wa mmiliki wa mafuta hayo, alikiri bidhaa ya mafuta iliyokuwapo nyumbani ni mali yao, lakini akasistiza kuwa ni kwa ajili ya malori yao matatu.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, alisema Jeshi la Zimamoto na kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura), watafanya oparesheni kuwakamata wanaouza mafuta ya petroli kiholela au kuhifadhi karibu na makazi ya watu.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema wako katika oparesheni maalum ya kuwakamata watu wote wanaojihusisha na biashara hiyo kinyume cha sheria.

## Wapewa ndoo, redio kujikinga na corona

**Na Neema Emmanuel,MWANZA**

KATIKA kuhakikisha wananchi wanaoenda kupata huduma katika ofisi za Serikali za Mitaa wananawa mikono na maji tiririka ili kujikinga na ugonjwa wa corona sambamba kupata taarifa sahihi za a ugonjwa huo, Kata ya Lwanhima imepokea msaada wa ndoo 40 na redio 10.

Msaada huo wenye thamani ya Sh. 450,000, umetolewa na Shirika la Ni Hekima Pekee chini ya ufadhili wa Mwembe Association la Finland, kwa lengo la kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa msaada huo, Mkurugenzi wa Shirika la Ni Hekima Pekee, Onesmo Kajuna, alisema lengo la ndoo hizo ni kuwezesha ofisi za wenyeviti wa mitaa pamoja na wananchi wanaowahudumia wanawe mikono, hatua ambayo itasaidia kupata mbinu mbalimbali za kujikinga na ugonjwa huo.

Kajuna, alisema kipindi hiki ambacho Serikali imesitisha masomo kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo, wamewezesha redio 10 zinazotumia nishati ya jua (solar) kwa familia zenye mazingira hatarishi, ambazo hazina mawasiliano na zinahudumiwa na shirika hilo, kwa kuwa watoto wamefunga shule ili wao na wazazi wao waweze kupata taarifa.

Diwani wa Lwanhima, Ruben Kasanga, alisema anafurahi kwa kata yake kuletewa vifaa hivyo kwa ajili ya kusaidia wananchi wa mitaa 18 ili kujikinga na ugonjwa huo ulioikumba nchi na dunia, na kuwa watagawa katika mitaa yote na maeneo mengine ya kata hiyo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu, akimsikiliza Mbunge wa Hanang. Mary Nagu, alipofanya ziara katika Ziwa Basotu wilayani Hanang mkoani Manyara kujionea changamoto ya kufurika na kuzingira makazi ya wakazi wa eneo hilo na kuharibu miundombinu ya barabara. **MPIGAPICHA WETU**

# Bodi Maji Bonde Kati yawataka wananchi kuchukua tahadhari

**Na Dotto Mwaibale, SINGIDA**

KUTOKANA na mvua za masika zinazoendelea, Bodi ya Maji Bonde la Kati, imewataka wananchi wote waishio kwenye maeneo ya vyanzo vya maji kuchukua tahadhari na ikiwezekana kuondoka mara moja.

Lengo ni kujiepusha na majanga yanayoweza kujitokeza zaidi kwa kipindi hiki ikiwamo vifo.

Aidha, bodi hiyo imeanza rasmi kuweka alama za ukomo wa maji ya mafuriko kwenye maziwa ya Kindai, Munang na Singidani, ambazo zitasaidia kutambua hifadhi sahihi ya maziwa hayo kabla ya kuanza zoezi la kuongeza mita 60 ambazo zipo kwa mujibu wa sheria ya uhifadhi wa maziwa nchini.

Akizungumza wakati akikagua athari za mafuriko yaliyotokana na kupitiliza kwa ujazo wa maji kwenye maziwa ya Kindai na Munang mwishoni mwa wiki, Ofisa wa Maji, Bodi ya Maji Bonde la Kati, William Mabula, aliwataka wananchi wote waishio kwenye maeneo hatarishi ya vyanzo vya maji kuchukua tahadhari.

“Mvua hizi ni kubwa na huenda zikaendelea kunyesha kwa kipindi kirefu, niwatake tu wananchi waliojenga na hata wengine wanaoendeleza shughuli za kibinadamu kwenye maeneo haya ya chanzo cha maji wachukue tahadhari mapema kabla hatari kubwa zaidi hazijajitokeza,” alisema Mabula.

Alisema endapo mvua hizo zitaendelea kunyesha kwa kasi hiyo kulingana na utabiri unaotolewa na TMA, basi ni dhahiri maji nayo kupitia vyanzo na mikondo yake ya asili pia yataongezeka.

Akizungumzia kuhusu uwekaji wa alama kwenye maziwa ya Kindai, Munang na Singidani unaoendelea, Mabula alisema ofisi hiyo imeanza kuweka alama za muda mfupi sehemu ambazo maji ya mafuriko yanaishia, na wataendelea kusogeza alama hizo endapo maji yataongezeka.

“Tunaweka alama hizi ili zitusaidie kujua ukomo wa vyanzo hivi na hatimaye kuvihifadhi kwa usahihi, lakini pia zoezi hili litatupa taswira chanya hapo baadaye wakati wa kuongeza zile mita 60 ambazo zipo kwa mujibu wa sheria ya uhifadhi wa maziwa nchini,” alisema Mabula.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi wa ofisi hiyo, Nelea Bundala, alisisitiza kwamba kwa hali halisi ya mafuriko ilivyofikia kwa sasa suala la wananchi kuondoka kwenye maeneo ya vyanzo hivyo vya maji haikwepeki.

Alisema kwa mwaka huu mvua za masika zimekuwa juu ya wastani, na vyanzo vya maji karibu maeneo yote vimejaa, mathalani kwenye baadhi ya mabwawa na maziwa maji yameanza kupita kwenye utoro na yamekuwa ni mengi kuliko uwezo wa vyanzo vilivyopo.

“Niwaombe tu wananchi waanze kuchukua tahadhari ikiwezekana kuondoka maeneo haya kwa usalama wao...athari zake ni kubwa kama unavyotazama makazi ya watu yameendelea kuzama, shughuli za kibinadamu na miundombinu ya thamani kubwa vyote vimeathirika,” alisema Bundala na kuongeza:

“Tukiwa kama wasimamizi wa rasilimali za maji tunawasihi watu waepuke kuishi kwenye maeneo hatarishi yenye vyanzo vya maji, Kinachoonekana hapa sio kwamba maji yamevamia watu hapana. Haya maji yapo mahala pake pa asili na watu ndio wameyafata haya maji.”

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Stesheni, Kata ya Utemini, Juma Kanka, alisema mtaa huo ambao upo jirani na maziwa hayo umeathirika kwa kiasi kikubwa ikiwamo viwanda na miundombinu kadhaa kufunikwa kwa maji.

# Waiangukia serikali kusaidia kukamilisha ujenzi zahanati

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WAKAZI wa Kijiji cha Mapilinga Kata ya Igokelo wilayani Misungwi, mkoani Mwanza, wameiomba Serikali kuwaongezea nguvu ili kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wananchi wa Kijiji hicho, Restuta John, alisema shida wanayoipata kukosa huduma ya afya ya uhakika ambayo wanalazimika kuifuata katika hospitali ya wilaya hiyo iliyopo mbali.

Alisema kutokuwapo kwa kituo cha afya kunasababisha kinamama kujifungulia njiani au nyumbani, hivyo wanahitaji kupata kituo cha afya kwa kuiomba serikali kuwasaidia kumalizia jengo lao la kituo cha afya ili waweze kupata huduma hiyo katika kijiji chao.

Alisema ujenzi wa kituo hicho cha afya ulianza miaka mitano iliyopita kwa nguvu za wananchi, ambapo ukikamilika utasaidia kaya 525 kutatua changamoto inayowakabili ya kulazimika kufuata huduma ya afya vijiji jirani.

Mkazi mwingine wa kijiji hicho, Shamsa Mvamba, alisema kituo hicho ambacho walianza kujenga kwa zaidi ya miaka mitano, hadi sasa hakijakamilika kimefikia hatua ya mwisho.

Alisema kwa sasa wakienda hospitali ya wilaya wanaambiwa warudi zahanati ya kijiji jirani cha Ng'ombe na wakati mwingine wakifika katika zahanati hiyo wanaambiwa daktari hayupo, wakati huo wanakuwa wametumia gharama nyingi.

"Tulianzisha kujenga kituo chetu cha kijiji ambapo mpaka sasa tumekwama katika suala zima la umaliziaji, tunahitaji msaada wa kumalizia ujenzi pamoja na kupatiwa vifaa tiba na wahudumu wa afya ili na sisi tuweze kuondokana na adha hii inayotukabili kwa sasa," alisema Mvamba.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mapilinga, Sospeter Cornely, alisema jengo hilo ni la muda mrefu na kwamba nguvu ya wananchi ndiyo iliyotumika kuchimba msingi, kuujenga, kuinua boma na baada ya hapo wakapaua.

Alisema mpaka jengo hilo lilipofikia wananchi wamejitoa vya kutosha na sasa wanahitaji msaada wa serikali ili kumalizia.

Alisema vituo vya afya vipo mbali na wanalazimika kutembea umbali mrefu kufuata.

## Vijana Katoliki wapewa siri ya mafanikio

**Na Ndalike Sonda, Kahama**

VIJANA wa Kanisa Katoliki wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamehaswa kumtumainia Mungu katika maisha yao kwa kusali na kumwamini kwani ndiye muweza wa yote.

Paroko wa Parokia ya Kahama Mjini, Padri Salvatore Guererra, aliyasema hayo jana wakati wa ibada ya misa ya Jumapili ya matawi iliyofayika katika Kanisa kuu la Mtakatifu Karoli Lwanga.

Alisema vijana wanayo nafasi ya kumtumikia Mungu na kwamba waache kufuata mambo ya dunia, kukata tamaa na kubweteka badala yake wafanye mambo ya kumpendeza Mungu pamoja na kutumia elimu, ubunifu na maarifa walio nayo kwa manufaa ya jamii na kanisa kwa jumla.

Aidha, Padri Salvatore, aliwataka waumini kuzidi kumwomba Mungu kila wakati na mahali popote ili taifa liondokane na janga la virusi vya corona ambalo limekuwa tishio katika mataifa mbalimbali.

Alisema Mungu aliwapenda watu wake na hawezi kuwaacha waangamie, hivyo ni jukumu la kila mmoja kuendelea kusali na kumuomba, hasa katika juma la mateso, kufa na kufufuka kwa yestu Kristo ili Mungu asamehe dhambi za ulimwengu na hatimaye taifa lake lirejee katika hali ya amani na desturi ya awali.

**Alisema vijana wanayo nafasi ya kumtumikia Mungu na kwamba waache kufuata mambo ya dunia, kukata tamaa na kubweteka badala yake wafanye mambo ya kumpendeza Mungu pamoja na kutumia elimu, ubunifu na maarifa walio nayo kwa manufaa ya jamii na kanisa kwa jumla.**




Aliyekuwa Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Alex Kimbe (CHADEMA) ambae ni Diwani wa Isakalilo, akionyesha nyoka aina ya chatu, aliyemuua shambani kwake wakati akichunga mifugo, baada ya chatu huyo kumeza mbuzi juzi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Wauza pombe za kienyeji bila 'sanitizer' kufungiwa

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, amesema wafanyabiashara wa pombe za kienyeji mkoani hapa ambao watashindwa kutekeleza maagizo ya kijikinga na ugonjwa wa virusi vya corona, watafungiwa.

Dk. Nchimbi aliyasema hayo kwenye mkutano wa Baraza la Jumuiya wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Singida, uliohusu namna ya kujikinga na ugonjwa wa virusi vya corona.

Mkuu huyo wa Mkoa ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Mkoa huo, alisema katika kipindi hiki wauzaji wa pombe hiyo watatakiwa kuhakikisha kila mteja wanayemhudumia anakuwa na chombo chake cha kuwekewa kinywaji hicho, tofauti na ilivyozoeleka kwa kunywa pombe hiyo kwa kuchangia chombo kimoja.

"Kila mmoja anayetaka kufanya biashara hiyo ni lazima ahakikishe ananawa mikono yake kwa kutumia maji yanayotiririka na sabuni, kukaa mbali ni lazima... kila mmoja awe na chombo chake, hatuoni vibaya kama kila mtu atakuja na chungu sawa, atakuja na kopo haya na akija na sijui na kitu gani haya au hata akikutana na chupa akaikata sawa, cha msingi ni kila mtu awe na chombo chake," alisema Dk. Nchimbi.

Alisema kila muuzaji atalazimika kuwachotea pombe wateja wake na siyo kila mtu kuingia kwenye chombo kilichohifadhiwa pombe na kuanza kujichotea.

Dk. Nchimbi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa, alisema kwa mfanyabiashara ambaye hataweza kutekeleza maagizo hayo hawatasita kumfungia biashara.

Alisema kuwa kuwa hapatakuwa na ruhusa kwa wanywaji wa kinywaji hicho, kupokezana kama mbio za vijiiti na atakayetimiza masharti hayo ataruhusiwa kufanya biashara hiyo.

"Mgambo au jeshi la akiba watakuwapo imara wakiona tu dalili za hali ya kuzidiwa na kinywaji wanakutoa na akifanya upuuzi wa kutotii tunamchukulia hatua za kisheria, na hivyo ndivyo angalizo letu kwa watumiaji wa kinywaji hicho," alisema Dk. Nchimbi.

Kwa upande wao baadhi ya wajumbe wa UWT, waliishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuendelea kutoa elimu kwenye maeneo ya vijijini ambako kwa kiasi kikubwa bado elimu hiyo haijawafikia wananchi kwenye maeneo hayo.

Mwenyekiti wa UWT, Wilaya ya Manyoni, Blandina Mawala, alisema akiwa katika ziara zake wilayani kwake alishuhudia wanywaji wa pombe hiyo licha ya kunawa maji lakini wamekuwa wakichangia chombo kimoja kunywa pombe hiyo.

Naye Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Singida, Jenny Kessy, alisema kwamba corona ni ugonjwa hatari sana na kuwashauri kuwa kila mfanyabiashara ahakikishe wateja wake wananawa maji na sabuni kwanza kabla ya kuingia na kununua biadhaa wanazohitaji.



# CHELSEA YAJITOSA KUMSAJILI COUTINHO

**LONDON, England**

CHELSEA imeripoti kwamba imetoa ofa yake ya kwanza kwenye mbio za kumsajili Philippe Coutinho kipindi cha majira ya joto kijacho.

Kiungo huyo mshambuiaji alijiunga na Barcelona akitokea Liverpool kwa dili lililogharimu kiasi cha pauni milioni 145 miaka miwili iliyopita.

Mambo hayakwenda sawa kwa nyota huyo wa kimataifa wa Brazil na alishindwa kuonyesha kiwango cha kuvutia pale Nou Camp na akapelekwa kwa mkopo Bayern Munich kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Coutinho amekuwa na wakati mzuri nchini Ujerumani, lakini miamba hao wa Bundesliga hawana mpango wa kulipa kiasi cha pauni milioni 105 kilichopo kwenye mkataba wake ili kumchukua moja kwa moja.

Na hilo limezifanya klabu nyingi kuwania saini yake pamoja na Chelsea kuna Manchester United, Tottenham na Leicester.

Gazeti la Daily Mail limedai kwamba, Blues hao wamewasiliana na wakala wa mchezaji huyo, Kia Joorabchian, ambaye klabu hiyo ina uhusiano kubwa naye.

Na ingawa Barcelona haitakuwa tayari kukubali fedha kidogo kumuuza mchezaji wake huyo.

Kocha wa Chelsea, Frank Lampard ni shabiki mkubwa wa mchezaji huyo na anafedha za kufanya usajili baada ya kufungiwa kusajili kwa msimu mmoja.

## UNITED, SPURS KUBEBA NYOTA BOURNEMOUTH

**LONDON, England**

KLABU ya Bournemouth, inatarajia kuwauza wachezaji wake nyota kipindi cha majira ya joto ili kumaliza matatizo yao ya kifedha, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Tottenham na Manchester United ni miongoni mwa timu zinazowawania wachezaji wake kama Callum Wilson (pichani), Joshua King na David Brooks mwishoni mwa msimu huu.

Tangu ilipopanda Ligi Kuu mwaka 2015, mmiliki wake, Maxime Demin, alivunja benki kwa kufanya usajili wa gharama sokoni wakiwamo Jordon Ibe na Dominic Solanke lakini sasa anataka kuwauza ili kupunguza gharama zao.

Klabu hiyo itawapoteza Ibe na Ryan Fraser ambao wanaondoka wakiwa wachezaji huru kipindi cha majira ya joto, na Wilson na King wanaweza kuwafuata kwa kuuzwa kwa fedha nyingi wakati kocha, Eddie Howe, akipanga kukifumua kikosi hicho.

Wilson alijiunga na timu hiyo akitokea Coventry mwaka 2014 na aliisaidia klabu kupanda Ligi Kuu mwaka mmoja baadaye, akifunga mabao 91 katika mechi 249 licha ya kuumia mara mbili goti kwa kipindi hicho.

King, kinda wa zamani wa Manchester United, alikaribia kuuzwa Januari kwa pauni milioni 45 ili kutua kwa klabu yake hiyo ya zamani, hata hivyo, dau hilo lilikataliwa, lakini sasa njia ni nyeupe kwake.

# Roma yaingia vitani kumuwinda Gotze

**ROME, Italia**

AS Roma imejiunga kwenye mbio dhidi ya klabu kadhaa za Ulaya kumsajili kiungo wa Borussia Dortmund, Mario Gotze, kwa usajili huru kipindi kinachokuja cha majira ya joto.

Gotze anatarajia kuondoka Dortmund wakati mkataba wake utakapomalizika Juni 30, mwaka huu, huku timu kadhaa zikipigana vikumbo kuwania saini ya mshindi huyo wa Kombe la Dunia.

Kiungo huyo amefunga mabao matatu katika mechi 13 alizoichezea Dortmund msimu huu, lakini hawana mpango wa kumpa mkataba mpya.

Kwa mujibu wa gazeti la nchini Italia la Corriere dello Sport, wakala wa Gotze tayari amefanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Roma, Gianluca Petrachi.

Roma inakabiliwa na ushindani kutoka kwa timu za Ligi Kuu ya England Everton na West Ham, ambazo zimeonyesha nia ya kutaka huduma ya mchezaji huyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ana nia ya kutaka kubakia Ulaya, lakini pia kuna ofa ya fedha ndefu kutoka nchini Qatar na Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

Gotze alianza soka pale Dortmund, ambako alikuwa nyota chini ya Jurgen Klopp kabla ya kujiunga na wapinzani wao, Bayern Munich. Alifunga mabao 22 katika mechi 73 alizoichezea Bayern kabla ya kurudi Dortmund.



# VAN DE BEEK: BADO SIJAIKUBALIA MADRID

**AMSTERDAM, Uholanzi**

KIUNGO wa Ajax, Donny van de Beek, amesisitiza kwamba, mpango wa kujiunga na Real Madrid bado - huku akiifungulia mlango Manchester United.

Miamba hao wa Old Trafford, wameripotiwa kwamba wanawania kumtwaa Van de Beek ambaye taarifa za awali zilibainisha kwamba anaelekea nchini Hispania, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amebainisha kwamba majaliwa yake bado hayajajulikana.

Kwa mujibu wa ripoti Van de Beek tayari alishafikia makubaliano binafsi na miamba ya Ligi Kuu ya Hispania, Real Madrid na kwamba angejiunga nao mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi alikuwa akitajwa kujiunga na Madrid kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini alibakia Ajax baada ya miamba hao wa Hispania kushindwa kumuuza Gareth Bale au James Rodriguez.

Na wakati uvumi kuhusu uwezekano wake wa kutua pale Bernabeu ukiwa bado haujulikani, Van de Beek ameelezea kuhusu majaliwa yake.

"Kucheza kwenye jua mara zote ni vizuri, lakini bado sijaanza kujifunza Kihispania," alisema katika mahijoano na jarida la Helden.

"Bado sijasema "ndio" kwa yeyote, bado mlango upo wazi. Najua nini nilichonacho hapa, napendwa na Ajax na naipenda Ajax.

"Hisia zangu ni chanya kuhusu klabu, si kwa namna wanavyonipenda, lakini ni namna ninavyofiti kwenye mfumo wao wa uchezaji."

## Uefa kufutwa corona ikiendelea hadi Agosti

**MUNICH, Ujerumani**

SHIRIKISHO la Vyama vya Soka vya Ulaya (Uefa), limethibitisha kwamba fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya itafutwa kama mashindano hayatamalizika hadi Agosti 3, mwaka huu.

Ligi za soka barani Ulaya zimesimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona duniani kote.


Bado haijajulikana msimu wa 2019-20 unamaliziwa au utafutwa moja kwa moja barani Ulaya, lakini Rais wa Uefa, Aleksander Ceferin (pichani) ametoa siku ya mwisho ya mashindano ya Ulaya.

Ceferin amesema kupitia Televisheni ya Ujerumani ya ZDF: "Inatakiwa kumalizika Agosti 3, yote, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Europa.

"Tupo kwenye hali mbaya, tunabanwa na tarehe za kuanza kwa mashindano mengine. Kama tatizo litamalizika mapema, tunaweza tukaanza haraka."

Baadhi ya taarifa zinadai kwamba, mashindano hayo makubwa ya soka ngazi ya klabu barani Ulaya yanaweza kubadilishwa na kuchezwa kwa mtoano wa mechi moja moja na Ceferin amekubali kwamba, mfumo mpya unawezekana.

Aliongeza: "Tunaweza kucheza chini ya mfumo wa sasa, au kwa mchezo mmoja kwenye uwanja tofauti. Kwa sasa bado tunaangalia nini cha kufanya."



# Arsenal yajipanga kumtwaa Lingard

**LONDON, England**

ARSENAL inaonekana kama ndiko sehemu ambayo Jesse Lingard atatua kama akiondoka Manchester United dirisha la usajili linalokuja.

Kwa mujibu wa gazeti la The Athletic, 'ni ngumu kukataa' Arsenal inajaribu kumsajili Lingard kabla ya dirisha linalokuja la usajili, hasa kama Dani Ceballos anayecheza kwa mkopo hapo hawataweza kumpa mkataba wa kudumu.

Mwezi uliopita iliripitiwa kwamba, kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer amepoteza imani kwa Lingard, na ataridhia kuondoka ikiwa sehemu ya kukisafisha kikosi chake mwishoni mwa msimu.

Mkuu wa soka wa Arsenal, Raul Sanllehi, ametajwa kuwa amekuwa akiwasiliana na wakala wa Lingard, Mino Raiola.

Lingard hivi karibuni alisifiwa na mchezaji mwenzake, Paul Pogba kwa kuwa 'mchezaji mkubwa' akisema kwamba mara zote amekuwa akitoa mchango mzuri wa mabao katika mechi muhimu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alifunga bao la ushindi kwenye fainali ya Kombe la FA mwaka 2016 na Ngao ya Jamii, na mwaka 2017 alifunga kwenye fainali ya Kombe la Ligi, lakini amekuwa kwenye wakati mgumu tangu baada ya Kombe la Dunia mwaka 2018.

Amejikuta akikosa namba msimu huu baada ya kushindwa kufunga bao lolote wala kutoa pasi ya mwisho 'asist' kwa United mwaka jana na ujio wa Bruno Fernandes ndio umempoteza kabisa.

Wakati huo huo, Ceballos ameonyesha kiwango cha kuvutia chini ya Mikel Arteta wakati huu akicheza kwa mkopo kutoka Real Madrid, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amesema angependa kwenda Real Betis kuliko kubaki Arsenal.

Anatarajiwa kutosaini mkataba wa kudumu kipindi cha majira ya joto kinachokuja na Lingard anaonekana kama ndiye anayekwenda kuwa mrithi wake.

Lingard amecheza mechi 35 katika mashindano yote msimu huu, lakini amefunga mabao mawili tu.

Kama ataondoka klabuni hapo, watafanya haraka kwani mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2021.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI BORA DUNIANI- GUNDOGAN

●●●Kiufundi mara zote ni bora, lakini sasa ameimarika zaidi, namna anavyofunga mabao ni ya kuvutia...

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski amejitengeneza yeye mwenyewe "mshambuliaji aliyekamiliza zaidi duniani", kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa zamani wakiwa Borussia Dortmund, Ilkay Gundogan.

Wawili hao walicheza pamoja pale Dortmund kuanzia mwaka 2011 hadi 2014, kabla ya Lewandowski kuondoka na kwenda kujiunga na Bayern Munich.

Gundogan naye akiondoka BVB mwaka 2016 na kutua Manchester City, ambako anacheza na mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Sergio Aguero na mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus.

Lakini jicho lake amekuwa akilikodolea katika maendeleo ya Lewandowski na sasa anaona mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland yupo kwenye dunia tofauti ya soka.

Msimu huu Lewandowski mwenye umri wa miaka 31, amefunga mabao 25 katika mechi 23 za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, akiwa pale Bayern, na mabao 39 katika mashindano yote, kabla ya mlipuko wa virusi vya corona kusababisha ligi za Ulaya kusimamishwa.

"Ilikuwa furaha kubwa kucheza naye. Ameimarika tena," alisema Gundogan akiiambia Televisheni ya DAZN.

"Kiufundi mara zote alikuwa bora, lakini sasa ameimarika zaidi. Namna anavyofunga mabao ni ya kuvutia.

"Kwa upande wangu kwa sasa yeye ni bora, mshambuliaji aliyekamilika duniani."

Lewandowski hivi karibuni alibainisha kwamba Sergio Ramos na Cristiano Ronaldo walijaribu kumshawishi kusaini Real Madrid baada ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, miaka mitatu iliyopita.

## KWA UFUPI

**SOUTHGATE KUKATWA MSHAHARA**

KOCHA wa timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate amekubali kukatwa asilimia 30 ya mshahara wake kutokana na mlipuko wa virusi vya corona kuikumba duniani. ***(Sky Sports).***

**ARSENAL YAJIPAGA KWA FRASER**

KLABU ya Arsenal inajiamini kwamba itafanikiwa kumsajili winga wa Bournemouth, Ryan Fraser, mwenye umri wa miaka 26, wakati mkataba wake utakapomalizika kipindi kinachokuja cha majira ya joto. ***(Teamtalk)***

**SANCHO AMPA ULAJI COUTINHO**

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 20, kukataa kwake kusaini Chelsea kipindi kinachokuja cha majira ya joto kunaweza kukachangia nyota wa Barcelona, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 27, kuhamia pale Stamford Bridge. ***(Daily Mail)***

**SLIMANI KUTUA SPORTING**

STRAIKA wa Leicester, Islam Slimani mwenye umri wa miaka 31, anahusishwa na uhamisho wa kwenda Sporting Lisbon baada ya kushindwa kung'ara kwenye klabu yake hiyo ya sasa. ***(O Jogo)***

**LEICESTER KUTUA FENERBAHCE**

KLABU ya Leicester inajipanga kumsajili beki wa Fenerbahce, Hasan Ali Kaldırım, mwenye umri wa miaka 30, lakini watakabiliwa na ushindani kutoka kwa Galatasaray. ***(Hurriyet)***

**ARSENAL KUMSAJILI LINGARD**

ARSENAL inaweza kujaribu kumsajili kiungo wa Manchester United, Jesse Lingard, mwenye umri wa miaka 27, kabla ya msimu ujao, hasa kama wakishindwa kumbakisha Dani Ceballos mwenye umri wa miaka 23, anayecheza hapo kwa mkopo akitokea Real Madrid. ***(The Athletic)***

**KENNY HATAKI KURUDI EVERTON**

BEKI wa Everton, Jonjoe Kenny, mwenye umri wa miaka 23, anataka kubakia Schalke msimu ujao baada ya kufurahia kipindi chake cha kucheza kwa mkopo kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga. ***(Bild)***

**MORELOS AITESA RANGERS**

KLABU ya Rangers tayari imeweka orodha ya wachezaji ambao watamrithi mshambuliaji wao, Alfredo Morelos mwenye umri wa miaka 23, ambaye anatakiwa na klabu kadhaa za Ulaya. ***(Goal)***

**BERNARD AIKATAA ROMA**

WINGA wa Everton, Bernard mwenye umri wa miaka 27, amekanusha madai kwamba anaweza kujiunga na miamba wa Ligi Kuu ya Italia, AS Roma kipindi kinachokuja cha majira ya joto. (Liverpool Echo).

**WEST HAM YAMWANIA KOCH**

KLABU ya West Ham imejiunga kwenye mbio za kumwania beki wa kati wa Freiburg, Robin Koch mwenye umri wa miaka 23. ***(Daily Star).***

**NEWCASTLE YAMFUKUZIA SOUMARE**

KLABU ya Newcastle itajaribu tena kumsajili kiungo wa Lille, Boubakary Soumare, mwenye umri wa miaka 21, wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja baada ya kushindwa kukamilisha dili hilo Januari. ***(Sport).***

HABARI MICHEZO

# KOCHA AZAM FC ALIA NA MAZOEZI BINAFSI

**Na Saada Akida**

WAKATI majaliwa ya kurejea kwa Ligi Kuu Bara yakiwa bado hayajajulikana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Aristica Cioaba, ameendelea kulia na wachezaji kuonyesha nidhamu ya mazoezi binafsi ili kujiweka fiti.

Ligi Kuu imesimama kwa kipindi cha mwezi mmoja tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na agizo la serikali la kuzia shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ili kuepuka kasi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19).

Na kupitia mtandao wa klabu ya Azam FC, Cioaba amesema nidhamu ya mazoezi binafsi ndiyo silaha pekee kwa wachezaji kuwa fiti katika kipindi hiki ambacho ligi hiyo imesimama.

Alisema anafahamu wachezaji wake wapo katika wakati mgumu kufuatia klabu kusitisha maozezi ya pamoja kutokana na hofu ya maambukizi ya virusi vya corona.

"Najua huu ni wakati mgumu kwa wachezaji, wanatakiwa kuonyesha nidhamu ya hali ya juu katika mazoezi, hasa kwa kipindi hiki ambacho hatuna mazoezi ya pamoja na kucheza mechi," alisema.

Alisema wakati huu wakiwa nyumbani wanapaswa kufuata program maalumu ya mazoezi aliyowapa kwa nidhamu ya hali ya juu kwa kuwa anahitaji kupata urahisi wa kuiunganisha timu ikiwa na wachezaji fiti watakaporejea.

"Nadhani ni muhimu kwamba katika wakati huu mgumu tunaopitia kuonyesha umoja, mshikamano na uelewa, ninahitaji kuwa na nguvu zaidi katika siku zijazo, nawatakia kila mtu Tanzania na mashabiki wa Azam afya njema," alisema Cioaba.

Kocha huyo, amekuwa akitoa programu za mazoezi binafsi kwa wachezaji wake katika kipindi hiki wakiwa nyumbani kwa ajili ya tahadhari ya kuenea virusi vya corona.

Ligi Kuu ilisimama Simba ikiwa kileleni ikiongoza kwa pointi zake 71, ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 54 baada ya timu zote kucheza mechi 28, wakati Yanga ni ya tatu kwa pointi zao 51 za mechi 27 na Namungo ya nne ikiwa na pointi 50 za mechi 28.

## Kaheza aongeza kasi nyumbani

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akiwa msaada mkubwa kwa Polisi Tanzania katika nafasi yao ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 45 baada ya mechi 29, mshambuliaji Marcel Kaheza, amesema yupo katika program maalumu ili kuongeza makali ya ubora wake.

Hadi Ligi Kuu Bara inasimama ili kukwepa kasi ya maambukizi ya virusi vya corona, Kaheza ametupia mabao sita na pasi za mwisho nne, hivyo kuisaidia Polisi Tanzania kuwa hapo ilipo.

Kaheza alimwambia mwandishi wetu mwishoni mwa wiki kuwa kwa sasa anakitumia kipindi hiki kufanya mazoezi binafsi ili kulinda ubora wake.

"Tumepewa progamu na kocha ambayo ninaifuata kwa kuwa kipindi hiki ni muhimu kujilinda na kuchukua tahadhari pia kwa virusi vya corona," alisema huku akisisitiza mazoezi kwake ni kitu muhimu.

Bado haijajulikana majaliwa ya kurejea kwa Ligi Kuu Tanzania Bara licha ya kusalia siku 11 kabla ya mwezi mmoja ambao serikali iliagiza shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya wa tu ikiwamo michezo kote nchini kusimama ili kujikinga na kasi ya maambuzi ya virusi vya corona.




Nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta, akifurahia nje ya nyumbani kwake, Birmingham nchini Uingereza, anakoichezea klabu ya Aston Villa wakati huu Ligi Kuu ya England ikiwa imesimama kuepuka kasi ya maambukizi ya virusi ya corona (COVID19). **PICHA: MTANDAO**

## Matola awafunda wachezaji Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amewataka wachezaji wake kutokulala kipindi hiki na badala yake kuongeza kasi ya mazoezi binafsi.

Matola ambaye kwa kushirikiana na Kocha Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, wamerithi vema kijiti cha Patrick Aussems na msaidizi wake, Dennis Kitambi, amesema wachezaji ambao hawatafuata program walizopewa watarudisha nyuma maendeleo ya timu.

Bado haijajulikana majaliwa ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kufuatia agizo la serikali la kusimamishwa shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ili kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya corona. Hata hivyo, Matola alitoa wito huo kwa kuwataka wachezaji wote wa Ligi Kuu kuzingatia program ambazo wamepewa na makocha wao ili kulinda vipaji vyao pamoja na kutoziangusha timu zao.

**"Kwa wachezaji ambao watashindwa kufuata program ambazo wamepewa na makocha itakuwa ni kurudisha nyuma maendeleo ya timu kiujumla kwani wao ndio wanacheza kutafuta matokeo, wasipofanya mazoezi hawatakuwa bora.**

"Endapo ligi itarejea na wao hawajafanya mazoezi, itakuwa kazi nyingine kwa makocha kuanza kufundisha upya huku mechi zikiwa zimebaki chache ndani na ikumbukwe kuwa nyingine zipo kwenye hatari ya kushuka daraja," alisema.

Hadi Ligi Kuu inasimama, Simba ipo kileleni ikiongoza kwa pointi zake 71, ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 54 baada ya timu zote kucheza mechi 28, wakati Yanga ni ya tatu kwa pointi zao 51 za mechi 27 na Namungo ya nne ikiwa na pointi 50 za mechi 28.

# Chafu atoa sababu kutoibeba Mlandege

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KIUNGO wa timu ya Mlandege inayoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar, Ali Juma Chafu, amesema msimu huu kwa upande wake haukuanza vizuri kutokana na mfululizo wa mechi nyingi za msimu uliopita hali iliyomsababishia maumivu mwilini ya mara kwa mara.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, mchezaji huyo alisema msimu uliopita alicheza karibia mechi zote za Ligi Kuu Zanzibar akiitumikia timu yake hiyo hali iliyomsababishia muda mwingine kusikia uchovu na maumivu mwilini wakati anapokuwa uwanjani msimu huu.

Alisema timu yake hiyo ilikuwa ikimtegemea kuanza na kumalizia uwanjani uhususan msimu uliyopita hali iliyochangia msimu huu kushindwa kufanya vizuri kutokana na umri wake ambao amedai bado mdogo ikilinganishwa na majukumu aliyonayo katika timu hiyo.

Alisema anaamini kusimama kwa ligi hiyo kutokana na kuepuka maambukizi ya virusi vya corona kutatoa mapumziko mazuri ya mwili wake ikiwa ni pamoja na kujifua binafsi jambo ambalo litamsaidia kuwa fiti na ligi itakaporejea kuweza kuisaidia timu yake.

"Kipindi hiki mimi nakitumia kwa kupumzisha mwili wangu, muda mwingi nafanya mazoezi nikiwa nyumbani ili ligi itakapoanza basi nitakuwa vizuri na naamini nitafanya tena vizuri kama ilivyo kwa msimu uliopita," alisema.

Mlandege ipo nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 44 baada ya mechi 20.

# Michezo

Jumatatu Aprili 6, 2020

Nipashe



## Lewandowski bora duniani- Gundogan

HABARI UK 30

ANAWASIKILIZIA...



Kiungo wa zamani wa Simba, James Kotei, wakati akiitumikia Kaizer Chiefs kwa sasa FC Slavia-Mozyr ya Belarus. Kotei anahusishwa na kurejeshwa Simba msimu ujao. **PICHA: MTANDAO**

# KOTEI AFUNGUKA KURUDI SIMBA SC

Awataja mashabiki, wachezaji na viongozi Msimbazi huku akisema kama Yanga...

**Na Saada Akida**

HUKU mashabiki wa Simba wakitaka aliyekuwa kiungo wao mkabaji, James Kotei, arejeshwe msimu ujao kuitumikia timu hiyo iliyopo kileleni mwa Ligi Kuu Bara msimu huu, lakini pia akielezwa kuviziwa na mahasimu wao wa jadi, klabu ya Yanga, Mghana huyo amefunguka sababu zinazoweza kumrejesha.

Awali zilienea tetesi kuwa Kotei yupo mbioni kurejea Ligi Kuu Bara na huenda akatua Simba ama Yanga, baada ya klabu hizo kila moja kudaiwa kuhitaji huduma yake, lakini kiungo huyo amesema endapo hilo litatokea basi atawapa nafasi zaidi timu yake hiyo ya zamani ya 'Wekundu wa Msimbazi'.

Kotei anayeichezea FC Slavia-Mozyr ya Belarus, baada ya mapema mwaka huu kusaini mkataba wa mwaka mmoja, alisema kipindi akiitumikia Simba mashabiki wa timu hiyo walionyesha mapenzi makubwa kwake, hivyo atalazimika kuipa nafasi zaidi kama akiamua kurejea kucheza soka Tanzania.

"Muda ukifika kila kitu kitakuwa wazi, lakini kwa sasa akili yangu ipo Slavia-Mozyr, ukifika muda huo ninaimani itakuwa Simba kwanza, nilipokuwa hapo nimeishi vizuri kuanzia na wachezaji, viongozi hata mashabiki," alisema Kotei.

Alisema kutokana na hali hiyo Simba watakuwa katika nafasi ya kwanza kurejea endapo muda wa kurudi kucheza soka Tanzania utafika.

Kiungo huyo alisema bado anakumbuka mapenzi ambayo alionyeshwa na Wanasimba kipindi ambacho aliichezea timu hiyo na kufanikiwa kuchangia kupata ubingwa wa Ligi Kuu na kufikia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kotei ambaye alitua Slavia Mozyr akitokea Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, aliyojiunga nayo baada ya kumaliza mkataba na Simba, alitengeneza 'kombinesheni' nzuri na Jonas Mkude katika safu ya kiungo wakati akiwatumikia Wekundu wa Msimbazi hao.

Tangu kuondoka kwa Kotei safu ya kiungo mkabaji ya Simba haijatulia, huku kwa nyakati tofauti makocha wa timu hiyo wakiwajaribu Mzamiru Yassin na Mbrazil Gerson Fraga ambao wameshindwa kutengeneza kombinesheni nzuri na Mkude.

## Athari 6 Ligi Kuu Bara ikifutwa

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI virusi vya corona (COVID-19), vikiitesa dunia, bado mashabiki wa soka wamekuwa na mijadala mbalimbali juu ya mustakabali wa ligi duniani.

Tayari nchini Ubelgiji ligi ya nchini humo imefutwa na klabu iliyokuwa inaongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo, Club Brugge ikitawazwa kuwa mabingwa,

UK.18




## Kwa nini Ceballos abakishwe Arsenal?

**LONDON, England**

JE, Dani Ceballos amefanya ya kutosha hadi anunuliwe kwa kitita cha fedha ndefu Arsenal? Ana uwezo wa kuziba pengo la Aaron Ramsey? Kuna nafasi ya kumsajili mwingine zaidi ya yeye?

UK. 20



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >